**4 NOVEMBA, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Nne – Tarehe 4 Novemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Kunusuru Barabara Wilayani Kyela**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati wa kukarabati barabara zilizo katika hali mbaya Wilayani Kyela kwani bajeti ya TARURA haitoshi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kunusuru barabara ambazo zipo katika hali mbaya sana Wilayani Kyela, Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kuzipandisha hadhi barabara za udongo kwenda changarawe *(Gravel standard*);

(ii) Kuzipandisha hadhi barabara za changarawe kuwa barabara za lami;

(iii) Kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara, mfano, bajeti ya TARURA Kyela kwa mwaka 2020/2021 ilikuwa Sh.611,136,079.47; mwaka 2021/2022 bajeti ya Kyela ilikuwa ni Sh.2,436,996,341.18; na

(iv) Kuendelea kutoa fedha za dharura kunusuru barabara zilizoathiriwa na mvua, mfano, katika mwaka 2021/2022 zimepelekwa milioni 901.52.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa kwa maelekezo maalum ni kwa ajili ya kutatua changamoto

za muda mfupi za barababara zilizoathiriwa na mvua ili ziweze kupitika kwa wakati huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Swali la kwanza; kwa kuwa Kyela ni sehemu ambayo ina mvua nyingi sana na huwa inakumbwa na mafuriko kwa kipindi kila mwaka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta fedha ambazo zimekosekana kwa muda mrefu kwa maendeleo ya barabara Wilayani Kyela?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa inajulikana barabara haziwezi kudumu kwenye mafuriko hasa hizi za changarawe na udongo. Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa kutafuta namna nyingine ya ujenzi wa barabara kwa mfano, kutumia *enzymes* katika kitengo chake cha utafiti hapo *TARURA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya barabara na nimwondoe shaka tu. Bahati nzuri Serikali sasa hivi imeongeza bajeti yake na sisi tumekuwa

tukitekeleza vya kutosha. Kwa hiyo, hilo aondoe shaka kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tafiti katika maeneo ambayo barabara hazidumu kutokana na mvua nyingi kama ilivyo Kyela, utafiti huo umefanyika na moja ya mipango yetu ni kuja na majibu ambayo yatasaidia barabara za maeneo hayo ziweze kupitika muda wote. Kwa hiyo, Serikali ipo kazini na inafanya hii kazi kwa umakini kabisa ili kuwasaidia wananchi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Barabara ya Igalukilo – Badugu – Nyaluhande – Sayaka – Bubinza Kuhamishiwa TANROADS**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara ya kutoka Igalukilo - Sayaka inayounganisha Mikoa ya Mwanza na Simiyu itahamishiwa *TANROADS*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara, Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009, imeainisha vigezo na utaratibu wa kuhamisha barabara ili iwe chini ya *TANROADS* ambapo barabara inaweza kupandishwa au kuteremshwa toka daraja moja kwenda daraja lingine.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaielekeza Halmashauri ya Wilaya Busega kupitia *TARURA* kufuata utaratibu huo ili kuiweka barabara hiyo katika mpango wa kupandishwa hadhi na kuwa ya mkoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa zoezi hili alilolisema Mheshimiwa Waziri hapo awali lilishawahi kufanyika na halikuwa na mafanikio na barabara hii ni muhimu sana kwa Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mwanza. Je, nini maelekezo yake ya haraka kwa wafanyakazi wa *TARURA* ili zoezi lifanyike haraka ili tuweze kuunganisha barabara hii katika mikoa hii miwili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeshatoa maelekezo kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Busega kupitia *TARURA* waanze mara moja mchakato huo ili nia ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka huduma kwa wananchi na nia ya Mbunge wa jimbo lile kuhakikisha barabara hiyo inapitika muda wote ifikiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maelekezo haya nimeshayatoa na nayarudia tena na nitakuwa wa kwanza kuyafuatilia maelekezo hayo ili yaweze kutekelezeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. Tuna Barabara ya kutoka Makambako – Mlowa – Kifumbe ambako inakwenda kutokezea kule Ilunda. Barabara hii tumekuwa tukiiomba ipandishwe hadhi na kuwa ya *TANROADS* na kwa kuwa kule mbele inakotokezea barabara hii tayari ni ya *TANROADS*. Je, kwa nini sasa barabara hii inakoanzia isiwe ya *TANROADS* ikaunga na kule mbele ambako inatokea kwai le iliyo ndani ya *TANRAODS*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa maelekezo katika swali la msingi la Mbunge wa Jimbo la Busega, niielekeze vilevile Halmashauri ya Makambako na Mkoa wa Njombe, kuhakikisha wanaanza na wao mchakato rasmi sasa ili barabara hii na yenyewe watu wa *TANROADS*, wakishapitisha vile vigezo vyao na wakaona inakidhi, iweze kupandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa ili iweze kusaidia wananchi wa eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara ya kutoka Bashineti – Lukumanda – Seche – Basodeshi – Ibadalu – Zinga, kutoka *TARURA* Kwenda *TANROADS*? Kwa sababu barabara hii upande wa Singida iko *TANROADS* na upande wa kutoka Babati kwenda Mbulu iko upande wa *TANROADS*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maelekezo yetu katika halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Hanang na mikoa yote, ni kuhakikisha zile barabara

ambazo zinaunganisha kati ya halmashauri moja na nyingine, mkoa mmoja na mwingine ambazo zinaangukia katika upande wa *TARURA* ili ziunganishe mkoa, ni kuanza mchakato wa kuhakikisha sasa zinakuwa na vigezo vya kupandishwa hiyo hadhi.

Mheshimiwa Spika, maelekezo yangu kama katika swali la msingi na kwa Waheshimiwa Wabunge ni hayo na tutafuatilia maelekezo hayo kwa nia moja tu ya kutaka kuwasaidia wananchi katika maeneo yenu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara inayotoka Mangaka Wilaya ya Nanyumbu - Nachingwea Tarafa ya Kilinalondo - Liwale katika Kata ya Ilombe, tumeshaiombea iingie *TANROADS,* lakini mpaka leo tunapigwa danadana.

Je, ni lini barabara hii itaweza kupandishwa hadhi kuwa barabara ya *TANROADS* kwa sababu barabara hiyo imepita katika wilaya tatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ameshasema Mheshimiwa Mbunge walishaomba na mchakato upo katika ngazi husika na wenye jukumu la kufanya hivi ni watu wa *TANROADS*, naamini sisi Serikali ni moja tutalifuatilia ili kuharakisha huo mchakato uweze kukamilika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itamalizia kipande kilichobakia kwenye Kawawa Road kufikisha Marangu Mtoni kwa hadhi ya lami, tulipewa ahadi na Mheshimiwa Rais Kikwete awamu zile na iko kwenye Ilani ya CCM?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimwondoe hofu kwa sababu tumeshajenga awamu ya kwanza na kilichobaki nikumalizia katika eneo la pili na uzuri barabara hii iko katika mipango ya *TARURA*. Kwa hiyo, kwa sasa tunatafuta fedha tutakapopata mara moja naamini kabisa kwa sababu iko katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi barabara hii tutaitengeneza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Mchakato wa kupeleka barabara za *TARURA*, kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* ni barabara ya kutoka Bukama – Mikulusanga – Mikomalilo tulishafanya mchakato na umekamilika. Sasa hoja ya kujiuliza ni kwamba *TANROADS* na *TARURA* wakitaka kupeleka barabara, vigezo vya kuwapelekea *TANROADS* wanasema sisi mpaka tupelekewe na Wizara. Sasa ni lini muunganiko huu wa *TARURA* na *TANROADS* utakuwepo ili barabara za *TARURA* ziondoke kwenye *TARURA* ziende *TANROADS*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMImajibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna muunganiko mzuri kati ya *TANROADS* na *TARURA* na tunafanya kazi kwa kushirikiana pamoja. Kwa hiyo, kinachofanyika tu ni kwamba kwenye zile barabara ambazo ziko chini yetu, huwa tunazipeleka kwao na wao wanaangalia vile vigezo vinavyostahili. Kwa hiyo, siyo kwamba wana nia ya kuchelewesha hizo barabara, ni kwa sababu wanaangalia vile vigezo, vikashakamilika

wanatafuta fedha na ndiyo wanatangaza hizo barabara na kuwa za mkoa.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuimarisha ushirikiano wetu ili haya maswali ya Waheshimiwa Wabunge tuweze kuyajibu kwa wakati na kwa urahisi zaidi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Athari Itokanayo na Mafuriko – Mto Mbezi**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, kuna Mkakati gani wa kukabiliana na mafuriko katika Mto Mbezi yanayosababisha uharibifu wa miundombinu ya shule na makazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Hamza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazotokana na mafuriko katika mito yetu nchini ukiwemo Mto Mbezi. Kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali imeandaa Mwongozo wa usafishaji mchanga, tope na taka ngumu kwenye mito na mabonde katika Mkoa wa Dar es Salaam wa Mwaka 2021. Mwongozo huu unalengo la kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kusafisha tope na mchanga kwenye mito na mabonde ili kuruhusu uwepo wa mtiririko mzuri wa maji kuelekea baharini ili kuepuka athari za mafuriko.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kumhakikishia Mbunge kuwa, itaendelea kuimarisha utekelezaji wa Mwongozo ili kutatua changamoto ya mafuriko katika mito na mabonde yaliyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kukabiliana na madhara ya mafuriko na kuhakikisha miundombinu ya shule na makazi ya watu yanaendelea kuwa salama. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya jumla ya Serikali kwenye changamoto hii kwamba imeandaa mwongozo wa usafishaji mchanga, kutoa tope na taka ngumu. Hili ni jukumu ambalo halmashauri yetu ya Manispaa ya Ubungo imeshafanya sana, lakini madhara ni makubwa sana kwenye mto ule, unazidi kupanuka na kuvunja shule na taasisi za Serikali pamoja na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, inawezekana changamoto hii inahitaji Wizara ya kisekta ingejibu. Naomba niruhusu

niulize maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza; je, Serikali itakuwa tayari kujenga kingo imara kwenye Mto wote huo wa Mbezi ili madhara haya yaweze kuondoka?

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri husika atakuwa tayari kwenda nami jimboni ili tuutembelee mto na aone madhara ambayo yametokea kwa wananchi na yatakayotokea kwenye siku zijazo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya miongoni mwa jukumu letu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kuhakikisha kwamba tunazingatia na tunashughulikia masuala ya vyanzo vya maji ili visiathiriwe na visiathiri wananchi. Niko tayari kufuatana na yeye kwenda kutembea katika Mto Mbezi kuona changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake lingine, Ofisi ya Makamu wa Rais, Serikali tuko tayari kuhakikisha kwamba tunajenga huo mradi wa ukuta ambao utatenganisha ili sasa maji yasiweze kuingia huko yakaleta mafuriko. Ila namwomba Mheshimiwa Mbunge yeye kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kwanza wafanye tathmini ya ujenzi huo, lakini kingine waandike halafu watuletee Ofisi ya Makamu wa Rais ili tuone namna ambavyo tunaweza tukapata fedha kwa ajili ya kuandaa mradi huo. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Kumaliza Mgogoro wa Wananchi na Mwekezaji wa Madini Kata ya Guta – Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza**:-**

Je, kuna mpango gani wa kumaliza mgogoro kati ya Wananchi na Wawekezaji wenye leseni ya uchimbaji madini Kata ya Guta – Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro uliopo unahusisha wamiliki wa mashamba waliojichukulia haki madini *(Mineral Rights)* bila kufuata sheria kwenye eneo ambalo leseni zilikwishatolewa kwa mwekezaji aitwaye *JB & Partners* ambaye alipewa leseni ndogo za uchimbaji (*PMLs*) nane (8). Leseni hizi zimo ndani ya mashamba 21

ya wakazi wa maeneo ya Mtaa wa Stooni, Kata ya Guta Wilaya ya Bunda. Mpango uliopo ili kumaliza mgogoro huo ni kuendelea na majadiliano ili kufikia maridhiano kati ya wamiliki wa mashamba hayo na mwekezaji aliyepewa leseni. Hadi sasa kupitia majadiliano wamiliki wa leseni wamekwishaingia maridhiano na kusaini makubaliano ya uchimbaji kwa ubia na wamiliki wa mashamba 13 kati ya 21 wanaotambulika katika eneo hilo la uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mashamba 13 mgogoro wake ulifika tamati na machimbo kufunguliwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mara mnamo tarehe 6 Oktoba, 2022 na shughuli za uchimbaji zinaendelea. Wamiliki wa mashamba nane waliobaki waliogoma kufanya majadiliano na walifungua kesi ya ardhi *(Land Case No. 12 of 2021)* katika Mahakama ya Musoma ambayo inaendelea kusikilizwa. Hata hivyo, wamiliki wa mashamba hayo nane wamepatiwa nafasi nyingine ya majadiliano na katika maeneo yao uchimbaji umesimamishwa hadi pale watakaporidhiana. Endapo watashindwa kuridhiana ndani ya muda uliowekwa kwa mara nyingine basi taratibu nyingine za kisheria zitafuatwa kwa mujibu wa Kifungu cha 97 cha Sheria ya Madini, Sura 123. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Maboto swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kati ya hawa 21 hawa Nane ndiyo wako kwenye *source* ya eneo lenyewe la uchimbaji, ndiyo maana hawajakubaliana na masharti ya wale Wawekezaji. Wizara ningewaomba wao wafanye kila

linalowezekana ili kuwaweka vizuri, kwa sababu wale mashamba Nane waliobaki ni kwa sababu hawaoni kama wanapata haki zao zinazowastahili.

Swali la pili, ningeomba Mheshimiwa Waziri mara baada ya Bunge hili kuisha tuende nae mpaka kwenye eneo la tukio ili akajiridhishe yeye mwenyewe. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali lake la kwanza, kama nilivyokwishasema katika jibu langu la msingi, kwamba Mahakama imetoa fursa waendelee kujadiliana na endepo majadiliano hayo hayatazalisha ridhaa na wao waingie kwenye ubia kama wenzao, taratibu za kisheria, Sheria ya Madini Sura ya 123, Kifungu cha 97 kinachoeleza jinsi ambavyo suala la *compensation, reallocation* na *resettlement,* yaani fidia au kuhamishwa na kuwekewa sehemu mbadala au kujengewa makazi mengine utafuatwa kwa ushirikiano na Wizara ya Ardhi na Mthamini Mkuu wa Ardhi wa Serikali. Kwa hiyo, tumejipanga katika kuhakikisha kwamba maridhiano ama yafikiwe au sheria ifuatwe ili madini hayo yenye thamani katika maeneo hayo yaweze kuchimbwa na kunufaisha Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali lake la pili, ni mtu wa *field* sana niko tayari baada ya Bunge hili tutapanga ratiba pamoja nae, tuone siku muafaka

ambayo naweza kufika ili tukashuhudie maeneo hayo na kumaliza mgogoro uliopo. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia stahiki wananchi wa mitaa ya Mwasonga, Madege na Sharifu wanaoguswa na mradi wa uchimbaji wa madini ya mchanga kupitia Kampuni ya Nyati katika Wilaya ya Kigamboni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna kampuni ya uchimbaji wa madini ya mchanga mzito unaitwa *heavy sands* katika Jimbo lake, na kampuni husika inaitwa Nyati na hivi sasa ninavyojibu swali lake majedwali yote ya malipo ya fidia yameshakamilishwa, wapo watakofidiwa wapatao 1,198 na Mdhamini Mkuu wa Serikali ameshamaliza kazi yake na hivyo mpango wa malipo yao unaweza ukafanyika ndani ya miezi miwili ijayo. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naulizia kuhusiana na eneo la Bunda. Eneo lile limekua ni muhimu sana kwa maisha na uchumi wa wachimbaji wadogo wadogo katika Wilaya yetu ya Bunda.

Je, kwa nini Serikali isiende pale na kulikata lile eneo ili sehemu nyingine ibakie kwa wachimbaji wadogo wadogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la rafiki yangu Mheshimiwa Charles, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Madini, kazi yetu ni kusimamia Sera, Sheria na Kanuni. Wawekezaji wa machimbo ya madini wawe wa ndani au wa nje, kazi yetu ni kuwasimamia na inapotokea kwamba eneo lina maslahi mapana ya Kitaifa na wenye eneo wamegoma kabisa kutoa ushirikiano, tunachofanya ni kufuata sheria zilizowekwa za huo utaratibu unaobainishwa katika Kifungu cha 97 cha Sheria yetu ya Madini Sura ya 123, kwa kuangalia suala la fidia, suala la kuhamisha watu na kuwapangia makazi mengine kwa mujibu wa sheria ambayo inashirikisha Wizara ya Ardhi pia, Sheria ya Vijiji au Sheria nyingine inayohusika na masuala ya ardhi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Hitaji la Kituo cha Forodha Mpaka wa Olaika – Ngorongoro**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Forodha katika mpaka wa Olaika Wilayani Ngorongoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Chande majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, *TRA* ilifanya utafiti katika maeneo yote nchini yenye uhitaji wa Ofisi za kudumu za usimamizi wa kodi ikiwemo mpaka wa Olaika Wilayani Ngorongoro na kubaini kuwa gharama za usimamizi wa shughuli za forodha katika mpaka wa Olaika zitakuwa kubwa ikilinganishwa na kiwango cha ushuru wa forodha unaotarajiwa kukusanywa. Kwa muktadha huo, *TRA* itaendelea kufuatilia mwenendo wa ukuaji wa shughuli za forodha katika mpaka huo ili kufungua kituo cha forodha cha kudumu. Aidha, *TRA* itaendelea kuimarisha mfumo wa sasa wa kuhudumia mpaka huo ili kuwawezesha wananchi kuendesha shughuli zao za kibiashara kwa ufanisi zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa una swali la nyongeza au umeridhika na majibu. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina uhakika kwamba tathmini ya mwisho kufanyika katika eneo hilo ni mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, basi naomba kumuomba Mheshimiwa Waziri kama inawezekana ili kuthibitisha yale anayoyasema tuongozane akaongee na wafanyabiashara wa Wilaya ya Ngorongoro ambao ndio wahitaji wa kituo cha forodha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla ya kujibu swali hilo naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia na kufanyia kazi katika Jimbo lake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania ni Serikali sikivu sana. Kwa hiyo, niko tayari kufuatana na yeye Mheshimiwa Mbunge kwenda katika eneo hilo na kuona uwezekano na kuongea na wananchi na wafanyabiashara kwa jumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi – Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika Mji wa Kilwa Masoko?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi. Mkataba wa ujenzi wa Bandari hiyo ulisainiwa tarehe 07 Juni, 2022 kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya *M/S China Harbour Engineering*. Aidha, maandalizi ya awali ya ujenzi wa Bandari hiyo yameanza na ujenzi unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kufuatia ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, wananchi wa Kilwa Masoko tumeandaa eneo la kutosha kwa ajili ya sekta mbalimbali. Je, Serikali sasa iko tayari kuhakikisha kwamba sekta rafiki au taasisi rafiki na bandari ya uvuvi kama vile Chuo cha Uvuvi, viwanda vya kuchakata samaki pamoja na soko la samaki vinajengwa Kilwa Masoko?

Swali la pili, wapo wananchi wapiga kura wangu ambao wamefanyiwa tathmini ili kupisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi wakiwemo Ndugu Mwanawetu Zarafi, Ndugu Fatima Mjaka, Ndugu Fadhila Sudi pamoja na Ndugu Suleiman Bungara (Bwege) na wenzao 50.

Je, ni lini Serikali itakwenda kulipa fidia kwa wapiga kura wangu hawa.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza naomba nimhakikishie kuwa ujenzi wa bandari hii kubwa ya mfano na ya kielelezo katika Taifa letu inaendana na yote aliyoyasema ya uwepo wa miundombinu wezeshi. Kwa hivyo, nataka nikuhakikishie ya kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeliona jambo hili na nikipaumbele

chake. Kutakuwepo na soko, patakuwepo na maghala ya kuhifadhia bidhaa za chakula, kutakuwepo na miundombinu mingine yote inayoendana na hadhi ya bandari ya uvuvi ya kisasa na ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni hili la tathmini naomba nilichukue jambo hili kwa kuwa jambo hili tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kwa maana ya Mamlaka yetu ya Bandari *(TPA)*, kwa hiyo nataka niwahakikishe nalichukua hili jambo nakwenda kulisimamia kuhakikisha kwamba wananchi hawa waweze kupata haki yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki katika Ziwa Duluti kwa lengo la kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kule Arumeru Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan ilitenga kiasi cha Shilingi Bilioni 20 kwa ajili ya kuanza mradi maalum wa vizimba vya Samaki. Vilevile tunao

mradi kwa ajili ya maeneo ya ufugaji samaki nje ya vizimba kwa maana ya mabwawa. Naomba niseme tu kuwa Ziwa Duluti tutalifanyia tathmini ikiwa kama ni katika maeneo yenye kuweza kufanyiwa shughuli hizi za vizimba katika mwaka mwingine wa fedha tutaliwekea mpango na lenyewe, kwa sababu siyo kila mahali tunaweza kujenga vizimba kulingana na taarifa za kitaalam. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Barabara ya Turiani – Handeni**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, ni lini kipande cha barabara ya Turiani hadi Handeni kitajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote kutoka Magole - Turiani – Mziha hadi Handeni yenye urefu wa kilometa 147.7. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Magole – Turiani (Km 45.27) umekamilika na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha ujenzi wa sehemu iliyobaki ya Turiani - Mziha – Handeni yenye urefu wa kilometa 102.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naishukuru Serikali kwa barabara hii ya kuanzia Magole hadi Tuliani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jibu hili limekuwa la muda mrefu tangu 2010 mpaka sasa hivi mnaendelea hivyo hivyo, ndiyo jibu hilo hilo na kipande ni kilomita102 tu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti kwenye kipande hiki cha Km 102 kwenye bajeti ijayo?

Swali langu la pili; je, barabara ya Lupilo mpaka Mahenge ni lini nayo itajengwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaanza kuijenga hii barabara hizo kilomita na hata katika bajeti ya mwaka kuna fedha imetengwa kwa ajili ya barabara hiyo, lakini Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa iko kwenye mpango tunaweka katika miaka inayokuja ya bajeti tutaendelea kutenga fedha ili kuikamilisha barabara yote hii.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kwa barabara ya Lupilo – Mahenge, barabara hii ni kati barabara kuu kwa maana ya *trunk road* na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wako Wakandarasi ambao tayari wameshapita Lupilo – Mahenge kwa ajili ya kuangalia kama itajengwa kwa mpango wa *EPC*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii pia Serikali inategemea kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Iringa kwenda Ruaha *National Park*, tayari ilishapewa fedha kwa maana zile fedha za mkopo.

Je, ni lini sasa Serikali itatangaza *tender* ili hiyo barabara ianze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya kwenda Ruaha *National Park* Lusembe ina Kilomita 104 na inafadhiliwa na *World Bank*. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zote za kuandaa zabuni zimeshakamilika na muda wowote itatangazwa kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami barabara yote. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mkuyuni kupita Maina mpaka Mwatex yenye Km 11 tayari usanifu wake umekamilika.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo kwa lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Furaha, Mbunge wa Viti Maalum – Mwanza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ya Mkuyuni hadi Maina imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, Wizara ya Ujenzi kwa kusaidiana na TAMISEMI

tunatafuta fedha ili kuijenga barabara hii muhimu ambayo pia itakuwa kama *bypass* ya kuingia Mjini Mwanza. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea, kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njiapanda - Rugali – Ndembe – Longa Km. 10, kwa mbele kuna lami lakini kipande hiki hakina lami. Je, ni lini Serikali itaunganisha kipande hiki kutoka Mbinga Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoisema ni kweli ilijengwa mbele kwa sababu ya changamoto ya huko ilikojengwa ili kuhakikisha kwamba inapitika. Sasa hivi nimuhahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha hiko kipande kilichobaki kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilitaka kuuliza, kwa kuwa mchakato wa ujenzi wa barabara inayotoka Kakola kwenda Kahama umekalimika. Sasa ni lini na nini kimekwamisha Wizara kutangaza barabara hiyo ili ianze ujenzi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge tumekutana naye sisi na Wizara lakini pia na watendaji wa *TANROADS.* Ni barabara ambayo kweli fedha imeshapatikana, taratibu zinaandaliwa ili kuitangaza barabara hiyo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo mwaka huu wa fedha itaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Babati-Galapo-Kimtoro hadi Kibaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba, sijamsikia Mheshimiwa Mbunge, barababara aliyoitaja, kuanzia Babati na inapokwenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Babati-Galapo-Kimtoro hadi Kibaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum Manyara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Babati-Galapo kwenda Kibaya, tuanakamilisha usanifu wa kina; na mwaka huu itakamilika na baada ya hapo Serikali itaanza kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa sasa usanifu wa kina unaendelea kukamilishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya kutoka Mnivata-Tandahimba-

Newala-Masasi kilometa 160 tunafahamu kwamba fedha zake zimepatikana na kipindi cha mvua karibia kinaanza.

Je, ni lini sasa ujenzi utaanza rasmi wa barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, taratibu zote za zabuni na kuandaa zimeshakamilika. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zote za manunuzi zitakavyokuwa zimekamilka, barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaendelea na matengenezo ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma uliosimama kwa muda wa mwaka mzima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya matengenezo ya Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma yatafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank – EIB)* pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, matengenezo yalisimama kwa sababu Mfadhili alichelewa kutoa idhini ya kumpata Mkandarasi atakakayetekeleza kazi hizo. Kwa sasa, idhini *(No Objection)* imeshatolewa.

Mheshimiwa Spika, mfadhili wa mradi huu ameshatoa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu. Kwa sasa rasimu ya Mkataba imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio.

Meshimiwa Spika, mara baada ya taratibu za *vetting* kukamilika na Mkataba kusainiwa, utekelezaji wa kazi za matengenezo ya upanuzi wa mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma utaanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kigoma, Wizara ya Ujenzi imetoa taarifa kwamba mna mpango wa kuupanua uwanja huo *running way* yake kutoka 1.8 kilometa na kuja kilometa 3.1; na wananchi wamepata taarifa hizo, lakini mpaka sasa hawajui ni eneo gani mtalichukua la wananchi.

Je, ni lini Wizara yako itakwenda ku-*earmark* maeneo ambayo yatayachukua, ili maeneo ambayo hamyachukui wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo?

Je, baada ya kuyachukuwa, mtaweza kulipa fidia kwa wakati tofauti na ilivyokuwa hapo nyuma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli ahadi imeshatolewa, lakini pia nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari hata usanifu Wizara imeshafanya tayari, kutoka kilometa 1.8 mpaka kilometa 3.1. Kuhusu fidia, tayari taratibu zinaendelea ili mara taratibu, na hasa tunataka uwanja utakapoanzwa kujengwa kwa awamu

ya kwanza kwa uwekezaji wa fedha ndipo awamu ya pili itakapoanza kupanua uwanja.

Kwa hiyo nikuhakaikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuanahitaji sana huo uwanja kuwa mrefu ili kupokea ndege. Serikali imejipanga kulipa fidia kwa wakati na kuanza kujenga, na taratibu zitakapoanza tutakuja kuwajulisha wananchi, wapi uwanja huo utapita. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali iliweka mpango wa kujenga viwanja katika mikoa kumi na moja, ukiwemo Mkoa wa Singida. Sasa nataka kujua ni lini ujenzi huu wa Uwanja wa Ndege Mkoa wa Singida utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mpango upo wa kujenga Uwanja wa Singida na kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study* ya Uwanja wa Singida. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ta, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'TA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Je, ni lini uwanja wa ndege wa Sumbawanga Mjini utaanza kujengwa? Nataka *commitement* ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ta, Mbunge wa Rukwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nililotoa, jibu hili linafanana kabisa na swali la Mheshimiwa Bupe. Tuna viwanja vinne ambavyo ni Kigoma, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga, ambavyo vyote vinafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ulaya. Pia, huyu mfadhili ameshatoa fedha na muda wowote uwanja huu, kama nilivosema wa Kigoma, nao utaanza kujengwa ikiwa ni pamoja na Uwanja wa Tabora na Shinyanga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Uwanja wetu wa Iringa ni uwanja ambao tayari umeshawekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Rais;

Je, ni lini sasa utakamilika kwa sababu ujenzi umechukuwa muda mrefu sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uwanja huu unaendelea kujengwa lakini pia uwanja huu *World Bank* imekubali kuufadhili, na kwa kuwa unaendelea. Kama kulikuwa na changamoto za kuchelewa, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kasi imeongezeka na tuna hakika uwanja utakamlishwa kwa sababu mkandarasi yupo *site* na anaendelea na kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Simiyu upo kwenye ilani na eneo tayari limeshatengwa,

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege Mkoa wa Simiyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri waa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Simiyu, kama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Uwanja wa Simiyu unatakiwa Kujengwa na mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kufanyia usanifu. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi sasa hivi kuna gesi ambayo tunategemea itakuwa inawekezwa pale.

Je ni lini Uwanja wa Ndege wa Lindi Mjini utatatengenezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pathan, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Lindi upo kwenye mpango, na katika bajeti hii upo kwenye mpango wa kuanza taratibu za kuujenga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Ujenzi wa Barabara ya Sengerema – Nyamazungo – Nyehunge na Nkome**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Sengerema – Nyamazugo – Nyehunge na Nkome kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Ujenzi Na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Erick James Shigongo, Mbunge wa Buchosa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ipo katika hatua za Manunuzi ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Sengerema – Nyamazugo – Nyehunge yenye urefu wa kilometa 54.4. Zabuni zilifunguliwa mnamo tarehe 30 Agosti, 2022. Uchambuzi wa zabuni unaendelea na mkataba wa kazi za ujenzi unatarajiwa kuwa umesainiwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena, ukiwa muulizaji wa swali la msingi, usiposimama maana yake huna swali la nyongeza. Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Nataka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana Serikali kutuletea barabara ya lami, lakini ilishafanyika tathmini lakini wananchi wanasubiri malipo. Kwa sababu mchakato unaendelea, je tathmini italipwa lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu barabara hii inahusisha Majimbo mawili, Jimbo la Sengerema na Jimbo la Buchosa, je Serikali iko tayari kuchukua ushauri wa wananchi wa Buchosa, kwamba ujenzi wa barabara hii uanzie Buchosa kuelekea Sengerema badala ya Sengerema kuelekea Buchosa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilimuelewa kuhusu tathmini, nadhani ni fidia, italipwa lini? Kama nilimuelewa ni kwamba fedha ambazo tumetenga, kitu cha kwanza itakuwa ni kulipa fidia ya wananchi ambao watapisha ujenzi huo, halafu barabara itaanza kujengwa. Kwa hiyo, itakuwa ni hatua ya kwanza ya kufanywa kabla ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri alioutoa, kwa mujibu wa barabara ilivyo ni Sengerema-Nyamazugo-Nyehunge; hili suala ambalo tayari hata zabuni kama zimeshatangazwa, maana yake zinataja kuanzia wapi kwenda wapi. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kwamba majimbo ni hayo mawili

lakini barabara itaanzia huku tulikoitaja na kwenda pale inapokwisha kwa sasa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Ninapenda kutaka kujua jibu la uhakika leo, ni lini barabara ya kutoka Kolandoto-Kishapu-Lalagwa hadi Meatu itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza la Mheshimiwa Minza, Mbunge wa Viti Maalum Simiyu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha kuanza ujenzi wa Kolandoto hadi Lalago, bababara hii ambayo ni barabara kuu na tutaanza kwa kilometa 10 kwa sababu fedha tumetenga katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almasi Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMANI A. MAIGE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniruhusu na mimi niulize swali la nyongeza. Barabara ya Tabora - Mambali ambayo ufanisi wake umekwishafanyika siku nyingi, lini itaanzwa kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maige, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tabora - Mambali tulishakamilisha usanifu wa kina na fedha tumetenga; na Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga hii barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ipo ahadi ya kujenga kwa kilometa kumi kumi barabara kutoka Lushoto mpaka Mlalo. Je ni lini ahadi hiyo itaanza kutekelezwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli ahadi ilishatolewa na Serikali inatafuta fedha ili kuanza ujenzi wa hiyo barabara kwa kilometa kumi kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami, tumeshaanza, tumeshafika Magamba tukiwa tunaelekea Mlalo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Barabara ya Zamahero-Babayo-Makorongo hadi Donsee ndicho kipande pekee yake kitakuwa sasa hakina lami, ukizingatia barabara ya Kibarashi - Handeni hadi Singida inajengwa na ni kibarabara cha kilometa 18 tu, nataka kujua Serikali mna mpango gani wa kutumalizia hiko kibarabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, alichosema ni kweli, barabara hii tutaijenga kwa kiwango cha lami lakini itategemea na upatikanaji wa bajeti. Kwa hiyo, Serikali inalifahamu na inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha hicho kipande ambacho ndicho kilichobaki. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ambayo ipo kwenye ilani na ipo kwenye mpango wa maendeleo, kutoka Mtwara - Pachani - Rusewa na Rasi-Tunduru barabara hiyo ambayo ni barabara ya ulinzi, na Naibu Waziri uliitembelea na kuona umuhimu wa barabara hiyo ambayo ina viijiji visivyopungua 40?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli alichosema, barabara hii tumeitembelea na ni barabara muhimu ina kilometa zisizopiungua 300. Tumeshakamilisha usanifu wa kina na kabla ya kuanza tumeainisha maeneo yote korofi kwanza na madaraja ili tuweze kuyajenga wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga barabara yote hii muhimu kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Utekelezaji wa Mkataba Kati ya Serikali na *Dubai World***

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini utekelezaji wa Mkataba wa kibiashara kati ya Serikali na Kampuni ya *Dubai World* utaanza?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2022 Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* ilisaini Hati ya Makubaliano *(MoU)* na Kampuni ya *Dubai Port World (DP-World)* ya Umoja wa Falme za Kiarabu, kuhusu uwekezaji katika maeneo ya bandari nchini. Aidha, tarehe 25 Oktoba, 2022 Serikali ilisaini makubaliano na Serikali ya Dubai *(Inter-Governmental Agreement - IGA)*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkataba wa kibiashara unakwenda katika hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza ni mkataba kati ya nchi na nchi *(Intergovernmental Agreement - IGA)* ambao tayari umesainiwa. Mkataba huo unaweka msingi wa Serikali za pande mbili kuanza majadiliano kuhusu maeneo ya uwekezaji. Baada ya kusainiwa kwa mkataba huo, majadiliano yataendelea kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi ili kuhakikisha kwamba uwekezaji huo unakuwa na tija kwa nchi. Matarajio ya Serikali ni kuwa majadiliano hayo yatafikia tamati mwishoni mwa mwezi Desemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na bora kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya

nyongeza. Kwa kuwa sisi tayari tunalo eneo letu la kibiashara: Je, ni kwa kiasi gani Serikali imejiridhisha juu ya uwezo wa ufanisi na uwezo wa mtaji wa Kampuni ya *DP World* ili kuja kuongeza soko katika bandari zetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kwa kiasi gani Serikali imejiridhisha uwezo wa kuweza kuongeza ushindani kwa kuwa tayari tunazo Bandari za Beira (Msumbiji), Mombasa (Kenya), na *Durban (South Africa)* ambazo tunashindana nazo? Mmepima uwezo wa *DP World* kuja kuongeza ushindani katika eneo hili la ukanda wa *SADC* na ukanda wa Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali pasi na shaka imejiridhisha kwamba *DP World Port* ina uwezo wa kuendesha bandari zetu nchini hususan Bandari yetu ya Dar es Salaam. Tumejiridhisha kwa maana ya kwamba, kwanza, inafanya kazi katika mataifa yasiyopungua 69 duniani, na pia wataalamu wetu wametembelea mataifa hayo ikiwemo Uingereza, Canada, India, Dubai kwenyewe na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, vile vile Bandari hii ya Dar es Salaam hivi sasa inapata wateja wake kwa njia ya mfanyabiashara kuleta meli yake, lakini kupitia *DP World,* wao wana *connection,* au mtandao mpana wa kibiashara huko duniani, kwa hiyo, watatutafutia masoko.

Zaidi ya yote, wamejenga bandari kavu katika nchi ambazo tunahudumia kama Taifa hususan kule Congo pamoja na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kujiridhisha kuhusu ushindani na uwekezaji ambao atafanya *DP World.* Ni kweli kwamba ushindani katika bandari zetu ni mkubwa hususan katika ukanda wetu wa Bahari ya Hindi. Tuna Mombasa, ni washindani wetu; tuna Beira (Msumbiji), pamoja na Durban (Afrika Kusini). Kupitia *DP World*, Bandari ya Dar es Salaam, itaongeza ufanisi kwa ushindani kwa sababu kwanza ataleta vifaa na vyombo vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mifumo ambayo tumekuwa tukizungumza miaka mingi katika Bandari yetu ya Dar es Salaam ili taasisi zionane kupitia mifumo ya *electronic single window system,* pia itawekezwa na itakuwa *automated* ili kuongeza ufanisi. Sasa hivi ukienda bandarini utakuta meli ni nyingi lakini muda wa kupakua na kushusha mizigo ni mrefu. Hili ndilo tunataka sasa tuongeze ufanisi kwa kupunguza huo muda ili Bandari yetu ya Dar es Salaam iendane na ushindani wa bandari hizi nyingine ambazo nimezitamka.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Hitaji la Vituo vya Polisi Tarafa za Gonja na Mamba – Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Vituo vya Polisi katika Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika Tarafa ya Gonja kuna Kituo cha Polisi cha Daraja *B* kinachoongozwa na Mrakibu Msaidizi wa Polisi na kina Askari 16 na gari moja. Tarafa ya Mamba haina Kituo cha Polisi wala haijatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo na makazi ya Askari. Hivyo tarafa, hiyo hupata huduma za Polisi toka kituo cha Polisi Gonja na vituo vidogo vya Polisi vya Kihurio na Ndungu vilivyo katika Tarafa ya Mamba.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wetu kwa Mheshimiwa Mbunge kushirikisha Halmashauri ya Wilaya ya Same kutenga eneo katika Tarafa ya Mamba kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi, pamoja na nyumba za

makazi ya Askari ili Serikali iweze kuingiza katika mpango wa kukitengea bajeti ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nitoe, sijui niite dukuduku au nini; lakini nimesikitika sana kwa majibu haya ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali hili niliuliza hapo nyuma *engineer* akiwa Naibu Waziri, akanijibu hivi hivi. Ni kwamba wewe hujui tofauti kati ya tarafa na kata. Hapa hapa kwenye jibu lako umeji-*contradict*. Umesema Tarafa ya Mamba haina Kituo cha Polisi. Hapa mwisho unasema kuna kituo ambacho kipo Tarafa ya Mamba.

Mheshimiwa Spika, naomba wakalifanyie kazi hili swali. Tarafa ya Gonja iko milimani mbali sana kutoka kituo hiki killichopo Maore, Tarafa ya Ndungu. Tarafa ya Gonja ina kata nne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, swali hili halikufanyiwa kazi. Naomba kwa heshima na taadhima, wakalifanyie kazi swali hili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyoka, nimekusikia, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri hatatakiwa kujibu chochote hapo, ni mpaka sisi tukajiridhishe na haya majibu. Wewe

umeshaeleweka, huna haja ya kueleza kitu kingine. Mimi nimeshakuelewa.

Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tarafa ya Ulyankulu yenye kata saba haina kabisa Kituo cha Polisi, hali ambayo inapelekea vitendo vya kihalifu kuwa ni vingi: Je, ni lini Serikali itatujengea Kituo cha Polisi kwenye hii Tarafa ya Ulyankulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rehema Migilla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tarafa ya Ulyankulu haina Kituo cha Polisi chenye hadhi ya tarafa, lakini ni suala la kuweka katika mipango yetu ili kiweze kufikiriwa kujengewa Kituo cha Polisi. Kwa hiyo, bajeti itakaporuhusu tutaliingiza hili na kituo kitajengwa kwenye hiyo Tarafa ya Ulyankulu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako. Ah, Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilikuwa nataka tu nami nipate majibu ya Mheshimiwa Waziri ya swali langu dogo la nyongeza. Nimekuwa nikiahidiwa mara nyingi

sana, zaidi ya mara sita, saba juu ya vituo vyangu katika Jimbo langu la Chumbuni, lakini sijapata mwendelezo wala kujengewa vituo hivi na hali ya kiusalama kila siku zikivyoenda imekuwa siyo nzuri na wananchi wanafuata huduma mbali kiasi ambacho kama kuna mhujumu ametokea, basi watu kupata usaidizi inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba majibu ambayo yataeleza ni lini tutapata huduma hii katika Jimbo letu la Chumbuni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ussi anafahamu nilitembelea Zanzibar na kwenye jimbo lake nilifika nikaona hali ya vituo vidogo vya polisi vilivyopo na kwa kweli kwenye eneo lake anastahili kujengewa Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba tu upande wa Kamisheni ya Polisi ya Zanzibar iingize mahitaji ya Kituo cha Polisi eneo la Chumbuni ili iweze kupangiwa bajeti kwa ajili ya kuanza kujengwa kwenye bajeti itakayofuata.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, nalipitia jibu la Wizara na swali ambalo Mheshimiwa Kaboyoka aliuliza kwa sababu hajauliza swali la msingi, anauliza kuhusu hiki kilichopo hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri ukae katika eneo lako nitakapoanza kutoa maelezo kuhusu haya majibu.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Bei ya kuunganisha umeme maeneo ya kata za mjini zenye sura za vijiji**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaainisha bei rasmi za kuunganisha umeme maeneo ya kata za mjini zenye sura za vijiji?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na zoezi la utambuzi wa maeneo na wananchi wanaoishi katika maeneo ya Kata za Mjini zenye sura za vijiji.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili linatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Desemba, 2022 na baada ya zoezi hili Serikali itapanga bei muafaka za kuunganisha umeme kulingana na uhalisia wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Naishukuru Serikali kwa sababu wakati natoa swali hili nilikuwa na mahitaji ya kata mbili zenye mitaa zaidi ya 14, yenye sura za vijiji. Sasa hivi ninavyozungumza Kata za Lwanima na Kishiri, mkandarasi wa *REA*, kwa gharama ile ile ya Shilingi 27,000/= anaendelea kufanya kazi na wananchi wangu wanafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali. Nitoe tu msisitizo uchambuzi huo utakapokamilika utatusaidia kujaziliza maeneo ambayo yatakuwa yamebaki kwa gharama nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kupokea pongezi na maombi ya Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana na kwamba tunashukuru ameona Serikali inavyojitahidi kuendelea kutekeleza

huduma hii ya kupeleka umeme kwa wananchi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, hili la kukamilisha zoezi la utambuzi wa maeneo kama tulivyojibu kwenye swali la msingi, tutahakikisha linakamilika kwa wakati na liweze kutusaidia katika maeneo yetu sote.

Mheshimiwa Spika, nami Jimbo langu la Bukoba Mjini likiwemo linafanana na la kwake pia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru… oh, kuna Mheshimiwa amesimama. Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naomba tu nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri; tulileta malalamiko kuhusu hii miji midogo ambayo ina sura ya vijiji, mkasema tathmini inafanyika na hiyo timu itakuja kwa Wabunge ili tufahamu kama mnafika maeneo yetu. Sasa ni lini hii timu yenu itafika kwa Wabunge hawa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, tuliahidi kwamba kuna timu itaenda kuwatembelea na kuzungumza na Wabunge ili kuweza kubaini yale maeneo ambayo tunataka kuyafanyia kazi. Timu hii imeanza kufanya kazi

ya ndani, ni kama ku-*plot* maeneo ambayo inatakiwa iende kuyatembelea kwa sababu kuna mengine yanafahamika, hayahitaji kwenda kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii shughuli ya ndani ya utambuzi itakapokuwa imekamilika kwa taarifa iliyokuwepo, ndiyo sasa itaenda *site* na Waheshimiwa Wabunge wote wanaohusika wataiona hii timu kwa sababu maelekezo ya Wizara ndivyo yalivyo kwa ajili ya kushirikiana kuweza kutambua maeneo hayo kwa usahihi zaidi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Ukarabati Mahakama ya Mwanzo Chala – Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo Chala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Chala yenye Kata nne; za Chala, Nkadasi, Kipande na Mkwamba, ina Mahakama za mwanzo mbili za Chala na Kipande. Katika kuimarisha majengo ya Mahakama kwa kuzingatia mpango uliopo wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama nchini, Mahakama ina mpango wa kukarabati jengo la Mahakama ya Mwanzo Chala katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza. Jimbo la Nkasi Kusini Tarara ya Kate, huduma za kimahakama wanatumia *godown*; upande mmoja magunia, upande mmoja Mahakama inaendelea.

Mheshimiwa Spika, nilimpigia simu Mheshimiwa Naibu Waziri, akafika, tukatembelea Tarafa ya Kate yeye mwenyewe akajionea mazingira magumu, jinsi gani huduma za haki za kimahakama zinatolewa katika mazingira ambayo siyo mazuri. Ni *godown*, wakiweka dawa kwenye mazao, Mahakama haikaliki, ni harufu tupu: Je, ni lini serikali inakuja kujenga jengo la kisasa Tarafa ya Kate? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia sana masuala haya kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kupata eneo sahihi la kupata huduma za haki. Ni kweli kabisa nilitembelea Kate, na nilikuta ni kweli wanatumia *godown* ambalo ndiyo linakuwa kama Mahakama.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo tumelichukua na kwa sasa hivi katika ule mpango kazi ambao Mahakama imejiwekea, tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge, katika kipindi hiki tunachoendelea nacho mpaka kufika 2025, Makao Makuu yote ya Tarafa nchini tunakwenda kujenga majengo ya Mahakama ya Mwanzo. Kwa hiyo, kwa sababu Kate ni Tarafa, inaenda kupata upendeleo wa pekee katika kipindi kijacho cha fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 62

**Wananchi Walioathirika na Uvamizi wa Wanyama Wakali Kyerwa - Kagera**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, ni wananchi wangapi wameathirika na uvamizi wa wanyama wakali katika Wilaya ya Kyerwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imepokea taarifa ya matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ambapo jumla ya wananchi 54 katika Vijiji vya Kibare, Businde na Nyakashenyi walipata madhara ya uharibifu wa mazao yao uliosababishwa na tembo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sekwa Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na uharibifu huo uliojitokeza wananchi hawa walihamishwa kwenye vitongoji vile kwa sababu ya uharibifu wa wale tembo. Mpaka sasa hivi wananchi wale wanaendelea kupata shida hakuna walicholipwa. Je, ni nini mpango wa Serikali angalau wa kuwapa fidia hawa wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwenye Kata ya Businde, Kata ya Bugara pamoja Kikwechenkura, tembo wanaendelea kufanya uharibifu mkubwa, taarifa zinaendelea kutolewa lakini hakuna chochote ambacho Serikali inafanya. Je, ni nini mpango wa Serikali wa

kudumu kuweza kuwahamisha wanyama hao waharibifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitoe pole kwa wananchi wote ambao wamekuwa wakikutwa na kadhia hii ya changamoto ya wanyama wakali na waharibifu. Serikali inatambua changamoto hizi na ndio maana tumeanza ujenzi wa vituo vya askari ili kusogeza huduma hii kwa ukaribu zaidi na wananchi waweze kutoa changamoto zao na huduma hii iweze kutolewa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tumeanza kufundisha vijana kwenye maeneo husika hususan vijana wa kwenye maeneo ya vijijini kama *VGS* ambao watashirikiana na askari kuhakikisha kwamba, wanyama wanaposogea katika maeneo ya shughuli za kibinadamu, basi iwe rahisi kuwaondoa.

Mheshimiwa Spika, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inachukua hatua na suala la kifuta machozi na kifuta jasho, tayari tumeshaanza kufanya tathmini na utekelezaji wake utafanyika hivi punde. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchester Rwamlaza, swali la nyongeza.

**CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wananchi 71 wa Kata ya Busindi, Kijiji cha Businde na Kitongoji cha Nyakabumbwe, pia katika Kijiji cha Nyakashenye, waliambiwa wapishe eneo lao kwa sababu ni ushoroba wa kupita tembo na waliahidiwa kupewa maeneo mengine, lakini hadi sasa pamoja na kupita katika mamlaka mbalimbali hawajapewa mahali popote. Je, ni lini Serikali itawapatia eneo la kuishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo yamevamiwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo hata ujenzi wa nyumba. Eneo la Kitengule ni eneo ambalo ni *ranch* ambapo sasa wananchi walipoyavamia yale maeneo tembo wakawa kama wako kwenye kisiwa. Moja ya tiba ambayo tulitaka kuifanya ni kufungua ule ushoroba ili tembo waweze kuruhusiwa ku-*move* kwenda kwenye Hifadhi ya Burigi Chato. Tulielimisha wananchi katika eneo hilo na utaratibu sasa wa kufungua hizi shoroba ni pamoja na wananchi kukubali kupisha zile shoroba.

Mheshimiwa Spika, tunafanya tathmini na tukishafikia muda ambao ni muafaka fedha na namna ya kuwahamisha wale tembo basi tutarudi kwa wananchi kuwafahamisha zoezi hili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Utekelezaji wa Kampeni ya *AFR 100***

**MHE. MOHAMED JUMAH SOUD** aliuliza:-

Je, Kampeni ya *AFR 100* imetekelezwa kwa kiasi gani na maendeleo gani yamefikiwa hadi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imefikia hatua zifuatazo katika utekelezaji wa Kampeni ya *AFR 100*: kuondoa wavamizi na kurejesha ardhi iliyoathiriwa; Kuimarisha usimamizi wa misitu ya mikoko; Kutoa elimu ya kudhibiti moto wa msituni ili kulinda uoto wa asili; na Kutekeleza Mpango wa Dodoma ya Kijani.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yaliyofikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa makubaliano ya Kurejesha Mandhari ya Kiafrika – *(AFR 100)* na Mbinu ya Tathmini ya Fursa ya Marejesho. Aidha, Tanzania imefanikiwa kuandaa na kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kurejesha Mandhari ya Misitu. Mkakati huu unatarajiwa kuwasilishwa

katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa kujadili masuala ya Mazingira *(COP 27)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa nchi yetu Tanzania hivi sasa inakabiliwa na wimbi kubwa la ukataji na uchomaji moto wa misitu ya asili. Je, Wizara ina mkakati gani wa ufuatiliaji kuona mpango huu wa *AFR 100* unakwenda kufanikiwa ili kukabiliana na tatizo la uharibifu wa misitu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa utekelezaji wa lengo la mpango huu linajumuisha nchi nzima pamoja na Zanzibar. Naomba tu kujua tumeishirikishaje Zanzibar ili kuona mpango huu tunautekeleza kinchi zaidi ili kuweza kukabiliana na tatizo la uharibu wa misitu kule Zanzibar? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud Mohammed Jummah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mhifadhi mzuri kwenye masuala haya ya misitu kwa sababu kwa asilimia kubwa

amekuwa anatoa mchango mzuri sana kwenye eneo hili la uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mingi na mikakati hii tayari ilishaanza kutekelezwa tangu mwaka 2018 ambapo Serikali iliingia mkataba na dunia. Mkakati huu ni wa kidunia lakini kwa Afrika tumeelekezwa kutekeleza jumla ya hekta milioni 100 kuziongoa ili ziingie kwenye uhifadhi. Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimeingizwa katika mkakati huo ambapo jumla ya hekta milioni 5.2 tumeziwekea mkakati huo na malengo yetu ni kuhakikisha tunaziongoa.

Mheshimiwa Spika, mikakati hii imeendana sambamba na zoezi la uongoaji na urejeshaji wa maeneo ya hifadhi. Hivi karibuni utashuhudia ziara ya Mawaziri Nane wamekuwa wakitembea kila mikoa kuhakikisha kwamba maeneo yale ambayo yanastahili kurejeshwa, yarejeshwe ili tuweze kuingia kwenye mpango huu wa kidunia ambao tunaongoa jumla ya hekta milioni 350.

Mheshimiwa Spika, swali lake lingine ambalo ameuliza, je, Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo ziko ndani ya mkakati huu. Zanzibar ni kweli ipo na kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Muungano zoezi hili linafanyika kama Tanzania Bara na Zanzibar hivi karibuni kuna Mradi wa *FAO* ambao umeunganisha Zanzibar na Kigoma na tayari wanatekeleza katika maeneo mbalimbali ikiwemo kurudisha maeneo ya hifadhi ili kurejesha uoto wa asili.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Serikali Kutoa Bei Elekezi ya Maji – Karatu**

**MHE. DANIEL T. AWACK** aliuliza:-

Je, ni lini itatolewa bei elekezi ya maji katika Karatu ili kuondoa tofauti kati ya *KARUWASA* wanaouza *unit* 1 Sh.1,700 na *KAVIWASU unit* 1 Sh.3,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha hakuna changamoto katika ulipaji wa bili za maji kwa wananchi. Hivyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023, imeviunganisha vyombo vya usimamizi wa huduma ya maji *KARUWASA* na *KAVIWASU* na kuunda chombo kimoja cha *KARUWASA* ambacho kitakuwa imara ili kiweze kutoa huduma ya maji kwa ufanisi katika eneo lote la Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Spika, bei elekezi ya kuanzia kwa uniti moja ya maji imeshatolewa na inatumika. Aidha, marekebisho yataendelea kufanyika kwa kuzingatia miongozo kutoka *EWURA*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL T. AWACK:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nishukuru Serikali kwa bei elekezi katika eneo la Mji wa Karatu. Pamoja na shukrani hizi nina swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatoa bei elekezi katika maeneo mbalimbali vijijini kutokana na kwamba kwa sasa bei ni tofauti kati ya kijiji na kijiji na hizi bei huwa inaamuliwa na Jumuiya za Maji Vijijini? Je, ni lini Wizara itatoa bei elekezi katika maeneo mbalimbali katika Jimbo la Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, kubwa ambalo nataka nilieleze Wizara yetu ya Maji eneo la vijijini, tunatoa huduma kupitia Taasisi yetu ya Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)*. Tulifanya tathmini kuona baadhi ya maeneo ya mjini na vijijini unakuta eneo la vijijini walikuwa wakilipa gharama kubwa katika suala zima la ulipaji wa maji. Wizara imeshatoa bei elekezi, ipo miradi ambayo inatumia nishati ya umeme, ipo miradi ambayo inatumia nishati ya jua. Kwa hiyo tumetoa maelekezo kila mradi kutokana na *pump* zinazotumika imewekwa hela yake rasmi kwa ajili ya kulipa hususan kwa maeneo ya vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Felix Kavejuru.

Na. 65

**Mradi wa Maji Kata ya Kazuramimba**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji Kata ya Kazuramimba ?

**SPIKA :** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Maji wa Kata ya Kazuramimba ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu kilometa 3.3, ulazaji wa mabomba ya usambazaji Kilometa 26.7 na ujenzi wa tanki la ukubwa wa lita 470,000. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felix Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itapeleka miradi ya maji katika Vijiji vya Lusawa, Mdoha, Ukuba na Janda katika Jimbo la Buhigwe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kutumia maji ya Mto Malagarasi kutatua changamoto ya maji katika Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, mkakati wa Wizara yetu ya Maji hasa maeneo ya vijijini kuhakikisha kwamba itakapofika 2025 asilimia 85 ya upatikanaji wa maji iweze kutekelezeka. Tumeshapokea mitambo 25 na kila mkoa utakuwa na mtambo wake. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge maeneo yale ambayo ameyaainisha tutawapa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba tunajenga miradi hii kwa wakati na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo mahususi Wizara yetu ya Maji kwamba tutumie rasilimali toshelevu ikiwemo mito pamoja na maziwa ili kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto kwa eneo kubwa sana. Kwa hiyo kikubwa nimhakikishie Wizara yetu ya Maji kwa eneo la Kigoma tumelenga kutumia Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua changamoto hii ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mradi wa Igongwi ambao unahudumia Kata tatu Matola, Luponde na Uwemba tunashukuru Serikali kwa pale tulipofikia, lakini

unasuasua sana. Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwa wananchi wa Njombe kuhusiana na mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, natambua mradi ule ni wa kimkakati ambao utatoa huduma kwa watu wengi sana. Mwezi huu tumekwishapokea zile fedha na moja ya maeneo ambayo tunatakiwa tulipe ni mradi ule. Nataka nimhakikishie mwezi huu tutalipa mradi ule wa maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge nilisema nitarejea kwenye swali namba 59 na majibu yaliyotolewa ili niweze kutoa maelekezo mahususi kuhusu kanuni yetu ya 53 ambayo inataka maswali yajibiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Kaboyoka unalo jibu hili hapo kwako, jibu la Waziri alilolisoma unalo.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Sawa, sasa ninavyosoma utanieleza walipokosea ni wapi, kaa tu Mheshimiwa. Utaniambia nikishatoa haya maelezo walipokosea ni wapi ili nijue nini cha kuiagiza Serikali. Jibu linasema katika Tarafa ya Gonja kuna Kituo cha Polisi cha Daraja B kinachoongozwa na Mrakibu Msaidizi wa Polisi na kina askari 16, na kina gari moja. Hiki kituo kipo kwenye hii Tarafa ya Gonja?

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, hapana, Tarafa ya Gonja iko milimani, mbali sana na hapa anapoongea. Hapa anapoongea Gonja panaitwa Maore ambayo ni kata iliyoko Tarafa ya Ndungu bondeni, kwa hiyo Tarafa ya Gonja iko milimani na ina kata nne na haina kituo chochote cha polisi hata *small post* haina.

**SPIKA:** Kwa hiyo Tarafa ya Gonja haina hiki kituo kinachosemwa hapa?

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, haina.

**SPIKA:** Sawa, Tarafa ya Mamba jibu la Wizara linasema: "Tarafa ya Mamba haina Kituo cha Polisi ila inahudumiwa na Vituo Vidogo vya Polisi vya Kihurio na Ndungu, hivi vituo vidogo vya polisi vipo au hiki kituo cha Ndungu ndio kile kinachosemwa mwanzo pale?

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Ndungu ndio yenye hivyo vituo vidogo ambavyo viko Kihurio na Ndungu yenyewe ikihudumiwa na hiki kituo kikubwa kilichopo inaitwa Kata ya Maore. Kwa hiyo Mamba iko huko milimani na inaitwa Tarafa ya Mambavunta yenye kata tisa.

**SPIKA:** Sawa kwa hiyo Tarafa ya Gonja haina kituo wala Tarafa ya Mamba haina kituo?

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli zote hazina kituo.

**SPIKA:** Haya, kama hivyo ndivyo nilikuwa nimesema kwa sababu alieleza hayo wakati akiuliza swali la

nyongeza sasa wacha nisimame ili nitoe maelekezo mahususi baada ya kuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo ya Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na swali lake alilokuwa ameliuliza, aliuliza mahususi kuhusu Tarafa ya Gonja na Tarafa ya Mamba, hakutaka zile Tarafa za Ndungu. Kwa hiyo Wizara ilete majibu ya swali hili, Wizara ilete majibu upya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa Serikali na Serikali kuweza kutoa majibu ya maswali yenu. Sasa nilete matangazo tuliyonayo hapa mbele tutaanza na tangazo la wageni.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Patrobas Katambi Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni miongoni mwa vijana 80 walioenda nchini Israel kwa ajili ya Kozi ya Kilimo ya miezi 11 iitwayo *Agricultural Capacity Building Studies, 2021/22* inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Haya karibuni sana na tunaamini yale mliyoenda kujifunza mtakuja kuyafanyia kazi katika mpango huu maalum kabisa wa Serikali wa kuinua hii sekta ya kilimo, tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Hawa ni Maafisa Tarafa kutoka Mkuranga, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Kanisa Kuu la KKKT, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dennis Londo ambao ni wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini wanaotokea Mikumi, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe, ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambao ni wapiga kura wake kutoka Kalenga, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ambao ni wapiga kura wake kutoka Bunda, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI- KATIBU MEZANI:**

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**SPIKA:** Hoja ya kutengua kanuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ili aweze kuwasilisha hoja ya kutengua kanuni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkutano wa Tisa wa Bunge umepangwa kufanyika kwa siku tisa za kazi kuanzia tarehe 1 Novemba, 2022 hadi tarehe 11 Novemba, 2022. Kwa kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 113(2) kwa siku zisizopungua tano Bunge linatakiwa kukaa kama Kamati ya Mipango kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa Fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kanuni ya 34(15) inaelekeza kwamba Bunge halitaendelea na shughuli zake siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko; na kwa kuwa shughuli zilizopo haziwezi kufanyika kwa ufanisi na kukamilika ndani ya muda wa siku tisa zilizotengwa kwa ajili ya Mkutano huu; hivyo basi ili kuiwezesha Bunge kutekeleza kazi zake kiufanisi na kuweza kumaliza shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa tisa Kanuni ya 113(2) na Kanuni ya 34(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, zitenguliwe kwa mujibu wa Kanuni ya 174 (1) kama ifuatavyo:-

(1) Kanuni ya 113 (2) itenguliwe ili Bunge litumie siku nne kukaa kama Kamati ya Mipango badala ya siku tano zinazotakiwa na Kanuni hii; na

(2) Kanuni ya 34(15) itenguliwe ili Bunge likutane siku ya Jumamosi Tarehe 5, Novemba, 2022, isipokuwa kwamba siku hiyo Bunge litaanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na kutakuwa na kipindi cha Maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Nasasa kwa utaratibu wetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge mnaoafiki hoja ya kutengua Kanuni kwa ajili ya hayo mambo mawili, kwa maana ya kujadili mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa siku Nne pia kukutana siku ya Jumamosi Tarehe 05 Novemba, 2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri wote tumeafiki, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI-KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu**

**za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na hapa ninayo majina ya Wabunge ambao wameomba kuchangia siku ya leo kwenye hoja zetu zote tatu. Mheshimiwa Mhandisi Ezra Jonh Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdalla na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia katika hoja zetu tatu hizi ambazo zinaendelea mezani, hoja ya Kamati ya *PIC, PAC* na Kamati ya *LAAC*. Nitajikita kwenye mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nitajikita kwenye Kamati hii yetu ya *PAC* juu ya ukaguzi na hasara ambayo tumeipata kutokana na matumizi mabaya ya fedha za umma ninayo ripoti hapa ya Kamati kuanzia ukurasa wa 10 mpaka ukurasa wa 11 kipengele 2, 5, 1 kuhusu riba kuchelesha malipo inayotokana na kuchelewa kulipa wakandarasi katika Wakala wa Barabara *TANROADs* Billion 68.7.

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite hapa, kutokana na taarifa ya Kamati inasema sharti la Kifungu cha 54 ya

jumla ya mkataba wa ujenzi *GCC* kinatamkwa kwamba Mwajiri atamlipa Mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na Meneja wa Mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila hati ya malipo (Mikata ya Kimataifa ni siku Hamsini na Sita (56) kwa msingi huo Mwajiri akichelewesha malipo Mkandarasi atalipwa riba ya kuchelewa malipo katika hati ya malipo inayofuata.

Mheshimiwa Spika, sasa nikipitia hapa tunaona kwamba *TANROADS* wanetusababishia matumizi mabaya ya Fedha ya Umma kwa takribani billion 68.73 katika Mwaka huu wa Fedha 2021. Nimejaribu kupitia baadhi ya miradi nikawa najaribu kuangalia nikaona kwamba yapo matatizo na hususan ambao tumetokea kwenye ukandarasi huko tunajua. Kumekuwa na shida kubwa sana ya kupoteza fedha za umma lakini fedha hizi zinapotea kwa mipangilio mibaya tu. Sasa kama wanakubaliana au wanakosea kwa kutokujua sasa ndiyo nataka leo tuangalie hapa.

Mheshimiwa Spika, pesa zote hizi ambazo tunaziongelea hapa tunao uzoefu kwamba hakuna Mkandarasi wa ndani ambaye huwa analipwa hizi pesa, mara nyingi Mkandarasi wa ndani ukidai tu *penalty* kwamba umecheleweshewa malipo mradi unaofuata sehemu hiyo hutopewa mradi hata siku moja, *experience* tunayo lakini pesa zote hizi wanapewa watu wa nje, kwa sababu kwenye mkataba kuna sehemu ya kulipa riba lakini kuna sehemu ya kukata *liquidated damage*.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani ripoti ya *CAG* inatuonesha kwamba *TANROADs* wamesababisha hasara hii kwakulipa riba lakini *nowhere* tunaoneshwa kwamba hata wao *liquidated damage* walikata wapi? Serikali peke yake ndiyo wanaokosea, lakini Mkandarasi katika

Wakandarasi wote waliowalipa kwa sababu kulikuwa na miradi ya takribani zaidi ya Billion 600 ambazo walikuwa wanadaiwa lakini *there is nowhere* tunapooneshwa kwamba na upande wa Mkandarasi napo huwa kuna makosa. Kwa sababu kipengele cha kumtoza faini Mkandarasi kama *liquidated damage* kipo, kwamba na yeye anapochelewesha mradi unaanza kumkata baada ya siku kadhaa mpaka pale mradi utakapoisha au *amount* ile ya *security* ambayo ameiweka, lakini *we don't see that* ila tunachokiona ni sehemu ile tu ambayo upande wa Serikali wanakosea.

Mheshimiwa Spika, kwa nini inafikia hatua hii? Kwanza iko tabia na mazoea yale ambayo tunayo sisi hapa, hakuna Mkandarasi anayefanya makosa. Mkandarasi akishaona tu muda wake wa ku-*expire* umefika kwamba mkataba unafika mwisho Mkandarasi anaandika barua ya kuomba *extension,* lakini upande wa Serikali hata humu ndani kuna Waheshimiwa Wabunge mnafanya biashara mnajua. Ukishampelekea *certificate* ya malipo wewe tena ndiyo unayetakiwa kugeukwa kuwa mtumwa kila siku kwenda kumbembeleza kama vile ile hela ni ya kwakwe mfukoni anakupa wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wenzetu wa nje hawafanyi hivyo. Wenzetu wa nje kwa sababu sisi tunapenda nchi yetu, tunapata kazi hapa lakini tunapenda nchi yetu hatutaki ugomvi wa kugombana na Serikali. Wakati wenzetu wa nje wakishapeleka *certificate* hatakupigia simu wala hakufuati yeye anakaa siku 56 zimeisha anasubiri, sasa mambo mengi tumeyaona ikitokea ziara ya Kiongozi wa Kitaifa hapo ndipo utakaposhangaa Mkandarasi anatafutwa kwa nguvu zote maana wanaona hela inaelekea huku, hata ile hela ambayo

ulikuwa umeomba *certificate* haijaja mtu yuko tayari kukutumia hela leo halafu Kiongozi anaingia keshokutwa, matokeo yake akifika pale Wakandarasi wazawa tunaonekana kwamba tunalipwa pesa na hatufanyi kazi! lakini jiulize ile pesa imelipwa lini?

Mheshimiwa Spika, ndio maana mimi kuna rafiki yangu mmoja nakumbuka aliwahi kuwaambia hata pesa wasimuwekee kwenye akaunti maana aliogopa, unaletewe hela leo halafu Kiongozi anaingia keshokutwa, akiingia keshokutwa wewe ukikubali kwamba hela umeipokea kwenye akaunti kinachotokea ni nini? Anayesoma ripoti atasema Mkandarasi tumemlipa mpaka hapa lakini kazi haionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naongea hii *generally* tujaribu kuangalia jinsi ya kuondokana na haya. Tukikumbuka *TANROADS* wamekuwa na na tabia ya kutangaza miradi yao yote mwezi wa Julai, tunapoanza tu mwaka mpya wa fedha wanatangaza miradi yao yote, lakini tujiulize chanzo cha pesa za *TANROADS* ni nini? Tunazo pesa za *Road Fund*, tuna pesa za Hazina - Mfuko Mkuu wa Serikali na tunazo pesa za *donors* saa nyingine. Sasa unapotangaza miradi yote mwezi Julai kwa pamoja, miradi ya mwaka mzima, kinachokuja kutokea ni nini? *Cash flow* haiji kwa pamoja!

Mheshimiwa Spika, wale watu ukishawapeleka *site* kila mmoja anafanyakazi bila kumuuliza mwenzake umefikia wapi? Sasa unajikuta *certificate* zinafika mwisho kila mmoja ana madai na pesa ile haijapatikana au haijaonekana. Kwa hiyo *the proper planning* ambayo inabidi tufanye kama Bunge kuielekeza ni kwamba ili tuondokane na hizo hasara, kwa sababu Billion 68 siyo hela ndogo, hapo ungejenga kilometa 68 zingine.

Unaongelea vituo vya afya zaidi ya 120, hii si pesa ndogo wanaenda kulipwa watu *interest!*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ukijaribu kuangalia pesa ya nje huwezi kuilipia *interest* tutalipa kwa kutumia pesa ya ndani, maana yake ni nini? Pesa yetu ile ambayo tumeikusanya kwa kodi na kwa taabu badala ingetusaidia hapa tunachukua kama *penalty* tunapeleka nje tena kwa Wakandarasi ambao wametoka huko nje waonatudai hizi *penalty*. Kwa hiyo, niombe Bunge tutoe maelekezo mahsusi, ni bora wakagawanya in *quarterly basis,* miradi wakaigawanya kama wana miradi mia mbili, ukafanya miradi hamsini ianze Mwezi wa Saba na miradi 50 ianze Mwezi wa Tisa, miradi hii iendane, iwe inapishana utakapoanza kupokea pesa, kwa sababu una uhakika hakuna Mkandarasi wa barabara ambae atafanya *mobilizations* afanye vitu vyote hivyo ndani ya mwezi mmoja au miezi miwili awe ameanza kudai *certificate*. Kwa hiyo, tukifanya hivi itatusaidia ku-*save* hizi pesa. Hivyo, mipango mibovu ya *TANROADS* imetufikisha hapa leo kutusababishia hasara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoendelea kuyasema haya mipango mibovu ni pamoja na *management* nzuri. Tumeangalia hapa kwenye ripoti ya Kamati yako hii ya *PAC* ukurasa wa 22 inasema hivi, Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi. Tunajua *TANROADS* hawana Bodi ya Wakurugenzi leo ni takribani mwaka wa pili. Sasa jiulize taasisi hii tunaiendeshaje na haina Bodi ya Wakurugenzi? Imesemwa hapa kwamba *complains* hizi tunazozitoa hapa, ushauri tunautoa hapa unampelekea nani? Bado *TANROADS* huyu amerundikiwa majukumu mengi, tumesikikia jana hapa Waziri Mambo ya Viwanja vya Ndege baada ya watu kuongea hapa tangu juzi, akasema ooh! tutafanya *adjustment!* Unajiuliza kasema

uwanja wa Msalato utaendelea kubaki chini ya *TANROADS,* nilikuwa najiuliza jambo moja hapa, Shule ya Msingi tukiwa tunasoma, tulikuwa tunafundishwa Wakala wa Barabara *TANROADS,* kazi yake nini? Kujenga barabara. Wakala wa Viwanja wa Ndege? *TAA,* Wakala sijui wa mambo ya Reli? *TRL.* Sasa tukianza kuchanganya haya mambo leo mtoto kesho na kesho kutwa miaka imepita, kwa sababu hivi vitu haviondoki.

Mheshimiwa Spika, nimeingia tu kwenye *website* uki-*type* pale Bajeti ya Mwaka gani unapata. Leo tuko na mtoto mmoja pendwa katika Wizara hii ambapo wote wapo chini ya Wizara moja. Lakini kuna mtoto mmoja ana mapenzi makubwa mpaka anapewa kazi za wenzake, bado tupo humu ndani ya Bunge tunaambiwa kwamba ataendelea na Kiwanja cha Msalato, sasa unajiuliza huyu mtoto mzuri namna hii kama Baba ni huyohuyo mmoja, kwa nini asiwaelekeze na wenzake wazuri wakafanya kazi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi ninachokiona tusichanganye mambo haya. Hili Bunge limejaa wasomi, wewe mwenyewe ni msomi wa *Degree* Tatu za Sheria, hebu tuende sawa tunapofanya maamuzi kama Bunge tuweke *legacy* na heshima ya Bunge hili. Tuelekeze *TANROADS* waachie miradi ya Viwanja vya Ndege, iende chini ya *TAA,* kama kuna matatizo ya *management* Waziri ni yuleyule. Hata hivyo, kwa kukumbuka hapa Bodi ya *TANROADS* ninavyojua na ambavyo jinsi nilivyofuatilia hii ni *advisory board* siyo *executive board,* ndiyo maana wanaweza hata kupeleka vitu huko wakaingilia fanya kazi ya fulani, ikakubali fanya kazi ya fulani ikakubali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapoongelea Uwanja wa Ndege, unapokuwa unajenga uwanja wa ndege huongelei *runway, runway* ndiyo barabara. Uwanja wa ndege una vitu vingi, una majengo pale, ina watu wa umeme na nini, sasa unajiuliza *TANROADS* ni Mkandarasi ndani ya ile Wizara anayetakiwa afanye kazi za wenzake au *TANROADS* ni nani ndani ya ile Wizara?

Mheshimiwa Spika, hivyo ninaomba kama *TANROADS* ana cheti cha ukandarasi tukakutane naye *site* tushindane naye, lakini kama hana cheti cha ukandarasi, miradi ya viwanja vya ndege irudishwe *TAA,* kwa sababu hii Miradi inafanywa kwa *standard*. *International Civil Aviation Organization* wametoa *standard* za kujenga viwanja vya ndege. Sasa sielewi *TANROADS* ya Tanzania yenyewe mpaka inajua, kesho tutawakuta na kwenye reli hawa kama hatutangalia hapa, tutakuja kuambiwa *TRL* hawafanyi vizuri *SGR* ipelekwe *TANROADS* tena. Kwa hiyo, ninachoomba tusimame kwenye *standard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Wananchi wa Tanzania, kama ni Bunge la Wananchi wa Tanzania kila mmoja afanye kazi zake kwa mujibu wa Sheria maana hizi *Organizations* au hizi Taasisi zimetundwa kwa Sheria ya Bunge, tusizibadilishie matumizi kwa mtu mmoja kukaa na kuamua anavyotaka wakati vitu hivi vimetungiwa na Sheria na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba juu ya hayo tuyaangalie ili yaweze kutusaidia, kesho na keshokutwa tutakapokuwa tunakimbizana na hasara kama hizi, huyu unayempelekea mpaka na viwanja vya ndege ametusababishia hasara namna hii na bado

tunazidi kumrundikia kazi. Kwa hiyo, ningeomba tuliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia najaribu kupitia hapa tena kwenye suala la miradi ambayo baadhi ya Wakandarasi wamepewa. Kuna Wakandarasi wametutoza *penalty* huko kwenye ile Billion 68, *yet* tumeenda na tumewapa na kazi nyingine kubwa tu wamesaini hivi karibuni na wanaendelea nazo. Sasa unajiuliza hawa Wakandarasi wa nje wana mapenzi gani na sisi? Wanatutoza *penalty* tunawalipa na bado tunawapa kazi nyingine wanaendelea nazo. Naomba tutoe kauli kwamba miradi hii ikae chini ya taasisi na hatimae iweze kufanyika, hata Watanzania wanapokosea au wanapocheleweshewa malipo na wenyewe pia walipe *penalty* kama hizi. Kwa sababu haiwezekani mtu anayetoka nje ya nchi tunampa pesa halafu wa ndani ya nchi tunamnyima.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja mbalimbali za Kamati ambazo zimewasilishwa ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wetu wa Kamati ambao wamewasilisha Taarifa

nzuri, pia Kamati zimefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kutoa maoni na kuishauri Serikali katika maeneo ambayo tumeona kuna changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhangaika kule na kule kutafuta fedha kwa ajili ya Uwekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Nchi yetu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, wetu kwa kuridhia fedha za *export levy* asilimia Hamsini kurudi katika Mfuko wa Maendeleo ya Korosho. Fedha hizi tulikuwa tumezikosa kwa kipindi cha muda karibia wa miaka Minne, mitano pia tulipata changamoto mbalimbli katika kuhakikisha kwamba zao la korosho linaendelezwa kama ambavyo tumelikusudia. Kwa hiyo, niishukuru sana Serikiali kwa kutoa uamuzi huu wa kuhakikisha kwamba asilimia 50 inarudi katika Mfuko wa Maendeleo ya Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba sana Bodi ya Korosho kuhakikisha kwamba fedha hizi zinasimamiwa ipasavyo katika matumizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Korosho. Tunajua kwamba Wakulima wetu walipata changamoto mbalimbali lakini hata Bodi ilipata changamoto katika kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao za kuhakikisha kwamba zao hili la korosho linaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Shirika letu la Maendeleo Tanzania (*NDC)*. Tumekuwa na mradi huu wa Mchuchuma na Liganga wa muda mrefu lakini tunashindwa kutekeleza kutokana na changanoto mbalimbali ziliyopo, ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba inamaliza mazungumzo na Mwekezaji huyu *GNT*

kuhakikisha kwamba *NDC* sasa wapewe fursa ya kuendeleza mradi huu wa Mchuchuma na Liganga. Ni mradi mkubwa, mradi ambao utatuletea fedha nyingi na utatuingizia mapato ya kutosha pia tutakuwa na ajira nyingi za kutosha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie suala la Shirika la *TPA* kwa maana ya Mamlaka ya Bandari Tanzania. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu amewekeza fedha nyingi katika kuhakikisha kwamba Babdari ya Dar-es-Salaam inapanuliwa, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kutoa huduma mbalimbali lakini kuongeza Mapato ya nchi yetu na kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaendelea kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais amewekeza katika mradi mkubwa wa *SGR*. Sasa ninaomba ndugu zangu wa bandari wachangamkie fursa hii, kuhakikisha kwamba wanajipanga vizuri kuona namna ya kutumia usafirisahaji wa mizigo kutoka bandarini kwa kutumia njia hii ya reli kupitia mradi wetu wa *SGR* ili kusafirisaha mizigo mbalimbali ambayo inatoka bandarini.

Mheshimiwa Spika, *SGR* inauwezo wa kusafirisha tani 10 kwa safari moja, kwa hiyo tutakuwa tumenusuru na tumesafirisha mzigo mkubwa kwa haraka, pia tutakuwa tumeongeza mapato na ajira na wadau mbalimbali wataendelea kufurahia huduma ya bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais pia, amewekeza katika mradi mkubwa wa *SGR*. Sasa ninaomba ndugu zangu wa bandari wachangamkie

fursa hii, kuhakikisha kwamba wanajipanga vizuri kuona namna ya kutumia usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini kwa kutumia njia hii ya reli kupitia mradi wetu wa *SGR* ili kusafirisha mizigo mbalimbali ambayo inatoka bandarini. *SGR* ina uwezo wa kusafirisha tani 10 kwa safari moja. Kwa hiyo tutakuwa tumenusuru na tumesafirisha mzigo mkubwa kwa haraka, lakini pia tutakuwa tumeongeza mapato na ajira na wadau mbalimbali wataendelea kufurahia huduma ya bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba ndugu zetu wa *TICTS* wanaosafirisha ma-*container* kutoka bandarini; uwezo wa bandari yetu ni mkubwa sana. Kamati yetu imetembelea katika Bandari yetu ya Dar-es-Salaam na tumeona huduma ambazo zinatolewa katika bandari ile. Hata hivyo, tuna changamoto kubwa kwa ndugu zetu wa *TICTS* hawa katika *terminal gate number* 8, 9, 10 na 11, na juzi madereva wamefanya mgomo kwa sababu ya huduma mbovu inayotolewa na ndugu zetu hawa wa *TICTS,* wanasababisha wanaotumia Bandari yetu ya Dar-es-Salaam kuona kwamba kuna changamoto na hatimaye tunaweza tukapoteza sifa ya Bandari yetu ya Dar-es-Salaam; na Bandari yetu ndio roho ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe ndugu zetu wa Bandari kuhakikisha kwamba wanaendelea kufanya mazungumzo ya kimkataba na ndugu zetu hawa wa *TICTS* ili waendelee kutoa huduma nzuri na bandari yetu iwe na sifa ya kuendelea kutumika katika nchi yetu. Niwaombe pia ndugu zetu wa Bandari kuhakikisha ujenzi wa magati mapya ya namba 12, 13, 14 na 15; kuhakikisha kwamba upanuzi huu unaendelea kufanyika na bandari yetu iendelee kuwa na sifa ya wadau na wawekezaji mbalimbali waweze kutumia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, sasahivi Serikali inabidi tujipange kuhakikisha kwamba tunapanua bandari kwa kujenga Bandari ya Bagamoyo. Kwa sababu sasahivi ukiangalia Bandari ya Dar-es-Salaam imeshasheheni. Na ukiangalia baada ya miaka 10 Bandari ile itakuwa imeelemewa. Kwa hiyo ni wakati muafaka sasa wa kuhakikisha kwamba, Serikali inajipanga vema kuhakikisha kwamba tunajenga Bandari yetu ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo ambalo tulishaondokananalo, lakini sasahivi linaanza kunyemelea katika Bandari yetu ya Dar-es-Salaam. Wanaopokea mizigo yao kuna kasoro ndogondogo za wizi wa vitu vidogovidogo. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali, niwaombe ndugu zetu wa Bandari kuhakikisha kwamba wanaendelea kuimarisha ulinzi ili kuhakikisha kwamba wanaosafirisha na kupokea mizigo yao basi iwe salama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hayo ni mambo muhimu sana katika mashirika yetu kuhakikisha kwamba wanaendelea kusimamia huduma zetu vizuri na wananchi mbalimbali waendelee kutumia Bandari yetu ya Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini ninajua ya kwamba, Serikali imewekeza fedha nyingi ili kupanua Bandari ya Tanga, pamoja na upanuzi wa Bandari ya Mtwara. Tuhakikishe kwamba tunaendelea kusimamia huduma zile muhimu ambazo zinahitajika katika maeneo ya bandari hizi ambazo nimezitaja ili ziendelee kufanya kazi vizuri. Tunaona kwamba Serikali imefanya kazi kubwa na imesogeza huduma karibu kwa wananchi, lakini pia imepunguza msongamano mkubwa ambao ulikuwa unajitokeza pale Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *TARURA*. Tunayo changamoto katika eneo hili la *TARURA*. Tunaona kwamba Serikali imewekeza sana fedha nyingi, lakini tunaona uwezo wa *TARURA* kuna upungufu mkubwa wa ma-*engineers* katika maeneo ya Halmashauri zetu, tumeona pia kuna changamoto ya uwepo wa Ofisi za *TARURA* pamoja na changamoto kubwa ya uwepo wa magari. Kwa hiyo ndugu zetu hawa wanashindwa kusimamia kwa sababu ya ukosefu wa vifaa hivi. Ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba tunakamilisha kuwa na ofisi za *TARURA,* lakini kuwa na vitendea kazi vya kuwarahisishia kufuatilia ujenzi mbalimbali ambao unaendelea katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru sana lakini pia niunge mkono ushauri uliotolewa na Kamati ya *PIC* pamoja na hoja ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na wewe nakutakia kila la heri, Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mheshimiwa Mwita, Mwikwabe Waitara ajiandae.

Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Miradi inayohusisha fedha za umma ama

fedha za Watanzania lazima itekelezwe kwa kuzingatia masuala yafuatayo; moja, lazima ichagize ufanisi; pili lazima iendane na thamani ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi; tatu, lazima iwekewe ushindani; nne lazima ilete maendeleo ya kuiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya umma ni lazima zitekelezwe kwa uadilifu mithili ya matendo ya mke wa mfalme, isiwe hata ina thumni ya udanganyifu ama isiwe hata ina thumni ya ubadhirifu wa aina yoyote. Miradi inayoendeshwa kwa fedha za Watanzania ambazo ni fedha za umma lazima iendeshwe kwa uwazi, kwa sababu rushwa mwenzake ni siri. Miradi yoyote inayoendeshwa kwa usiri mkubwa bila sababu za msingi lazima ilete mianya ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima ifahamike, kwamba, wale waliopewa dhamana ya kusimamia miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha umma lazima wafahamu kuwa hawana hati miliki ya miradi hiyo. Zile fedha ni za Watanzania. na kwa sababu tumewaamini kwa majukumu hayo lazima watekeleze majukumu hayo kwa uadilifu mkubwa, kwa kuzingatia sheria na taratibu na wahakiishe fedha za umma zinatumika kwa maslahi ya Watanzania, lakini si kwa maslahi ya mtu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii inapambana na umasikini kwa kiasi kikubwa sana. Nchi hii mpaka leo tunapambana na kupeleka huduma za msingi kwenye jamii, tunapambana na huduma za afya, tunapambana na huduma za maji, tunapambana na huduma za umeme, barabara; ni kwa sababu wananchi hawajafikiwa. Nchi hii mpaka leo Watanzania asilimia 28 ni masikini wa kutupwa wa huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii Mtanzania wa kawaida pato lake la kila siku ni 2,798/= na si kila Mtanzania anaweza kupata kiasi hicho cha fedha. Nchi hii bado tunapambana na Watanzania. Sasa inasikitisha, inashangaza, inahuzunisha kuona baadhi ya watu wanaweza kupandisha mabega juu wakajivika viti vya ufalme na kutumia fedha za umma kwa udanganyifu, kwa kiburi kikubwa na kwa uthubutu uliopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Tanga ni mojawapo ya bandari zenye umuhimu mkubwa si tu kwa Taifa letu la Tanzania bali Afrika Mashariki. Bandari hii hivi karibuni imefanyiwa maboresho kwa kuongeza kina pamoja na ujenzi wa gati ili kuweza kuongeza ufanisi katika kuhudumia mizigo kutoka tani laki saba hadi tani milioni tatu. Zoezi hili lilifanyika kwa kuongeza kina cha maji mpaka kufikia mita 13, lakini vilevile pamoja na ujenzi wa gati.

Mheshimiwa Spika, wakati wa maboresho ya bandari hii kina cha maji kilichokuwa kinaongezwa ilikuwa ni katika eneo la kuingilia baharini ambapo zamani mizigo ilikuwa inaenda kuchukuliwa baharini kwa kadiri ya kilometa 1.7, kwa hiyo maboresho ilikuwa ili ule urefu upungue mpaka kufikia mita 200. Hili lilikuwa ni jambo jema na kwa dhamira njema kwa maslahi ya taifa letu, lakini katika mchakato huu tumepigwa.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya CAG inasema, udanganyifu mkubwa umetokea katika zoezi hili la maboresho ya kuongeza na kufanya marekebisho katika Bandari hii ya Tanga. Tarehe 03 Agosti, 2019 Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba pamoja na mkandarasi mkuu kwa ajili ya kufanya maboresho katika bandari ya

Tanga. Mkandarasi huyu mkuu ni kampuni inaitwa kampuni ya *CHEC*.

Mheshimiwa Spika, wakati mkataba huu unaingia kazi iliyotakiwa ifanyike pale ilikuwa ni ya thamani ya bilioni 176.36 ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari iliiingia na Kampuni ya *CHEC* ambaye ndiye mkandarasi mkuu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hii. Kampuni hii ilipewa kazi na Mamlaka ya Bandari kwa kazi kuu tatu; moja kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika bandari ya Tanga; mbili kufanya tathmini ya athari ya kimazingira; tatu kununua vifaa kwa ajili ya shughuli za bandari.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu walioingia kati ya hawa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari pamoja na Kampuni ya *CHEC* ulikuwa ufanyike kwa kipindi cha mwaka mmoja kutoka tarehe 03 Agosti, 219 mpaka Agosti, 2020. Japo baadaye sasa kutokana na changamoto walizoelezea mkataba ulikuwa *extended* kwa mwaka mmoja kwa sababu haukuweza kumalizika mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Mkataba ule ambao ni kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na mkandarasi mkuu, Kampuni ya *CHEC*, ulikuwa una mapungufu makubwa sana. Moja, Kampuni ya *CHEC* ambaye alikuwa ni mkandarasi mkuu kabla hajapewa mkataba na bandari alikuwa ameshaingia mkataba na mkandarasi ubia kwa ajili ya kumpa kazi ile ambayo alikuwa anaenda kufanya na usimamizi wa bandari. Yani kazi yake aliyokuwa anapewa alikuwa ameshaenda kumpa *third part* aifanye, na aliingia mkataba huo na kampuni ubia ya Kitanzania tarehe 01 Agosti, 2019 kabla hajapewa mkataba na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari.

Mheshimiwa Spika, baada ya siku mbili ndipo mkandarasi mkuu Kampuni ya *CHEC* akaenda kupewa kazi na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Katika mkataba aliousaini, Kifungu kidogo cha (4.4) kinasema, hairuhusiwi mkandarasi mkuu kwenda kugawa kazi ambazo amepewa kwenye mkataba, labda kama ni ulazima lazima atoe *notice* ya kabla ya siku 28 kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, kama hiyo kazi ina umuhimu wa kwenda kuitoa. Cha kushangaza masharti hayo hayakufuatwa kwa sababu, mkandarasi mkuu tayari alikuwa ameshaingia mkataba na mkandarasi mbia wa kumpa kazi hata kabla hajasaini mkataba na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi mkandarasi mkuu, Kampuni ya *CHEC* baada ya kusaini mkataba na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, mkataba wa bilioni 176 akaenda kuigawa kazi ile kwa mkandarasi mbia kwa gharama za chini. Kazi aliyompa mkandarasi mbia ilikuwa ni ile kazi moja ya kuongeza kina na ujenzi wa gati, kazi ambayo ilikuwa inagharimu takribani asilimia 60 ya fedha yote bilioni 176, ile kazi ni ya bilioni 104 kwa ajili ya ile kazi ya kwanza ndiyo akampa mkandarasi mbia. Lakini badala ya kumpa kwa bilioni 104 aliyoichukua Serikalini akampa kwa bilioni 40. Kwa hiyo, mkandarasi mkuu hakufanya kazi, kazi akampa mkandarasi mbia kwa bilioni 40, bilioni 64 akaweka mfukoni.

Mheshimiwa Spika, wakati haya yanatokea Mamlaka ya Bandari ipo, Katibu Mkuu yupo, Naibu Katibu Mkuu yupo, Mkurugenzi wa Bandari yupo na Waziri yupo. Ubadhirifu kama huu unafanyika mbele ya macho yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki, bilioni 64 ingeweza kujenga madarasa 3,200, lakini kampuni, tena ya kigeni, bila ya woga wa aina yoyote, inaenda kinyume na masharti ya mkataba, anagawa kazi hata chini ya nusu ya bei ya fedha ya Watanzania aliyopewa. Zaidi ya nusu ya fedha, bilioni 64 kati ya bilioni 104 ya kazi moja tu anaweka mfukoni; inawezekana vipi? Kwenye nchi hii ya masikini asilimia 28 ya Watanzania inawezekana vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza zaidi ni kwamba, Kamati hawakuliona? Mbona haipo kwenye ripoti yao? Imekuwaje? Hawakupata maelezo kutoka Serikalini? Wakati wanafanya majumuisho watuambie kwa nini hawakuliweka jambo kubwa kama hili linalogusa maslahi ya Watanzania na fedha za umma kwenye ripoti ya kamati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikubaliki.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

## T A A R I F A

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Kapinga; ukisoma Ripoti ya *CAG* na kile ambacho Kamati imeleta, hawaku-*cover* maeneo yote, *it is hardly like 10 percent* tu. Sasa labda kama Bunge na wewe Mheshimiwa Spika, nampa tu taarifa lakini, tuangalie uwezekano labda wa ku-*extend* muda ili kamati iweze

kupata muda mwingi wa ku-*cover* ripoti nzima, lakini *as it stands* haija-*cover* maeneo yote.

**SPIKA:** Sasa hiyo ni taarifa kuhusu hoja gani? Au ni pendekezo? Mheshimiwa Judith endelea na mchango wako, nadhani yeye ametoa mapendekezo.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, hii imetoka kwenye Ripoti ya *CAG* kuhusiana na ukaguzi wa mashirika ya umma. Suala kama hili hata kama kamati ilikuwa ina muda mchache *it can't go under looked* ni suala liko *obvious* na ubadhirifu wa wazi. Yaani hata ukipima yale masuala makuu yaliyoletwa na Kamati hili lilitakiwa liwepo ndani ya ripoti ya Kamati. Kwa hiyo, Kamati ya *PAC* itakapokuja kujumuisha watuambie ilikuwaje hapa hili halikuwekwa hata katika yale au wali-*discuss* nini? Serikali ilitoa majibu gani; ili tuweze kupata, kwa sababu huu ni wizi wa wazi kabisa; ni udanganyifu wa wazi kabisa, yaani hauna konakona. Kwa hiyo, kamati inavyokuja kufanya majumuisho watuambie.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba kupendekeza; kwa sababu fedha za umma ni fedha ambazo zinakusanywa kwa Watanzania kwa jasho, mpaka leo tunahangaika na mikopo ya watoto wetu vyuo vikuu, tunahangaika na vituo vya afya, tunahangaika na barabara, tunahangaika na *TASAF,* halafu anakuja mtu anachukua bilioni 64 kiurahisi namna hii. Imeshapita miaka miwili, vyombo vya ulinzi na usalama viko wapi? TAKUKURU iko wapi? Kuna mtu hapa hafanyi majukumu yake inavyotakiwa. Tunaomba maelezo ya kina *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashindwa hata kusema maazimio kwa sababu, sijui kamati wali-*discuss* ama hawaku-*discuss* ama ilikuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama kutakuwa kuna maelezo naomba tuazimie kwamba hatua za haraka zichukuliwe kwenye jambo hili na wahusika wafikishwe kwenye vyombo vya ulinzi na uaslama.

Mheshimiwa Spika, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, kengele ya pili ilishagonga, lakini nakuongeza dakika tatu umalizie hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, sisi kama taifa. Sisi kama Wabunge tuliopewa dhamana tuna haki ya kuwa vinara kwenye kulinda fedha za umma. Tuna haki ya kuwa vinara kwenye kulinda fedha za umma. Kama kuna watu waliambiwa walete taarifa, hawakuleta, wanapaswa kuwajibishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupelekana kwenye vyombo vya usalama ni *end result*. Tangu mchakato unaanza wahusika walikuwepo wapi? Sheria na taratibu zinaonesha, yaani kila siku tutakuwa tunashikana mashati mwishoni?

Mheshimiwa Spika, lazima kama Taifa tuhakikishe fedha za umma ambazo ni fedha za Watanzania zinatumika kwa maslahi ya Watanzania kwa ujumla. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwamba, sasahivi fedha nyingi sana zinaenda katika Halmashauri katika miradi mbalimbali. Takriban kila Mbunge hapa ana jambo la kusimama na kusema juu ya Mheshimiwa Rais na juu ya Serikali ya Awamu ya Sita, tunamshukuru sana kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais alitoa muelekezo kwa wewe Mheshimiwa Spika na Wabunge ambao mlisaidia kusema; wananchi wa Tarime Vijijini wanashukuru sana kwamba, ile fedha ya *CSR* imetoka na miradi sasa inaendelea; hali ya kisiasa itakuwa tulivu jimboni.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais ametoa fedha ambazo kwa sasa vijana wa darasa la saba wakimaliza mitihani yao mwakani wataingia *form one* kwa kuwa madarasa yamejengwa na kazi inaenda mchakamchaka sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza *CAG* kwa kazi ambayo anaifanya. Ametoa taarifa ambayo kila Mbunge akisoma baadhi ya mambo ambayo yapo

kwenye majimbo yetu tunayaona kwenye ripoti hii. Tunamshukuru na tunaomba aendelee hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini ziko changamoto nyingi sana. Na ukitaka kusaidia Watanzania wakati ukiwa umekalia hicho Kiti kwa muda ambao Mungu atakupa na sisi kukujalia kuendelea kukaa hapo ni kuangalia namna ambayo tutapitia mfumo wa Serikali za Mitaa Tanzania. Mfumo huu umeanza tangu mwaka 61, ukashindwa 71, ukawa *resumed* mwaka 82, tukaanza *operation* mwaka 84; ni miaka 38 mpaka sasa tunao mfumo huu. Kunakuwa na *changes* ndogondogo sana.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yote humu Wabunge wakisimama tunazungumza fedha ambazo zikienda kwenye majimbo yetu zitaondoa kero za Watanzania ambao wametuchagua sisi kuja kukaa kuzungumza. Tunazungumza hoja ambazo kila Mbunge angetamani fedha zinazotajwa hapa, haya mabilioni yanayotajwa kwa namna mbalimbali kwamba, yamepotea tungetamani yaende yakaondoe changamoto za barabara, maji, afya, shule, mikopo watu wawasomeshe Watanzania wapate elimu na huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo ni muhimu sana kwa sababu tunazungumza hapa fedha nyingi katika halmashauri. Tuchukue mfano rahisi, tulipata fedha za Uviko zikaja kwenye majimbo. Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo, Wakuu wa Mikoa na Ma-*DC* wakafanye *special operation,* yale madarasa yakajengwa ndani ya muda mfupi yakakamilika. Malalamiko ni machache, lakini fedha hizi za Serikali, za wananchi kule, hili ni shamba la bibi, ndiyo fedha ambazo zimeibwa sana na

zimeliwa. Miradi mingi katika maeneo haya haijakamilika, na hoja nyingi ukisoma zinajirudia.

Mheshimiwa Spika, *CAG* miaka miwili mpaka mitatu nyuma alisema hoja ile ile. Sasa kama kuna mtu yupo mahali alipewa hoja mwaka uliopita, mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na mwaka huu imejirudia, mwakani ataleta *story* hiyo hiyo, kwa nini watu hawa wasiwajibishwe? Kwa nini wasichukuliwe hatua? Hawa ni watumishi, CAG na watu wake, wanalipwa posho, wanatumia muda, akili na damu, wanasafiri wanaumia, hawa wakienda wakaleta ripoti tunatarajia mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia michango ya Wabunge humu ndani, watu wanaumia sana, kwamba tunazungumza kwamba kwenye majimbo yetu kuna changamoto, tuna shida na watu wetu, lakini tunaambiwa fedha zimekusanywa, zimepotea. Ripoti hii imetoa tathmini ya ukaguzi wa fedha. Tungetaka tupate ripoti nyingine sambamba na hii ambayo inaonesha, watumishi ambao wamekula fedha za Umma ni akina nani; na wapo wapi; wanafanya nini kwa sasa? Lazima watuoneshe.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ameonesha fedha ambazo zimepotea, tupate ripoti ya wale ambao wamehusika. Yaani haiwezekani watu hapa watoe mishipa kujadili fedha imepotea, halafu kuna mtu anakula kiyoyozi tu, au mwingine amehamishwa kutoka *point* A kwenda *point* B. Hii haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, tukitaka kupiga hatua; tena Mheshimiwa Rais wetu yuko China, ningeomba akope sheria za Wachina kidogo tu, siyo zote, watu wa namna hiyo kule China hawawezi ku *survive*. Umefanya kosa,

imethibitika, hujaonewa, unawajibishwa, anakaa mtu mwingine. Wapewe nafasi watu wenye uwezo huo. Kama mtu amekaa mahali kwa bahati mbaya, atoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mjadalla wa sasa hapa, hata huko mtaani watu wanatushangaa. Tulikuwa tupewe hapa ripoti wahusika wote wakiwa korokoroni, ndiyo tunazungumza hapa. Anaitwa mmoja mmoja, anaulizwa fedha ziko wapi? Rudisha, kama umemeza, tapika fedha ili zirudi katika eneo lake. Ndiyo hoja ya msingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni mjadala hapa wa maneno mengi; kwa mfano, unaposema *MSD* wanaidai Serikali Shilingi bilioni 250, halmashauri tumekabana mashati, mia mbili mia mbili; mia tano, mia tano; buku buku; tumepeleka fedha pale kuomba dawa. Dawa hazijaja, kumbe hawa wanaidai Serikali hawajalipwa fedha. Sasa Mbunge unasema nini kwenye jimbo lako? Yaani wananchi wametoa kodi wamelipa kutoka mazao yao na shughuli mbalimbali, fedha imepatikana, tumepeleka pale *MSD,* dawa hazipo. Kwa hiyo, mzigo huo siyo wa kwetu. Tunaomba hao watu walipwe fedha ili wananchi wapate dawa na huduma kama ambavyo wamechangia.

Mheshimiwa Spika, hizo fedha wamepeleka miaka miwili mpaka mitatu hawajarejesha, dawa hazipo, fedha wamechukua na maelezo hamna, na watu wapo ofisini. Mimi naona hii siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine nataka nizungumze, kwenye halmashauri zetu na ndiyo maana naomba tupitie huu mfumo wa Serikali za Mitaa.

Halmashauri zile, Mbunge anazungumza hapa, ikitokea kuna shida kwenye jimbo, Mbunge utaulizwa, hujasemea watu wako, hufanyi kazi nzuri, lakini twende kwenye maeneo yetu, kuna maagizo ambayo Katibu Mkuu *TAMISEMI* anamwagiza Mkurugenzi. Mkurugenzi anaitwa Dodoma halafu anapewa maagizo, na halmashauri Madiwani wamepitisha mipango yao. Sasa wanasigana; Mkurugenzi ameambiwa lazima nitekeleze hili. Fedha nifanye *re-allocation* ifanye mradi fulani, na mradi huo haukupendekezwa, mradi wa Madiwani ni tofauti na ule pale. Kwa hiyo, Mkurugenzi anasimama kwamba bosi amesema lazima lazima nitekeleze; Madiwani wanasema, hiki siyo kipaumbele chetu; Mbunge anasema yuko kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekusikia umesema mara kadhaa kwamba kama Bunge likiisha kwa mfano 2025, wengi hapa asilimia 60 mpaka 70 hatutakuwepo. Sababu mojawapo ni miradi kwenye halmashauri na maagizo mbalimbali. Wapo Wakurugenzi kwenye halmashauri zetu hawafanyi kazi. Anaitwa mkoani asubuhi mpaka jioni, kaenda na gari, kaenda na dereva, kapewa maagizo; maagizo hayo, Mbunge hajui, Mwenyekiti wa Halmashauri hajui. Kwa hiyo, kuna shida. Kwa hiyo tuangalie hata mfumo wetu unavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hawa wakurugenzi pia wapewe watu wenye uwezo. Zamani walikuwa wanateuliwa miongoni mwa Watumishi wa Umma. Wanafanyiwa *vetting,* wana uzoefu. Leo kwa mfano ukimwuliza *CAG,* kwenye halmashuri hizi atuambie maeneo ambayo watu wameshindwa kuandaa ripoti ni wangapi? Pale Tarime ili wafunge mahesabu walikuwa wanaenda kuazima watu Serengeti. Wataalamu hawapo. Kwa hiyo, tunazo hoja nyingi sana za kuangalia.

Mheshimwa Spika, naomba kwamba fedha ambazo zimepotea, wamezungumza, sitaki kusema kwa sababu nilikuwa kule Tanga, lakini nimefurahi kuiona kwenye ripoti hii. Haya mambo yapo, yamefanywa, na wahusika wapo, peleka ukaguzi maalumu Bandari ya Tanga, watu wawajibishwe, tupone. Ukitaka kutengeneza taswira nzuri, kama kuna mtu amepoteza fedha ya Serikali, halafu amewajibishwa, hata kizazi kingine kitajifunza. Kama kuna mtu amepoteza fedha na hakuwajibishwa kwa sababu ni mjomba, shangazi, mnafahamiana, ni ukanda, kabila moja, hili Taifa litakufa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kujadili taarifa ya Serikali za Mita. Mimi nitajikita huko.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kilio cha Waheshimiwa Wabunge wote, kila aliyesimama analizungumzia kwa uchungu mkubwa sana suala hili. Naomba tusimalize kwa kuzungumza peke yake, tuje na maazimio makali ili Bunge hili liwe ni mfano ambao mtu mwingine yeyote aweze kufanya *reference* kwamba Bunge hili chini ya Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia walisimama wakakemea na wakachukua hatua kupinga ubadhirifu unaofanywa katika halmashauri zetu. Hiyo ndiyo *opening statement* yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye tathmini ya Mkaguzi. Ukifungua kwenye ukurasa wake wa tano, kwanza kabisa anasema, amefanya tathmini ya mifumo ya utawala ambayo tumeizungumzia na amebaini migongano ya kimajukumu kati ya wachaguliwa kwa maana ya Madiwani na watendaji. Hii migongano aliitolea mifano ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa au Madiwani kusaini Mikataba. Hapa ndipo penye matatizo na ulaji uko hapa. Ndiyo maana utakuta kwamba kwa kuwa tunafanya kazi pamoja, sioni Madiwani pamoja na sisi kuwa na *political will* ya kusimama na kukemea huu ubadhirifu. Kwa maana na sisi ni sehemu, si tunaitwa Madiwani na tunatoka katika halmashauri!

Mheshimiwa Spika, ukiangalia dhana nzima ya utawala bora inatuhitaji hata sasa katika Serikali za Mitaa tuwe na *separation of powers.* Hii dhana ambayo iko katika Serikali kuu inapaswa kushuka chini, madiwani tubakie au na kazi ya usimamizi na watendaji wafanye kazi za utendaji. Haya ndiyo matatizo, ingawa ndiyo sharti la kisheria la sasa hivi, lakini kwa miaka 38 mfumo huu haujatusaidia. Ni wakati wa kuungalia mfumo kwamba haufai.

Mheshimiwa Spika, kwa nini haufai? Hakuna ripoti ya *CAG* ambayo kwa mwaka mmoja itakuwa inaonesha kuna matumizi mazuri ya fedha za Serikali, hakuna. Kila mwaka kuna matatizo. Hebu chukulia mfano, fedha ambazo tunazipitisha hapa katika Bunge lako Tukufu, utakuta kati ya asilimia 60 mpaka 75 na kuendelea zinapelekwa katika Serikali za Mitaa, na kule ndipo tunapotegemea pajengwe shule, hospitali na huduma nyingine za wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu haujaonesha pia pesa za *COVID* ambazo nazo zilikwenda kufanya kazi hiyo hiyo. Je, leo ukaguzi ungeonesha fedha za ndani zimeliwa hivi na fedha za *COVID* zimeliwa hivi, pangekalika humu ndani? Sasa nilikuwa nashauri kwamba kwa kuwa ukaguzi umefanyika, matokeo yametokea, ningemwomba *CAG* akaangalie pia fedha za *COVID*. Kwa sababu ukiisoma hii taarifa kuna mambo mengi sana hasa yale ya *re-allocation* yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, fedha imeingia, inaonekana hii imekwenda kujenga shule fulani; na hii imetokea pale kwenye jimbo langu. Shilingi milioni 600 zimeletwa kwa ajili ya *Secondary School* Tandale, zimeondolewa zikapelekwa mahali pengine na shule haijajengwa. Haya mambo hayakubaliki. Ukiangalia haya yote ni kwamba hawa watu hawana uwoga kabisa. Wamejawa na dharau na siyo dharau tu, na jeuri, naweza kuthubutu kusema ni jeuri kwa Rais na kwa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unawezaje kupewa maagizo na Kamati ya *LAAC,* Kamati ambayo ni sehemu ya Bunge; kamati ikizungumza Bunge limezungumza. Kamati inatoa maagizo, wewe huyatekelezi, kama siyo dharau maana yake ni nini? Kuna tafsiri nyingine yoyote hapo? Bunge linaelekeza ukafanye moja, mbili, tatu, nne, nawe huyafanyi, unatarajia nini? Unatarajia kwamba huna utakachofanywa. Ndiyo maana kwenye *opening statement* yangu nimesema na kila mtu amezungumza, kwamba lazima tuje na mfano kwamba hawa watu, hatua za kishera zianze kuchukuliwa. Kama ukaguzi huu ni *sampling bases ten percent:* Je, hizo asilimia 90 zingeonesha nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mengine humu yanaonesha kabisa ni uhujumu Uchumi. Unapokeaje risiti ya kugushi. Jamani Waheshimiwa Wabunge, risiti ya kugushi inatafsiri ngapi? Inatafsiri kwanza kuna makosa ya kugushi; pia kuna tafsiri ya uhujumu uchumi ndani yake. Tumewaona hapa miaka miwili, mitatu iliyopita watu wanaotiwa ndani kwa ajili ya uhujumu uchumi. Lina tafsiri gani hili suala kama siyo uhujumu uchumi? Ukiikosesha mapato Serikali na ukiyatumia mapato ya Serikali visivyokusudiwa, yote hayo ni makosa. Tukikaa kimya na hili likapita; na humu ndani naona *CAG* ametumia lugha nyepesi, anawaambia TAMISEMI chukueni hatua hizi; maeneo machache, TAKUKURU chukueni hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako liazimie kwamba wale wote wenye dalili za kijinai katika ripoti hii watambulike walipo na wachukuliwe hatua. Kila ambaye amefanya kosa la dalili za kijinai za ubadhirifu wa fedha za Serikali achukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge hapa tumedharaulika sana wakati tunapitisha tozo, wametusema sana katika mitandao ya kijami. Uongo, kweli! Tumesemwa sana! Zile fedha tukazipata, tukazipeleka huko kwenye kujenga shule, barabara na ndiyo fedha hizi ambazo zimeliwa au hazionekani. Kama hatukuchukua hatua, leo wananchi watatuona ni watu wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kuna fedha nyingine zinapelekwa katika uwekezaji wa mitaji ambayo haina faida. *CAG* anazungumza na ametoa mifano kwamba Halmashauri sasa zinaigana katika kutengeneza miradi ya kuwekeza na wengine walikwenda kuwekeza hata katika mabenki. Kuna benki moja waliwekeza karibu *share* 24,000 ambazo

zina thamani ya Shilingi bilioni nne. Sasa hivi *shares* zile zimepungua zimekuwa za Shilingi bilioni moja. Hakuna faida kwa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama kuna sheria ambayo inasimamia mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda kuwekeza, tuilete hapa Bungeni tuifanyie marekebisho. Yawezekana kuna mambo mengine yanafanyika hatuyajui na hii ni sehemu ya asilimia kumi ya ukaguzi. Je, tungekwenda kwenye kila Halmashauri kuona wanawekeza wapi; wanafanya nini? Ni dhahiri kabisa tutakuta kuna fedha nyingi zimepotea.

Mheshimiwa Spika, kuna dharau nyingine. Mkaguzi anakuja anagundua kuna hoja 10,824; zimetekelezwa 3,511 tu ambayo ni asilimia 32. Asilimia 35 hazikuguswa kabisa. Hii ndiyo ninayosema kama siyo dharau ni nini? Wanajua kama hukutekeleza mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu, kama vile tutakavyobadilisha Bunge, Wabunge wakiondoka wanaopiga kelele kama akina Tarimba hawatakuwepo, yatapita. Haya ndiyo mazoea ambayo tumeyajenga. Bunge hili lisikubali. Kwa hali hiyo, tufanyeje?

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nilikuwa nashauri, mfumo mzima wa Serikali ya Mitaa Sheria ile sasa imechoka, inahitaji kuangaliwa. Sheria lazima tuifumue, hata Rais mwenyewe amesema, ameona udhaifu alipokuwa amepokea hii ripoti, akawataka *TAMISEMI* waangalie. Tuangalie mifumo iliyopo haitusaidii, itupeleke kwenye *separation of powers* ikiwezekana, kila mtu afanye lake, usimamizi uwepo.

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge sioni sababu ya kuwemo katika Halmashauri. Kama hali

yenyewe ndiyo hii, maana yake na sisi tunajumuishwa. Wewe sio Mbunge; Mbunge ni Mbunge na Mbunge ni Diwani, leo tutakataa vipi ule uozo ambao umefanyika kule kama sisi sio sehemu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kamati za fedha sisi ni Wajumbe, ndiyo yanayofanyika humo. Wanafanya vikao sisi hatupo, na muda mwingi sana tuko Dodoma, halmashauri zinakutana katika mabaraza sisi hatupo. Tunaandikwa pale hakuhudhuria kwa taarifa, lakini maana yake ni sehemu ya maamuzi yanayofanyika. Sasa maamuzi yale kama yanatisha kiasi hiki na sisi tumo mle ndani, naomba kati ya mambo ambayo tuangalie, ni Wabunge tusiwe Madiwani ili tuweze kuisimamia na kuishauri vizuri Serikali, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie na mchango wangu utajielekeza kwenye taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa maana ya *PIC*.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza zaidi kwenye Bima za Ndege *(Aviation Insurance)* za Shirika letu la ndege la *ATCL*. *ATCL* imekuwa ikikata bima za ndege zetu kupitia Shirika la Bima la Taifa *NIC,* ambao nao wamekuwa wakikata bima kwa kupitia kampuni ya nje *(International Broker)* inayojulikana kwa jina la *MASH*. *NIC* wamekuwa wakifanya hivyo. Kwa kutumia mfumo wa *single source*.

Sasa kwa ufupi, kila mwaka Shirika la *ATC*L limekuwa likilipa bima ya gharama ya ndege zake, zifuatazo, nanukuu:-

"Mwaka 2018/2019 Bima ya Afya kwa mwaka ilikuwa takribani Shilingi bilioni 5.8; kwa mwaka 2019/2020, gharama ya bima kwa mwaka ilikuwa takribani Shilingi bilioni 14.5; kwa mwaka 2020/2021 gharama ya bima kwa mwaka ilikuwa takribani Shiligni bilioni 18.7 na kwa mwaka 2021/2022 gharama ya hizi bima za ndege ilikuwa takribani Shilingi bilioni 21.3."

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023, Shirika la *ATC* liliamua kuitaka *NIC* walete kampuni nyingine ambazo zinaweza zikatoa huduma hii ili kufanya ulinganifu wa gharama ya bima kila mwaka ambayo Shirika la *ATC* wanalipia. Walipofanya zoezi hilo, waliweza kupata kampuni mbadala inayojulikana kwa jina la *WILL STAWA,* ambao walitoa *quotation* ambayo ilikuwa ni pungufu ya gharama ya yule *international broker* ambaye *NIC* anamtumia siku zote kwa takribani Shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kitendo hicho, Shirika la Bima la Taifa la *NIC* lilisababisha yule *single source, International Broker* wanayemtumia *(MASH)* naye akashusha *quotation* yake kwa gharama ya Shilingi bilioni tatu ili ifikie ile ya kati ya hao wapya ambao walikuwa wamejitokeza. Jambo hilo binafsi naona lina utata kidogo, inakuwaje kwa urahisi tu uweze kushusha kwa zaidi ya takribani bilioni tatu kwenye bima za ndege kwa mwaka?

Mheshimiwa Spika, ili Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* liweze kukidhi Matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma

inatakiwa yule *international broker* awe na *partner* wa hapa Tanzania. Kwa hiyo, ndivyo ambavyo wameendelea kuwa wanafanya hivyo. Yule *partner* wa Tanzania anapata 15% ya *premium commission,* lakini ikifanyika tafiti vizuri, inaonekana kwamba yule *local partner* ambaye ameandikwa yupo tu kwenye makaratasi, haonekani katika uhalisia. Jambo ambalo nalo linatiliwa shaka na inatakiwa tuliangalie kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kwa nyongeza, nimefanya tafiti ndogo kujaribu kulinganisha gharama ya bima za ndege zetu ambazo *ATCL* inalipa, kwa kulinganisha na gharama za bima za kila mwaka ambazo Mashirika ya Ndege ya Nchi za Afrika Mashariki wanalipa. Takwimu hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kenya *Airways* wana ndege 39 na gharama ya bima kwa mwaka ni dola za Kimarekani ni milioni 9.7 kwa ndege 39;

(ii) Rwandan *Airways* wana ndege 12 na gharama ya bima kwa mwaka ni dola za Kimarekani milioni 2.8; na

(iii) Shirika letu la *Air* Tanzania lina ndege 11, lakini gharama ya bima kwa mwaka ni dola za Kimarekani 5.9.

Mheshimiwa Spika, kwa hesabu za haraka haraka, unaona jinsi gani ambavyo Shirika letu la Ndege la Tanzania *(ATCL)* linalipa gharama kubwa kwa mwaka, kwa ajili ya bima za ndege ambayo haiendani na uwiano, yaani ukilinganisha na idadi ya ndege zilizopo na hii ni kwa kulinganisha na wenzetu wa nchi jirani kwa maana ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bima za ndege kwa sasa hivi mkataba uliopo unakwenda mpaka mwezi Juni, 2023. Kwa hiyo kwa unyenyekevu mkubwa naomba kupendekeza kwamba, tuongeze nyongeza ya azimio katika mapendekezo ya Kamati hii husika, kuielekeza *ATCL* ifanye *competitive tender* zabuni kwa ushindani ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kuokoa fedha za Serikali na umma. Maana hata taarifa ya Kamati imesema kwamba *ATCL* iko taabani kiuchumi. Sasa kama iko taabani kiuchumi wakati kwa upande mwingine tunalipa gharama kubwa kuliko inavyotakiwa kwenye gharama ya kila mwaka ya bima kwa ndege, hapo tunatakiwa tufanye jambo sisi kama Bunge ili kuhakikisha kwamba tunaokoa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko pia suala la *local content*, ambalo hata Mheshimiwa Rais Samia Hassan, amekuwa akilisemea kwa mara nyingi na ushiriki wa sekta binafsi kwa Tanzania. Sasa Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* hivi sasa ni kama lina *monopoly*. Kutokana na *monopoly* hiyo, *NIC* inakuwa na mamlaka ya kuamua kutumia *single source international broker. Single source* huyo pale ambapo inaelekea anaweza akatokea mbadala mwenye gharama ya chini, amepunguza kwa urahisi bilioni tatu kwenye *quotation* yake. Jambo ambalo naomba kwa unyenyekevu mkubwa tuone namna ya kuishauri *ATCL,* ihakikishe inatangaza zabuni za bima za ndege kwa kutumia ushindani na sio *single source,* kwa sababu *single source* inaweza ikapelekea mianya ya upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge, tunao wajibu wa kuhakikisha jitihada za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan za kutafuta fedha na fursa mbalimbali kwa ajili ya

nchi yetu na Watanzania hazififishwi kwa mianya hii ya *single source*. Kwa unyenyekevu mkubwa, naomba tutoe pendekezo hili la kuhakikisha kwamba zabuni za bima za ndege za *ATCL* zifanyike kwa *competitive bidding.*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni matumizi ya TEHAMA. Hili nalo ni eneo ambalo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akilisemea kwa nguvu kubwa. Nimejaribu kutafakari katika uwekezaji wa miradi yetu mikubwa hapa Tanzania, nikifanya rejea kwenye *SGR* pamoja na mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere, ukifanya tathmini ya kujua ni makampuni mangapi ya Kitanzania ambayo yamepata zabuni za TEHAMA kwenye miradi ile, majawabu yake ni ya kusikitisha sana. Pia ukitaka kufahamu ni wataalam wangapi wa TEHAMA wa Kitanzania ambao wamepata nafasi ya kufanya na wenzetu wa nje waliopata zabuni hizo ili waweze kupata kile kitu tunachokiita *transfer of knowledge*, nayo utasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, naomba nitoe angalizo kwamba, kwenye miradi yetu mikubwa ya kimkakati, tunapotoa zabuni za TEHAMA kwa makampuni ya nje, tunajiweka katika hatari ya kiusalama wa mfumo. Suala la TEHAMA ni suala nyeti. Kwa mfano, ile kampuni ikiamua kuzima mtambo, sisi kama nchi tutafanyaje? Wakati hatutumii watalaam wetu wa ndani?

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwenye suala la Sensa. Tumekwishajidhihirisha kupitia sensa. Shirika la Takwimu la Taifa limetumia wataalam wetu wa ndani na sensa yetu imeendeshwa kidigitali mpaka watu wa Mataifa ya nje wametusifia. Kwa hiyo, tunao uwezo wa kutumia wataalam wetu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, tutoe maelekezo mahususi kuhusu Serikali kuweka jitihada pale ambapo kuna miradi ya kimkakati, hususani masuala ambayo yanaendana au yanaweza kupelekea masuala ya kiusalama, tuweke mbele kuhakikisha kwamba tunatafuta Makampuni ya Kitanzania ambayo yanaweza kutekeleza ile kazi au Makampuni ya Kitanzania yashirikiane na makampuni ya nje ili kulinda maslahi letu likiwemo suala la kiusalama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa unyenyekevu mkubwa, nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Nina masuala kama matatu; la kwanza ni sakata la *KADCO* na Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro; la pili, suala la *TIC* kwa maana kwenye Muswada wa Uwekezaji; na la mwisho, suala nguvu za Kamati zako za Bunge ambazo sisi tunazitumikia dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtumishi mstaafu, nilibahatika kufanya kazi Wizara na Maliasili na Utalii. Kipindi changu nikiwa Wizarani nilishiriki katika shughuli za kufanya utafiti wa hali ya utalii nchini na bahati nzuri nilikuwa napangwa Kiwanja wa Ndege cha Kilimanjaro kwa miaka takribani mitano mfulululizo. Utafiti huo tulikuwa tunafanya watu wa Idara ya Utalii ya Wizara ya Maliasili, *Commission* ya Utalii ya Zanzibar, Idara ya Uhamiaji Tanzania pamoja na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, kipindi chote sehemu yangu nilipangiwa Kilimanjaro ndipo nilipata kuufahamu ule uwanja na kuifahamu *KADCO*. Kwa bahati mbaya sikubahatika kipindi kile kuifahamu *KADCO* vizuri mpaka juzi baada ya kuisoma taarifa ya *CAG* na baada ya kualikwa kwenye Kamati ya *PIC* kuweza kusikiliza haya masuala yanakwendaje.

Mheshimiwa Spika, kimsingi *KADCO* kwa sasa ni kama kigenge au kibubu cha watu kufanyia maisha nje ya mfumo wa Serikali. Kinachonisikitisha sikuona kama Katibu Mkuu wa Wizara ile au watu wa Wizara kama wanaumwa na hali hii. Sinema zinazoendelea *KADCO* wao wako *comfortable* kabisa, wanapumua vizuri na wanaendelea kula vizuri kana kwamba hakuna kinachoendelea mpaka *CAG,* Wabunge na wadau ndio wanakuja kuona matatizo ya mle ndani, jambo ambalo linasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, katika ushirki wangu wa kikao, tunamhoji Katibu Mkuu na watu wake ambao walikuja jopo zima pale, Waraka wa Baraza la Mawaziri Na.5 wa mwaka 2009, ulitoa maelekezo kuwa tutanunua hisa zote za *KADCO* kutoka kwa wale wabia ambao walikuwa wajanja wajanja. Tutanunua kwa 100% baada ya kumaliza zile hisa, umiliki uende kwa *TAA*. Aidha, iendelee ku-*operate* kama kampuni tanzu ya *TAA* au *KADCO* ifariki kabisa uwanja uendeshwe *direct* na *TAA* kama wanavyofanya Kiwanja cha Dar es Salaam na viwanja vingine, lakini jambo hilo halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, tunawauliza watu wa Wizara kwa nini hamjatekeleza maagizo haya? Wanajibu, Waheshimiwa mnajua tulikuwa na mchakato wa kutafuta mbia mpya wa kuendesha. Tukawaambia *KADCO* nani

anawapa mamlaka ya kutafuta mbia, nadhani lilipaswa liwe ni jambo la Wizara na Mkuu wa masurufu *(Accounting Officer)* wa Wizara ni Katibu Mkuu pengine wangefanya wao. Hata hivyo wanasema kwamba huu mchakato tulikuwa tunafikiria kutafuta mtu. Hali ambayo inaonesha kabisa mashaka na kuna nia ovu ya wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliwahoji, kama kuna mchakato wa kutafuta mtu mpya, sasa hivi ni miaka 12, maana ni mwaka 2010 ndio tulinunua hisa zote, hivyo kampuni imekuwa ya Serikali kwa 100%. Hadi leo tunazungumza mwaka 2022 ni miaka 12, mnachakata kwa miaka mingapi kumtafuta mtu wa kuendesha? Hawana majibu yaliyonyooka, wanaongea vitu ambavyo havieleweki. Nilitamani kumshawishi Mwenyekiti tuwafukuze kwenye kikao. Kwa hekima ya Mheshimiwa Hasunga, alisema tuwasikilize mpaka mwisho, tuone inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, tukasema kama kweli huo mchakato ulikuwepo, mmetangaza wapi kwamba jamani tunatoa tangazo, tunatafuta mbia, tunatafuta mtu wa kuendesha Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro, mna tangazo ambalo mmelitoa juu ya hili? Halipo. Katika mazingira yoyote inaonekana kabisa kuna nia ovu, hawa watu hawana nia nzuri na ni mchongo tu, wanataka watupige na waendelee kutupiga zaidi.

Mheshimiwa Spika, kituko kingine, wanajibu sasa hivi tuko kwenye mchakato wa ku-*renew* mkataba wa uendeshaji, ile *concession agreement*. Awali ile *concession agreement* ilikuwa baina ya wale wawekezaji na Serikali. Sasa hivi wawekezaji hawapo uwanja ni wetu tangu awali na *KADCO* imekuja kwetu kwa 100%, Mkataba Serikali inataka isaini na nani? Maana yake

wanajadili Serikali kuingia makubaliano ya kuendesha uwanja na jini au hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna muda huwa nawaambia wenzangu tukiwa tunazungumza, muda mwingine Mungu akikusaidia ukiwa huna akili unaishi kwa amani sana, lakini ukiwa na akili utapata *stress*. Maana upeo wako ukiwa mfupi unaona kila kitu sawa tu, nyeupe na nyekundu ni sare, ndefu na fupi unaona ni sawa tu. Kwa hiyo wenzetu ambao hawana akili wanaishi sawa kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nakishangaa, kwa maana baada ya sisik kuinunua ile kwa 100% nilitarajia Katibu Mkuu wa Wizara ndiye Mkuu wa Masurufu na watu wake waiagize moja kwa moja *KADCO* iende *TAA*, maana, *KADCO* pamoja na kwamba tumeinunua haiwezi kujipeleka yenyewe na watendaji ambao wako pale wananufaika na *KADCO,* hawawezi kujipeleka na kusema tumekuja *TAA*. Ni Katibu Mkuu wa Wizara (KM) anatakiwa aiagize iende, lakini hafanyi hivyo, hakufanya hivyo na anapumua na ana amani tele kabisa, ni kituko. Kwa hiyo, mambo haya yanakera na ni mambo ya wazi kabisa, inaonesha kuna nia ovu, kitu ambacho sisi sote hatukukubaliana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa hekima za Mheshimiwa Hasunga ambaye alikuwa anakaimu Uenyekiti katika kile kikao alisema, Waheshimiwa hebu tuwape muda kidogo, maana wenyewe waliomba walisema, tunahitaji muda tukajadiliane tutaleta majibu. Tukasema kwa nini mlete majibu mkishajadiliana, mnajadiliana na nani? Katibu Mkuu wa Wizara tuko naye hapo mbele, Mwenyekiti wa Bodi na Bodi yake ya *KADCO* yuko pale, Mkurugenzi wa *KADCO* yuko pale, Mwanasheria wa *KADCO* yuko pale, timu nzima ambayo

wanayojua hili sakata wako pale. Pembeni mnaenda kujadiliana na nani ili mtuletee majibu baada ya wiki moja? Ni vitu ambavyo havieleweki. Bahati nzuri kwa hekima za Mwenyekiti, Mheshimiwa Hasunga alisema tuwavumilie kwa wiki moja, Ijumaa inayofuata watuletee majibu. Akasema pia Mheshimiwa Mgungusi tutakualika tena, uje ushiriki na hicho usione kwamba leo tunakwepesha. Hata hivyo, mpaka kesho, mpaka mwakani, hawakuleta majibu.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna picha mbili, nia ovu ya moja kwa moja, kwamba wanapiga mchongo, lakini pia ni dharau kwa Kamati yako ya Bunge. Kwa hiyo, pamoja na mambo hayo yote, nashauri kwenye sakata hili tuagize ukaguzi maalum ukafanyike kuhusu *KADCO* kuanzia mwaka 2010 tangu tumenunua hisa kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu *KADCO* hawakuwa na Mwanasheria. Kituko kingine wana-*hire* huduma mtaani kwa maana wana Mwanasheria wao *private* mtaani na wanalipa. Ukiangalia zile *legal services* za kila mwezi unaweza ukazimia, bora usijue. Kwa hiyo, siwezi nikasema mengi, naomba tukubaliane ukaguzi maalum ukafanyike kule *KADCO,* wanaweza wakaona vituko vya hatari.

Mheshimiwa Spika, kingine niseme tu, kama ikiwapendeza, naomba Katibu Mkuu wa Wizara ajitafakari kwa maana ya sehemu ya Uchukuzi, Mwenyekiti wa Bodi ya *KADCO* ajitafakari, maana ni nje ya mamlaka yangu, lakini nashauri tu wajitafakari, Mkurugenzi wa *KADCO* na safu yake, Menejimenti nzima ijitafakari. Kwa suala la *KADCO* naomba niishie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwenye Muswada wa Uwekezaji. Suala la *TIC*- Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Kwenye ule Muswada ambao tulipitia Wizara ya Viwanda na Biashara katika kipengele cha *Board Members,* Wajumbe wa Bodi ya *TIC* tulipendekeza kuwepo na Wizara ya Mambo ya Nje kama moja ya *member* wa ile Bodi ya *TIC*. Kwa sasa kuna Wizara zimetajwa, Wizara ya Fedha ipo, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI ipo lakini Wizara ya Mambo ya Nje haipo kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya *TIC*. Kwa hiyo, sisi tulipendekeza, lakini sasa Serikali nadhani hawakuichukua hii, wakaacha kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, naona haja ya Wizara ya Mambo ya Nje kuwepo *TIC* kwa sababu gani? Tunapozunguzma Uwekezaji mkubwa leo *Foreign direct investment* zinatoka nje, makampuni makubwa yanatoka nje na leo hii mnajua sera yetu sisi ya kimataifa ni diplomasia ya uchumi. Tunawataka Mabalozi wapambane kuacha siasa bali watafute wawekezaji kuja Tanzania. Wawekezaji wanakuja na mitaji yao au pengine wanakopa lakini wanaingia hapa nchini, wangependa kuona mwenyeji wao yupo kwenye huduma zao. Mwenyeji wao ni Wizara ya Mambo ya Nje kupitia Mabalozi. Inawezekanaje katika Bodi ya Wakurugenzi ya *TIC* hakuna mtu wa Wizara ya Mambo ya Nje, lakini kuna TAMISEMi? Nawaza sijui kwa nini kuna TAMISEMI au kwa sababu ya ardhi, wanamiliki maeneo, lakini Wizara ya Ardhi ipo!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulipendekeza aidha, iongezeke Wizara ya Mambo ya Nje kwenye Bodi au apunguzwe mmoja, apunguzwe hata TAMISEMI, Wizara ya Ardhi anamwakilisha, lakini hakuna sababu ya msingi ya kufanya *Foreign Affairs* asiwepo kwenye Bodi ya

Wakurugenzi ya *TIC*, maana hata wawekezaji wanapoona wanalalamika au hawahudumiwi vizuri mwenyeji wao yupo wanabanana naye pale inapendeza, kuliko mtu wa Mambo ya Nje akienda kulalamikiwa na wawekezaji wake ambao amewaleta na yeye aanze kuuliza pembeni hai-*make sense* kwa hali ya kawaida. Hivyo, napenda kushawishi Bunge kama litakubaliana Wizara ya Mambo ya Nje iongezwe kwenye Bodi ya Wakurugenzi pamoja na ile Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni suala la nguvu za Kamati zako za Bunge ambazo tunazihudumia dhidi ya watendaji wa Serikali. Nimekuwa na uzoefu mdogo tangu nimekuwa nikifanya kazi za Kamati miaka hii miwili ya Ubunge, watendaji wa Serikali mara nyingi hawako *serious*. Wanakuja kwenye Kamati tunakaa nao, unaona kabisa hawako *serious*. Kuna watu ni Maprofesa na elimu kubwa lakini wengi unakuta hawa-*own* taarifa ambazo zinazokuja. Tunauliza maswali ya kawaida kabisa *very obvious,* hawawezi kusema mpaka unabaki unashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatoa maelekezo kwa mfano Bunge la Bajeti, tunawaambia Bunge lijalo mje na taarifa fulani, fulani wanaitikia ndio Waheshimiwa. *Session* inayokuja mnakutana hawaleti, yaani kama wametuzoea au wanatuweza hivi. Muda mwingine watendaji wanaambiana kwamba wewe peleka tu taarifa hata zikiwa kubwa, Waheshimiwa Wabunge huwa hawasomi. Waambie tu Mheshimiwa, Mheshimiwa huwa hawasomi. Sasa bahati mbaya wanakosea njia, siku hizi watu wanasoma sana na hata kukesha inapolazimu watu tunakesha, *we read between lines,* hata wakileta vitabu vikubwa tunasoma na tunafuatilia.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Wabunge wenzangu ambao ni Mawaziri na Naibu Mawaziri, sisi ni wenzenu. Tupo kuwasaidieni kuhakikisha kwamba tunasaidia hii nchi na inakwenda mbele, *there is nothing personal*. Mara nyingi utakuta Mawaziri au Naibu Waziri, hawatumii muda mwingi kubanana na watendaji wao. Sijui wanazoeana? Baadaye unakuta Kaibu Mkuu anamwingiza chaka, Waziri anakuja kukaangwa kwa ajili ya mambo ya watendaji wake. Naibu Waziri anakaangwa kwa ajili ya Mkurugenzi fulani aliye chini ya Taasisi zao, kwa nini? Wasiwachekee, sisi tukija kwenye Kamati tunakaza, wakitulaumu sawa, mahusiano yetu ya urafiki yakivunjika sawa, lakini *you need to be serious* kuwasimamia watendaji.

Mheshimiwa Spika, naomba uwatie moyo Wabunge wako kwenye Kamati kwamba waendelee kufanya kazi *seriously*. Mtu anashindwa kujibu halafu baadaye wanaongea pembeni kwamba hili suala ni zito sana, msilijadili sana maana huwezi kujua kwa nini halitatuliwi kwa miezi yote halitatuliwi, kutakuwa kuna kit utu. Wanataka kama kuanza kutishatisha watu, lionekane jambo sijui ni la nani? Halipo. kinachokuja kwenye Kamati tunajadili na tunakaza na watalifanyia kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa leo nashukuru sana, lakini nasisitiza Katibu Mkuu wa Uchukuzi na timu yake wajitafakari. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya *CAG* pamoja na ripoti ya Kamati Tatu ambazo zimeletwa mbele yetu. Nitajielekeza kwenye maeneo manne, nianze na *PIC* kwenye taarifa yao ya uchambuzi wa taarifa hii ya CAG, katika ukurasa wao wa 24 kipengele cha Mbili, Nne na cha Tano kuhusiana na mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo na pamoja na kwamba tunaangalia benki hizi za Serikali hasa *TADB* na *TCD* ni vizuri tulifungamanishe na suala la *interest rate* ambalo tunalipigia kelele kila siku, ukiongea na *Commercial Banks* kwa nini *interest rate* haiwezi kushuka wanasema ni kwa sababu ni *risk* kubwa kwa mikopo ya kwetu, ambayo inaonekana hata kwenye benki zetu kwamba mikopo, kwa mfano ukiangalia kwenye ile taarifa mpaka asilimia 58 ya mikopo inaonekana ni mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna mahali tunakwama hasa kwenye eneo la uhasibu, mimi nadhani kwa ukiangalia *SME* biashara hizi za kati na biashara ndogo nyingi zinapopeleka mahesabu hata kwenye *commercial Bank* kunakuwa na mahesabu ya benki ambayo yanaonyesha yanafanya biashara kubwa na anapata faida kubwa, lakini kuna mahesabu ya pili yanakuwa ni ya *TRA* ya kuonesha kwamba hawatengenezi faida au faida kidogo na haya yote yanakuwa *certified* na hawa watu wanaitwa *CPA* ninajua na huku wapo. nadhani ni suala la kuweka mfumo ambao utafungamanisha ili tuweze kwanza tutoe mikopo ambayo itawasaidia wafanyabiashara na taasisi zinazofanya biashara, lakini tutoe mikopo ambayo italeta tija pia kwenye Serikali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani tunaweza kufanya jambo moja tukapitisha Sheria ambayo inaifungamanisha *NBAA* taasisi za fedha pamoja na wafanyabiashara waliopo. Maana yake ni nini, taasisi inataka kutoa mkopo kwa mfanyabiashara fulani au kwa kampuni fulani ni rahisi tu, inatakiwa kuwe na sehemu ambapo *financial institution* ikienda inaona mahesabu yake ambayo yana uhalisia na yana-*reflect* kodi yanayolipa. Kwa sababu kama yanapata faida kwa nini asilipe kodi, kama halipi ina maana atakuwa na sababu gani asilipe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa tunaenda unakuta mtu anapeleka mahesabu makubwa kwenye taasisi za fedha, inaonekana faida ni kubwa, anapewa fedha ambayo pengine hana hata uwezo nayo ndiyo tunaingia kwenye mikopo hii ambayo ni mikopo isiyolipika au ni mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri tuangalie sheria ya namna ya kufungamanisha, kama kulivyotengenezwa *credit bureau* kuwe kuna sehemu ambapo *financial institution* ikienda ikichukua mahesabu ya biashara fulani inayotaka kukopeshwa anaweza akaona pia *output* ya kodi ambayo inaendana na mahesabu aliyoletewa na ikawa haina mawaa. Hilo ni wazo la kwanza kwa *PIC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kwenye taarifa ya *PIC* ni kwenye uwekezaji wa fedha hizi za umma, mitaji kwenye hasa shughuli hizi za kibiashara. Katika ukurasa wa saba waripoti yao wameeleza vizuri namna kile kipengele cha 22.1 na 22.2 wameeleza ni namna gani fedha za umma zinawekezwa na zinakusanywa vipi na zinategemea zilete faida gani? Ninaomba niende sehemu moja tu ya mfano, Serikali inawekeza fedha

nyingi sana pale Moshi Mjini kwenye Kiwanda cha Karanga *Leather,* nia yake ni nzuri na tunategemea kupata ajira labda 3,000 au zaidi, ukiangalia kwenye mnyororo wa faida, faida ni kubwa zaidi, lakini ukiangalia ule uwekezaji na namna ambavyo tunazi-*manage* ni dhahiri kabisa kwamba matokeo yake mwisho mtakuja kuiona Karanga Leather kwenye vitabu vya CAG tena! Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ni mkubwa mpaka sasa hivi ni zaidi ya Bilioni 156 lakini namna unavyokuwa *managed* ni jinsi mnavyoona sasa kwamba, tunasubiri matamasha tulete *pair* tatu za viatu hapa, tunasubiri warsha tulete viatu na mabegi, wakati *investment* hii inatakiwa itoe *production* kubwa ambayo inaweza ikatuelekeza kwenye *export*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sioni shida kwa sababu ukiangalia *structure* ya Dubai *Port* ambayo ni mali ya *UAE* wako wataalam kutoka nje wabobezi kwenye mambo ya bandari ambao wanafanyakazi na faida inakuja pale, kwa hiyo nafikiri kiwanda kikubwa kama hiki sasa hivi kimeajiri watu 253 tu na kiko miaka tayari imeshafika minne hakijamaliziwa, ninafikiri kuna haja ya kuwatafuta wabobezi wa biashara wa ndani na nje, na wabobezi wa masoko watusaidie kuendesha tuwalipe tupate faida, lakini tukiendelea kuviendesha kwa utaratibu wa teuzi na hizi Bodi ambazo *PIC* nao wameelezea matatizo yake, ni dhahiri kwamba matokeo ya kiwanda kama hiki hayataonekana na baadae itakuwa hasara na tutarudi kwenye vitabu kuonesha kwamba hela hii imepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine naomba niende kwenye taarifa ya *LAAC* na hapa nianze na ile mikopo ya

vikundi, ni dhahiri kabisa tunaipenda ile mikopo inawaidia watu wetu, lakini ukiangalia hii taarifa ya *CAG,* ukiangalia uwezo wa kurejesha wa hiyo mokopo ni dhahiri hizi hela tumezitoa kama ruzuku. Hii iitwe *TASAF part two* kwa sababu hizi hela kuna maeneo mimi nilifanya ziara Jimboni, kuna maeneo vikundi vimekopeshwa 45 kinarudisha kikundi kimoja tu, maana yake ni nini? Kwamba ni hela tumetoa za kwenda ku-*boost* uchumi siyo za kuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Ukiangalia *structure* ya ule Mfuko hasa baada ya kupitisha Sheria kwamba uwe wa mzunguko, ni kwamba fedha hizi za kila mwaka, kwa kila Halmashauri maana yake zikiwa zinarejeshwa na bado tunatenga ule mfuko utakuwa mkubwa, utaweza hata kuwafikia mtu mmoja mmoja. Lakini kwa sababu hazirejeshwi ule Mfuko haukui.

Mheshimiwa Spika, kwenye ule ukurasa wa 11 wamesema mwaka huu kwa mapato ya Halmashauri zote asilimia 10 inaweza ikafika Bilioni 75, hizi ni hela nyingi sana, lakini tunaenda kuitoa halafu haitarejeshwa, mwaka unaofuata tutatenga tena na tena, maana yake ni nini? Badala ya kuwasaidia watu wajikomboe kwenye umaskini au kuwasaidia wananchi kiuchumi, tunaenda kuwasababishia umaskini kwa sababu tunajua ni hela ya kwenda kufanyia shughuli ambayo siyo *serious,* hela hizi hazina riba na huweki *collateral.*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Mbunge aliyesema ni vizuri tuzi-*contract* kwa benki. Mimi nilishawahi kufanya *field* Benki ya Akiba Manzese, kuna hela ya kuwasaidia akina mama walio na uwezo wa chini sana kutoka *ILO* walikuwa *contracted Akiba Commercial Bank* ndiyo wakawapelekea wale watu, mabenki wana

uwezo wa kufuatilia kutathmini biashara ya mtu, kuishauri na wakaweza kutoa ule mkopo na kufuatilia kwa njia ambayo itakuwa haina matatizo kwetu, nasi tutakachofanya ni kuiongezea ile benki mtaji kwenye hizi hela, tunakubaliana kwamba wao watabaki na *percent* kiasi Fulani, siyo kwamba waongeze gharama ili waweze kuwachaji wale wanufaika, lakini kwa Afisa Maendeleo ya Jamii kwenda kukopesha hela, kutathmini biashara na akasema inatoa faida hii biashara na akafuatilia akusanye hiyo hela, tunajidanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tutafute mfumo mbadala, sijajua mfumo ambao TAMISEMI wameuanzisha kama utaleta majibu lakini tukikubaliana na benki zetu tukatangaza tenda, Bilioni 75 kwenye mfuko wa benki yoyote ni hela nyingi, tukawaelekeza, utaratibu ule wa kukopesha tukaufanya sisi wao wakaenda kumalizia kwa ku-*verify* na kutoa ushauri fedha hizi zinaweza zikaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hizi fedha bado kuna matatizo, uwiano ni asilimia Nne kwa vijana, Asilimia Nne akina mama na asilimia Mbili kwa walemavu. Sasa Serikali inataka kulazimisha kwamba hata mahali ambapo walemavu hawataki mkopo tulazimisha hizo hiyo asilimia Mbili wapewe, sasa hawataki au hawapo lakini inakuja ni kweli kwamba kwa nini mmekopesha akina mama zaidi? walemavu hawajakopeshwa? wapo hawataki kufanya biashara, maana yake sasa wanalazimishwa Afisa Maendeleo ya Jamii ili wasipate hiyo kero wanawalazimishia watu mkopo, wewe chukua tu! Sitaweza kurudisha, wewe chukua tu utarudisha utaangaliaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huu uwiano uwepo lakini maeneo ambayo kwa mfano, maeneo mengi nimejifunza vijana hawawezi kukaa pamoja kwa muda mrefu kwa sababu bado ni watu wanaotafuta wanaenda sana, kwa hiyo ni wachache sana wanakuwa kwenye makundi lakini akina mama ni watu walio-*settle* wapo kwenye lile eneo, kwa hiyo tusilazimishe kwamba huu uwuiano ufuatwe kama inaonekana wana uwezo zaidi au vijana wana uwezo zaidi hilo eneo wapewe fedha zirudi lakini kubwa zaidi ziweze kusimamiwa vizuri watu wapate. Isitokee kwamba kuna kundi linahitaji likakosa na *share* yake imetoka lakini kama halipo na mwaka unaisha wa fedha wapewe wale kundi ambalo liko tayari liweze kufanyia kazi hizo fedha *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende eneo la mwisho ni eneo ambalo kwenye taarifa ya *LAAC* ukurasa ule wa Saba kipengele 2.2.3 udhaifu wa manunuzi na usimamizi wa miradi. Watu wengi wameliongelea, ni kweli kabisa kuna udhaifu mkubwa kwenye manunuzi ambayo nafikiri kila mtu atasema ifumuliwe lakini ikifumuliwa sijui itawekwa kwa namna gani ili manunuzi yaweze kuleta tija, kwa sababu kalamu ya Shilingi 1,000 ambayo wewe unaweza kununua, ikinunua Serikali itanunua 2,000 mpaka 3,000 wataalam watashauri namna ya kurekebisha mfumo wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye *force account*. Hili ni janga *force account* by design ilitakiwa iende sehemu ambayo tunao wataalam wanaojitosheleza. Halmashauri iwe na Injinia wa ujenzi anayejua, iwe na Mthamini anayejua, iwe na watu wote wa *technica*l wanaojua ili ile hela waisimamie kama ilivyo kwenye kampuni.

Mheshimiwa Spika hela, zinapelekwa kwenye halmashauri zinaambiwa zifanye kazi kwa *force account,* hiyo Halmashauri haina hata Injinia tunachotegemea ni nini? Tunakwenda kutengeneza matatizo makubwa, iko miradi ambayo baada ya muda haitafaa. Nitolee mfano kwenye Halmashauri moja juzi wamepelekana TAKUKURU, mradi unavyoonekana ukiangalia kwa sababu hela tunapeleka sehemu moja, tunapeleka hela za kufanana maeneo yote, lakini ukija kuangalia hela sehemu moja imefanya vizuri tena Halmashauri zilizoko karibu, sehemu nyingine hakuna kitu kabisa, lakini kuna maeneo mengine inaenda hela kwa ajili ya *force account* lakini unakuta hata eneo la *labor* wamem-*contract* mtu, kwa hiyo contractor anapewa tena *labor* kampuni kabisa inapewa kazi ya *labor*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu wa *force account* ni lazima tukubaliane aidha hiyo sijui kuajiri tunaweza au hatuwezi ziende sehemu ambazo wataalam wapo wa kutosha ndiyo fedha zipelekwe kwa utaratibu wa *force account,* vinginevyo tuwape Wakandarasi kwa sababu bahati nzuri tunapata mpaka *retention* kule na baada ya muda kama huo mradi haujakaa sawa tunauwezo wa kuwaambia warudie, lakini kwenye *force account* ikishakuwa imeharibika inaharibika na ni ya kwako. Ninashauri *force account*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka atafuatiwa na Mheshimiwa John Danielson

Pallangyo, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja ya Kamati zetu hizi tatu za *PIC, LAAC* na *PAC*. Kwanza ninakushukuru sana kwa vile umerudisha heshima ya Bunge hili, umekumbusha Watanzania wote kwamba Bunge hili lina meno na kwamba kweli kipindi hiki hatuna mchezo, kwa hilo unamuunga Mama Samia Suluhu Hassan mkono, kwa vile nakumbuka tulivyokuwa Tanga kwenye semina ya Polisi wakifundishwa mambo ya maadili ambapo *CAG* alikuwepo alimsifia sana *CAG* kwa kazi yake kubwa anayoifanya, alikemea sana Polisi wanavyofanya ubadhilifu wa fedha za umma na akakagiza kwamba kwa kweli taarifa za *CAG* zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutupa muda wote mrefu huu wa kuchanganua ripoti ya *CAG* tunakushukuru sana, maana tumeweza kuongea na tutaweza kuongea mengi. Ninakuomba kwa muhtasari kidogo kabla sijachangia nieleze Bunge lako Tukufu wajue kwamba kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2022 *CAG* alifanya kaguzi kwa jumla taasisi 331 za Serikali Kuu. Pia kwa upande wa mashirika ya umma alifanya ukaguzi mashirika 200 na pia alifanya ukaguzi wa ufanisi kwa taasisi12, jumla alifanya kaguzi 543. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewaeleza hilo kwa kuzingatia kwamba Kamati ya *PAC* kwa nafasi ambazo tunapewa kisheria, tumeweza kupitia chini ya asilimia 10 ya haya mashirika yote, kwa hiyo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa nini ripoti ya *CAG* imetawanywa

kwa kila mtu? Ni kwamba tupitie, tuangalie, tuhoji, ndiyo kazi ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isionekane ni hii *PAC, LAAC* au *PIC* yenye jukumu lile, maana kama ni kupitia kila mahali basi ingebidi iwe kazi ya kila siku kama ambavyo nchi nyingine wanafanya. Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa *SADCOPAC*, PAC's zilizoko Kusini mwa Afrika, kuna nchi ambazo wao *throughout* wanafanyakazi ya kupitia kaguzi za *PACs* zao na kuhakisha kwamba wanamaliza taarifa za *CAG* na kuhakikisha kwamba wanazimaliza ndipo wazipeleke Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa taratibu zetu mashirika ni mengi na najua kwamba kwa hilo kwetu itakuwa shida kidogo, labda hapo baadae Bunge lako Tukufu linaeza kutoa muda zaidi tukaweza kupitia mashirika mengi yenye utata.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hiyo *background* niseme tu kwa kifupi kwamba, kwenye ripoti yetu tuliyoitoa kwa ukaguzi uliofanywa na *CAG* kwa mwaka wa 2019/2020 ripoti yetu tuliyoileta Bungeni hapa mapendekezo yote tuliyoyatoa ambayo Bunge lako Tukufu liliyachukulia kama maazimio mengi hayakufanyiwa kazi, na mengi yamejirudia katika taarifa yetu hii, ndiyo maana unaona kigezo chetu kikubwa tunachoweka ni kupitia yale mashirika ambayo tungeweza kusema au zile taasisi tunazoweza kusema wanashingo ngumu. Bunge lako Tukufu linatoa maagizo hawayafuati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia kwa mfano mwaka jana ripoti yetu ya *TRA* ilikuwepo, *TCB, TIB* yapo, *TANROADS* ipo, *NFRA* ipo, hapa tunayarudia tena.

Mengine hatukuweza kuyapitia kwa sababu gani? Kama ni *occurrence* imefanyika mara moja ile ina utaratibu wake mwingine lakini zile ambazo zimejirudia tunaona hao watu siyo wasikivu na hawako tayari kufuata maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia *TRA* kwa mwaka huu Juni 2021 wameshindwa kushughulikia madeni ya trilioni 7.5, mwaka jana walishindwa kushughulikia madeni ya Trilioni Tatu. Tuliwapa maagizo kwamba washughulikie madeni hayo, kama wenzangu waliopita walivyosema waliona kwani tusiposhughulikia tutafanywa nini? Hili Bunge si litasema tu halafu basi yanaisha? Ndiyo maana unakuta asilimia 95 katika mwaka mmoja ya kodi zile madai hayakufanyiwa kazi. Sasa swali tunalojiuliza hivi Serikali yetu itapata wapi pesa za maendeleo kama tunadai fedha Trilioni Saba kwa mwaka huu tunaozungumza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mapungufu katika mfumo wa *i-tax (Income Tax Management System*), Bilioni 11 hazikuweza kuwa *captured.* Na unaambiwa mfumo una matatizo na hili tulishawambia hata ripoti iliyopita kwamba, huu mfumo unatengenezwa na binadamu kaushughulikieni msipoteze kodi zetu. Wamekuwa na shingo ngumu leo tena tunayaona haya haya. Kwa hiyo ninachosema ni kwamba umeturudishia heshima yetu na nimesikiliza Wabunge wote wakiongea na kuonesha jinsi ambavyo kipindi hiki hakuna msalia mtume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANROADS*, kwenye Bohari, dawa zinaharibika, wazee hawapati dawa wakienda *dispensaries,* wanaambiwa hakuna. Tumeona yaliyofanyika kwenye *fake VISA* huko. Tumeona ujenzi wa vihenge ambaye anapewa Mkandarasi wa nje kana

kwamba sisi hatuwezi kujenga vihenge na ameondoka na hakuna anachofanyiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo ukianagalia kumekuwa ni kwamba kumekuwa na dharau kubwa sana kwa upande wa wale wenzetu ambao walipewa jukumu la kugawa au kutengeneza miradi mbalimbali kwa manufaa ya nchi hii. Kwa hiyo, tuseme hivi kama wakati ule aliposema Hayati Baba wa Taifa kwamba sababu tunayo, Bunge hili tuna sababu ya kuwawajibisha hao watu nia tunayo na uwezo tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukuombe kama itakupendeza italetwa labda kwenye mapendekezo, tuna Kamati yetu ya Maadili, yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge ambayo wanayasema, nafikiri itakuwa wakati muafaka. Waitwe hawa hawa watu kwenye maadili wajue Bunge lina meno ili Bunge lako tukufu liweze kupewa ripoti kamili ya jinsi ambavyo ubadhilifu huu mkubwa wa fedha za umma umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwamba mimi nipo kwenye Kamati ile na Makamu wangu Mheshimiwa Hasunga pia yupo kamati ile. Kwa hiyo, tutatoa yote, maana tumepitia ripoti yote ya CAG ni kwamba hatukuweza kuifanyia kazi yote, lakini wote tumeisoma na tunajua madhaifu yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe, mengi yameshazungumzwa na kazi yetu kubwa ni kwamba tutajua tulete mapendekezo gani katika Bunge lako Tukufu ili yachukuliwa hatua. Nisisitize kwamba, Mama Samia Suluhu Hassan, ambaye wakati wa Hayati Rais Magufuli, alikuwa halali anaamshwa usiku wafanye kazi; leo anakuwa Rais anafanya kazi, watu wachache

wanchukua hela wanatia mfukoni halafu wanajua Bunge litatufanya nini. Uzuri Rais mwana mama, Spika mwana mama, Wenyeviti wa Kamati ya *PAC* na *LAAC* wana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatukosei, kama tumeweza kuwafundisha wanaume kuvaa suruali, tumevalisha nepi, tumewanyonyesha, tukawalea, leo tunashindwa kuwawajibisha. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joan Johnson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam muda ukiruhusu tutaendelea na Mheshimiwa George Nataly Malima.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii ambayo ipo mezani. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya *PIC*. Kwa hiyo nitajikita zaidi kwenye Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kukupongeza wewe kwa kazi nzuri ambayo unafanya, unaongeza Bunge hili kwa umahiri mkubwa, hadi *IPU* imekuona; hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisiishie hapo, nimshukuru Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuandika historia kwenye Jimbo langu. Ametuletea fedha nyingi za maendeleo. Hapa si mahali pa kuzizungumzia sana, lakini itoshe kusema nashukuru mno, ameandika historia kwenye Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nichukue nafasi hii, kupongeza Wenyeviti wa Kamati hzi tatu *PAC, PIC* na

*LAAC*, pamoja na wajumbe na wote kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na hatimaye hizi taarifa zikaja mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama baba ambavyo anahangaika kutafuta *resources* huku na kule, mikopo ya bei nafuu, misaada, yote hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anatuletea maendelo wananchi wake. Fedha hizi Serikali imeamua kwamba, pamoja na mambo mengine tutumie *resources* zote kuziweka kama mitaji kwenye kampuni na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilipewa jukumu la kuchambua na kubaini ufanisi wa uwekezaji huu ambao Serikali inafanya, ambao ni uwekezaji mkubwa sana. Hadi kufikia tarehe 30 Mwezi wa Sita mwaka 2021 Kamati ilibaini kwamba Serikali ilikuwa imewekeza kwenye taasisi na kampuni zake shilingi trilioni 67.95. Hizi ni fedha nyingi sana. Pia, katika uchambuzi, tumebaini kwamba, *TR* alieka maotea; ali-*project* kufanya makusanyo ya *returns* za uwekezaji wa takribani bilioni 930.3, lakini halisi iliyokusanywa ni bilioni 637.66.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuchambua yale makusanyo ambayo yanatakiwa yakusanywe, kwa maana ya gawio *percent* 15 ya mapato ghafi ya Serikali na kampuni hizi, urejeshaji wa mikopo, urejeshaji wa *TTMS* na makusanyo mengine; tumeona kwamba kulikuwa na mapungufu. Kwa mfano, gawio, maoteo ya *TR* yalikuwa ni bilioni 408 lakini halisi ilikuwa ni bilioni 308.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo ufanisi hapa ilikuwa ni *percent* 75.61. *Percent* 15 ya makusanyo ya kisheria, maoteo ilikuwa bilioni 365.4 makusanyo halisi ilikuwa bilioni 202.2. Kwa hiyo ufanisi hapa wa mtaji ulikuwa *percent* 51.

Mheshimiwa Spika, tuliendelea kuchambua na kuangalia kwamba ni sababu gani zimepelekea haya mashirika na taasisi za Serikali zikashindwa kufikia malengo. Tukachambua changamoto, tukatazama mashirika yale ambayo yalikuwa yamelengwa, tukaona kulikuwa na matatizo kidogo. Moja, kulikuwa na shida kubwa, taasisi zile zinakuwa hazina Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu, lakini pia, taasisi zile zilikuwa hazina vibali vya kuajiri wataalum, kwa hiyo vibali vinachelewa sana, matunda yake ufanisi unakwenda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, pia, tuligundua kwamba kuna mwingiliano wa majukumu kati ya taasisi na taasisi. Kwa mfano *TANROADS* na *TIA*; ukijaribu kuangalia majukumu yake utakuta yanafanana; lakini *TIA* wamepewa umiliki, hawaangaliii ujenzi, wao wamepewa jukumu la kuangalia matengenezo ya kazi ambayo imefanywa na mtu mwingine; kwa hiyo, *quality* ya kazi hawaijui. Lakini pia kulikuwa na tatizo la kuajiri wataalamu. Tumekuta bodi nyingi sana hazina Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, au watumishi wana kaimu. Hilo ni tataizo kubwa sana kwa sababu hatimaye maamuzi hayafanyiki *on time* (kwa wakati).

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kulikuwepo na tatizo la mitaji. Utakuta Serikali inanzisha taasisi na kuahidi itatoa mtaji kamili, mfano mzuri ni Benki ya *TADB* ambayo ilikuwa inahitaji mtaji wa Shilingi bilioni 760. Hadi mwaka jana ilikuwa imepata bilioni 208, zikaongezeka bilioni 60. Kwa kweli tunaona kwamba uchelewaji wa mitaji au kutokuwa na mitaji kuna athiri *performance* za hizi taasisi za Serikali ambazo zimeanzishwa kwa lengo zuri tu la kuhakikisha kwamba fedha zinazungushwa na faida ipatikane, iweze kwenda kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna taasisi ambazo zilianzishwa lakini zina madeni chechefu; kwa mfano *TIB* na *TCB*. Hizo ni benki ambazo vitabu vyake vinaonyesha kwamba kuna madeni makubwa ambayo hatimaye hatuamini kama yatalipika. Wazo letu kama Kamati ni kuwa utaratibu ufanyike ili hao madeni yaangaliwe namna ya kufutwa bila kuathiri ukusanywaji wa yale madeni ambayo yanalipika.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo mafupi, Kamati ilikaa ikatoa maoni yake, ikatoa mapendekezo yake na maazimio. Kwa kulinda wakati, niseme kwamba, mimi kama Mwanakamati wa hii Kamati ya *PIC*, naungana na Mwenyekiti na Wajumbe wote kuunga mkono mapendekezo, maoni na maazimio ambayo yapo kwenye taarifa.

Mheshimiwa Spika, nisiishie hapo, pia nimesoma hizi taarifa za Kamati zingine; zinaeleweka, nako niseme kwamba pia naunga mkono yale maoni, mapendekezo na maazimio ambayo yamewekwa kwenye zile taarifa

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, niseme nashukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa George Nataly Malima, muda ukiruhusu atachangia pia Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia taarifa ya *CAG*. Ni kwamba Wabunge wengi

wamezungumza hapa kwa hisia kali, na wanaonesha wanavyoguswa namna upotevu wa fedha za Serikali. Hata hivyo kitu kinachonishangaza ni kwamba; mimi nilikuwa naangalia pamoja na ugeni katika Bunge hili kwa miaka miwili. Taarifa hizi zinazosomwa hapa za *CAG* ni hadi tarehe 28 mwezi wa pili mwaka huu. Sasa, kutokea mwezi wa pili mwaka huu tunakuja kusoma taarifa hizi kuja kuanza kuzichambua, ni mwezi wa kumi na moja, tofauti yake ikiwa takribani miezi kumi au tisa ipo pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa kunakuwa na ombwe kubwa sana hapa katikati; mambo mengi yanakuwa yamekwishakuharibika au yanakuja kurekebishwa wakati taarifa hii inaonekana kama inakuwa imepitwa na wakati. Kwa sababu kuna jambo linakuja kuzungumzwa hapa sasa hivi, limeshafanyiwa kazi. Sasa tunauliza, kwa nini hili jambo tusianze tu baada ya taarifa ya *CAG* kuletwa na kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais ikapokelewa. Pale pale, Kamati yako ya *PIC* ianze kazi hapo hapo, halafu na Bunge hili la Mwezi wa Tatu, tuanze kujadili kwa siku nyingi siyo hizi siku tisa; twende kwa siku 30 ili tuweze kuwaadabisha hawa watu.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopotea ni nyingi sana. Leo mimi nimekuja na vitabu hapa, yote nimeyasoma, nilikuwa naangalia. Hiki ni kitabu tu kwa ajili ya Sengerema peke yake, Jimbo langu, ninapotoka mimi. Hii ni kwa ajili ya Serikali za Mitaa, taarifa hii ni kwa ajili ya mashirika ya umma. Sasa ukichukua hizi taarifa na hii nyingine niliyonayo hapa, yakikaguliwa haya yote, hata yakisomwa haya, bado hatuwezi, sisi Wabunge, kwa nafasi yetu finyu na ratiba zetu za Bunge hatuwezi kwenda sawa kuzichokoa zote hizi tukaziweka zote hapa kwako. Kamati yako hii ya *PIC* pamoja na kazi nyingi ulizokuwa umeipa. Wanazunguka sana na hao

wanaokwenda kuwaita kwenda kwenye hao mashirika ya umma au taasisi za Serikali wanaonesha wana kiburi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hili Bunge lako tunataka kujiuliza, je, tulichokosea hapa ni wapi? Ni mfumo wetu wa Bunge? Tuangalie Mabunge ya wenzetu kule Jumuiya ya Madola yanashiriki vipi katika shughuli hizi zinazoletwa na taarifa ya CAG kuzifanyia kazi. Tukijifunza kwa wenzetu tukaona wanadhiti namna gani hili jambo, halitajirudia. Hapa kuna taarifa za tangu mwaka 2011. Kwa hiyo, wameshaona taarifa hizi zinazoletwa hapa labda zinaletwa kama taarifa za mapato ya harusi au zinaletwa hapa za michango ya kanisani, kwamba labda hii michango haitakaguliwa au michango ya msikitini.

Mheshimiwa Spika, lakini hizi ni fedha za kodi za wananchi, tukiwemo sisi Wabunge, tunakatwa kodi, na wewe unakatwa kodi kwa sababu na wewe ni Mbunge. Sasa, ifikie mahali tuje na maamuzi makali, kwa sababu sasa hivi naangalia hiki kitabu kimoja, kinazungumzia taarifa zilivyo pamoja na vielelezo. Sasa najiuliza tuje na sheria, tukuombe hapa umwambie Mwanasheria Mkuu wa Serikali aje na sheria ya kuiongezea meno kumuongezea meno CAG. Kwa sababu akimaliza kukagua anawaomba wale watu walete vithibitisho; taarifa zinazokosa vithibitisho ndizo zinaletwa hapa kama zimeiva vilivyo; kwamba hizi ni sahihi; kwa nini asiwapeleke Mahakamani moja kwa moja, huyo huyo CAG, kwa sababu yeye ndiye mwenye ushahidi na watoa ushahidi anao yeye? Hao watu baada ya hapo wanapelekwa TAKUKURU, hili jambo linakwenda kufia kule na hawa watu unawaona wanaendelea kupata vitambi, wanapiga miluzi barabarani na mwaka kesho, tunakuja kujadili taarifa nyingine tena ya CAG.

Mheshimiwa Spika, mimi napata kigugumizi sana. Mama yetu Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu kama sasa hivi tunavyomuona anavyosafiri, leo yuko China, sijui kesho kutwa ratiba yake inasemaje hayo ni mambo ya kiitifaki. Lakini anapokwenda huko anakwenda kutafuta hizi fedha, na bahati mbaya fedha hizi zingine zinazoletwa ni madeni. Sasa zikija hizi fedha hapa zinakuja kuibiwa, na tunakuja tena na taarifa nyingine mwezi wa pili tena, mwaka kesho tutapokea vitabu vingine kama hivi; hivi havijafanyiwa kazi anachukuwa vitabu vingine. Sasa mama anahitaji usaidizi wa hatua akali kabisa, zibadilishwe hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu sehemu ya Mawaziri na Manaibu wanatoka kwetu sisi kama Wabunge, na sisi ni wenzetu wale, lakini kule wanakokwenda kufanya nao kazi ni watendaji na wataalamu wa Serikali. La sivyo, taarifa zitakuwa zinakuja tunaondoka na Mawaziri, kesho tena tunaweka Wabunge wengine, tuanondoka nao. Sasa inaonekana tunajipiga sisi kwa sisi. Sasa jamani Wabunge ninachotaka kuwaambieni humu ndani, tukiwa pamoja lazima tuombe sheria kali kwa hawa watu; na anayetajwa na taarifa ya *CAG* kwanza hawa watu wangekuwa wako nje na wanaripoti polisi kila siku, mpaka kazi zao ziishe na mishahara ikatwe. Tuunde sheria kama hiyo, watu wataacha kucheza na hizi fedha *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichonisikitisha zaidi kumbe mpaka sasa na Ubalozini fedha zinaibiwa, tena Ubalozi wa heshimia kama Marekani. Naangalia hapa mimi fedha za *visa* tu ambazo zimeibiwa ni takriban milioni 670. Kule kule Marekani tumenunua jengo dola milioni 25 na lile jengo lilikuwa na sehemu za kukodisha lina *floor* sita na katika lile

jengo *floor* mbili zinafanya kazi. *Floor* nne hazifanyi kazi na wateja waliokuwa katika zile *floor* nyingine nne wamehama kwa sababu ya kushindwa kukarabatiwa lile jengo. Tumepata hasara shilingi bilioni 27 sawa sawa na vituo vya afya zaidi ya 70.

Mheshimiwa Spika, sasa huyu mama sijui tutamsaidiaje? Sisi Wabunge ndio tunatakiwa tumsaidie. Kama na mabalozi na wenyewe tena, ndio watu wa heshima, anaondoka anakwenda kule, balozi tena anakuwa naye ni sehemu ya upigaji, hii nchi sasa ni hatari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naangalia hapa Ubalozi, sijui wa Uholanzi, Addis -Ababa, Kampala, Berlin; yaani hakuna balozi hapa ambaye yuko salama. Sasa kama tuna mabalozi 43 tunaibiwa fedha kiasi hiki, hata fedha za *visa*, wageni ambapo wanapita, yaani watu hawaogopi. Kwa sababu mgeni anayepita, atapitia mipakani uwanja wa ndege, taarifa ziko kote, halafu na hizo na zenyewe zinaibiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la Msajili wa Hazina. Hii *KADCO* ni sehemu tu ya kampuni ambazo ninyi mnaziona ambazo Msajili wa Hazina anazo ambapo kule Msajili wa Hazina ninyi mnaona hiyo ni sehemu ndogo tu, kuna *TIPER* kule. Pale *TIPER* kuna tatizo kubwa. Tuna wanahisa wenzetu pale. Msajili wa Hazina ni sehemu ya mtu ambaye anatakiwa kuitwa aje aoneshe mashirika yote ambayo sisi tuna hisa, tunayoyamiliki na watu wengine tofauti, yaje yakaguliwe na Kamati hii ya *PIC*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo, bado kuna *PUMA*. Kule *PUMA,* kumenza kuuzwa kwa sababu kuliuzwa Sheli, Sheli wakauza kwa *BP* na *BP* wakaenda

kumuuzia *PUMA*. Sasa hivi *PUMA* sijui wanaenda kumuuzia nani tena! Kwa hiyo, kote kule Msajili wa Hazina na kwenyewe kule tuna mali zetu, siyo sehemu hiyo tu. Kwa hiyo, yaletwe mashirika yote halafu Msajili wa Hazina atakuwa anasema hapa hakuna fedha, hapa fedha ziko hivi.

Mheshimiwa Spika, pia tuna uwanja nyuma ya Chuo cha Mwalimu Nyerere pale Kigamboni na lile eneo linalozunguka katika hayo maeneo. Huu uwanja uko wazi, zaidi ya ekari 60 au 100 ziko pale, lakini *ICD* ziko Dar es Salaam sasa hivi kila kona, watu wanavunja nyumba wanaanza kuhifadhi makontena. Barabara ya kupeleka haya makontena kule kwenye huo uwanja ambao uko bandarini pale pale ng'ambo ya bandari, tungeweza kuweka makontena, haya makasha yote. Kasha moja linaanzia Dola 250 na kuendelea. Tungehifadhi makasha pale, hizi tozo zisingekuwepo. Inaonekana usaidizi kwa Mheshimiwa Rais bado hajapata watu sahihi wa kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na mambo mengine, hivi viwanja ambavyo majengo yanavunjwa; anaonesha hapa *CAG*. Viwanja vinavunjwa na vile viwanja vinakaa wazi. Si tungekuwa tunaweka haya makasha matupu na yenyewe yakawa ni sehemu tu ya *ICD* kule, mpaka siku watakapokuja kujenga hayo majengo, tuanze kupata hizo fedha za kontena. Kwa hiyo, mahali pa kupata fedha papo na *CAG* hapa anatuonesha.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha, *CAG* hapa amenishangaza mimi anasema, zaidi ya mashirika 60 ya Serikali hayana Bodi za Wakurugenzi. Sasa ni maajabu.

Bado anasema *CAG* ameshindwa kwenda kukagua… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia sentensi, dakika moja.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, *CAG* ameshindwa kwenda kukagua hizi Bodi za Wakurugenzi kwa sababu sheria inamruhusu Katibu Mkuu wa Wizara husika kusimamia tu kwa muda wa miezi 12. Baada ya miezi 12, *CAG* hawezi kwenda pale wala Katibu Mkuu hawezi tena kwenda katika lile shirika. Kwa hiyo, wale Wakurugenzi *(directors)* waliobakia kule walewe wanaendesha yale mashirika kama mali zao binafsi. Imenitia hofu sana.

Mheshimiwa Spika, pia pale pale kuna bodi ambazo ni za muhimu sana katika nchi hii. Kama Bodi ya Pamba; unakuta Bodi ya Pamba na ya Mbolea; leo tunatoa ruzuku ya mbolea, hakuna Bodi ya Wakurugenzi kule.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, muda ukiruhusu atachangia pia Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia katika ripoti hizi tatu za Kamati za *LAAC, PIC* na *PAC*. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pia

nikupongeze wewe binafsi kwa kazi nzuri ambayo unaendelea kutusimamia ndani ya Bunge hili. Tatu, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hizi tatu pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hizi tatu kwa ajili ya kazi njema ya kuandaa ripoti ambayo leo tunapata fursa ya kuichangia.

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza hotuba nyingi hapa ndani, malalamiko makubwa sana yapo kwenye utendaji hafifu wa mashirika yetu ya Umma. Malalamiko haya yanakuja kwa sababu mashirika haya yanatumia mitaji ya Umma, yaani fedha za walipa kodi, lakini faida ambayo ilikuwa imetarajiwa kutoka kwenye mashirika haya, haipo. Kwa hiyo, ndiyo maana Wajumbe au Wabunge wanalalamika sana.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi ambazo zinasababisha mashirika haya yasifanye vizuri. Wabunge wengi wameeleza, lakini nami nitaeleza. Moja, ni mashirika haya mengi kuendeshwa bila Bodi za Wakurugenzi kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya bodi yanajulikana. Bodi ndiyo chombo pekee kinachosimamia kutoa maamuzi, usimamiaji wa utekelezaji wa majukumu yote ya taasisi, lakini unakuta mashirika mengi kwa kipindi kirefu yanaendeshwa bila bodi.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe mifano michache tu. Katika ripoti ya CAG ukurasa wa 62 ameorodhesha kwamba mwaka 2020/2021 kulikuwa na orodha ya mashirika 31 ambayo yalikuwa yameendeshwa bila bodi kwa kipindi kirefu sana. Mojawapo ni Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere; kimekaa bila bodi kuanza Julai, 2015

mpaka Februari, 2022. Muda huu ni wa miezi 80 ambao ni sawa na miaka sita, taasisi kama hii inakaa bila bodi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda Tanzania, na lenyewe limekaa bila bodi kuanzia Oktoba, 2015 mpaka Februari, 2022, miezi 77 ambayo ni sawa pia na miaka sita na miezi kadhaa. Lingine ni Makumbusho ya Taifa, kuanzia Julai, 2015 mpaka Februari, 2022 sawa na miezi 38, nalo pia kwa miaka mitatu limekuwa halina bodi.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile uendeshaji huo wa mashirika yetu hauwezi kutarajia kupata tija kwa sababu menejimenti inajiendesha bila kuwa na mtu wa kumwangalia, matokeo yake ukiangalia mashirika yetu yote Kamati ya *PAC* ambayo tunashughulikia mashirika na tumepitia mashirika yote ama yana mzigo wa madeni, ama yanaendeshwa kwa hasara lakini ni kwa sababu hakuna chombo madhubuti, hakuna bodi ambayo inaweza ikasimamia utekelezaji wa majukumu yao na mwisho wa siku tuweze kushuhudia tija ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye ripoti ya *CAG* ukurasa wa 66 aya ya 47 na 48 ya Mwongozo wa Uhasibu *(NBAA)* ya mwaka 2021 zinaeleza umuhimu wa bodi, kwamba bodi lazima iidhinishe hesabu za taasisi yake. Kabla ya *CAG* kukagua, lazima bodi iidhinishe ndipo ikague; lakini *CAG* anasema, alishindwa kutoa maoni kwa mashirika Matano. Hakutoa maoni yake *(opinions)* kwa sababu hesabu zile zilikuwa hazijaidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunapoongea, hatuna uhakika; siyo Serikali na Umma kwa ujumla kwamba *status* ya mashirika haya ikoje? Maana jicho la

Serikali au jicho la Umma ni *CAG*. Kwa hiyo, tunasubiri *CAG* akishakagua atoe maoni kuhusu shirika husika, lakini mpaka sasa hivi mashirika hayo matano ambayo *CAG* alishindwa kutoa maoni yake ni kwa sababu hayakuwa na bodi na sheria inataka hesabu zake ziidhinishwe na bodi, halafu ndipo afanye ukaguzi na atoe maoni yake.

Mheshimiwa Spika, mashirika hayo nitayataja machache. Mojawapo ni Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda Tanzania, lingine ni Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere, na lingine ni Shirika la Utafiti wa Uvuvi. Haya mashirika *CAG* hajatoa maoni mpaka leo na hatujui yanaendeleaje mpaka sasa. Hilo ni eneo ambalo pia linaleta shida kwamba bila kuwa na bodi, kuna mambo mengi yanaweza kukwama kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia kuna *issue* ambayo pia *CAG* amei-*raise* kwenye ripoti yake ukurasa wa 75 anasema; mashirika manne hayakukata michango ya kisheria ya kupeleka kwenye Mifuko ya Pensheni na Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi. Sasa hayo yote ni kwa sababu ya udhaifu wa usimamizi. Haiwezekani mashirika yakakata makato ya kisheria halafu yasipelekwe kunakotakiwa. Hasara yake ni kukosekana kwa mafao ya wafanyakazi wanaostaafu. Watapataje mafao kama haya yamekatwa, lakini hayajapelekwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunaona wazee wengi wanakufa mapema wakishastaafu, kwa sababu wanamangamanga, wanakwenda kufuatilia fedha hazipo. Kumbe taasisi hiyo waliyokuwa wanafanya kazi ilikuwa haipelekei ile michango. Kwa sababu menejimenti ilikuwa haipeleki, hakuna mtu wa kuangalia juu kuona kwamba wanapeleka au hawapeleki. Kwa hiyo, jambo hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine au hasara nyingine ni kwamba kunakosekana na fidia kwa wafanyakazi inapohitajika. Mfanyakazi anaweza kuwa anahitaji fidia, lakini kwa sababu fedha hii haikuwepo kwenye ule mfuko, haitakuwepo, matokeo yake anapigwa danadana. Pia kushindwa kutuma hizo fedha kwenye taasisi hizi kuna hasara kubwa sana, kuna *attract invoice penalty*. Shirika linapigwa *penalty* kwa sababu halikupeleka michango kwa wakati au halikupeleka kabisa. Hii *penalty* inasababisha hasara na ndiyo maana tunaona mashirika mengi yanaendeshwa kwa hasara kwa sababu hizo; fedha nyingi zinalipwa kwa sababu ya *penalty* au adhabu, wakichelewa kupeleka kwenye mifuko ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la kuwa na bodi tungeamua kabisa kusema kwamba ni jambo la kufa na kupona ili taasisi hizi tunazowekeza fedha nyingi za Serikali ziweze kuleta tija iliyokusudiwa ni lazima mashirika yote yaendeshwe chini ya bodi zake za Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kipengele cha matumizi mabaya ya fedha za Serikali; mashirika yote yameonekana yanashindwa kudhibiti matumizi yake na ndiyo maana hayafanyi vizuri, na mengi hayawezi hata kutoa gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Nichukue mfano mmoja tu wa taasisi moja eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la Hifadhi ya Ngorongoro linamiliki ndege aina *Cessna* yenye namba ya usajili *5H-MPZ*. Ndege hii ni ya zamani sana. Mpaka mwaka 2021 ilikuwa na umri wa miaka 47. Taasisi hii ilikuwa inatumia ndege hii kwa ajili ya doria, lakini CAG

anasema katika ukurasa wa 59 Mamlaka hiyo ya Ngorongoro ilifanya matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 278.42, lakini *plan* yao ilikuwa ikishakamilika ifanye safari za saa 900, lakini cha kusikitisha sana ndege hii imefanya safari saa 18 tu.

Mheshimiwa Spika, sasa ukijiuliza, Shilingi milioni 278 zimetumika kukarabati ndege hii, lakini makusudio au matarajio waliyokuwa wametarajia kufanya safari au kuzunguka kuangalia doria kwa saa 900 inaishia kufanya doria kwa saa 18. Hasara hii ni kweli inafanyika na watu ambao wameenda shule? Je, hao watu tuliowaweka humo kufanya kazi hizo za kusimamia mamlaka yetu, wanao uwezo wa kufanya kazi kama hiyo? Ni kweli hawaoni kwamba hili lilikuwa ni kosa kubwa sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana hatua kali zichukuliwe kwa watu kama hao, kwa sababu hatuwezi kuendelea, hatuwezi kupata mafao, hatuwezi kupata tija kwenye mashirika kama haya kama tuna watu ambao wanaendelea kucheza na fedha za walipa kodi katika mazingira kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, naomba kuzungumzia changamoto ya kupata vibali vya ajira na mfumo wa ununuzi kwa mashirika ya Umma na hasa yale yanayofanya biashara. Mashirika mengi yanapata mitaji ya Serikali ili kufanya biashara na kuleta tija na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, kwa mazingira ya biashara ya leo, huwezi kushindana.

Mheshimiwa Spika, nashauri, tufanye biashara mashirika haya ya Umma, lakini tutumie *private thinking*. Maana yake ni kwamba, lazima tubadilike. Wenzetu wa

*private* wana-*enjoy flexibility* ya maamuzi. Mfano, akipata bidhaa fulani kwenye soko kwamba ina-*hit* katika soko, wao wanafanya maamuzi *overnight*. Wanahitaji mtaalamu wa kutengeneza hiyo bidhaa, kesho wameshampata. Kesho kutwa wanaanza uzalishaji. Wanahitaji *raw materials;* kesho wameshatafuta *raw materials* zinapatikana, wananunua na kuanza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaanza mchakato wa ajira, unachukua miezi mitatu ndiyo tumpate huyo mtaalamu kuja kutengeneza bidhaa hiyo ambayo wenzetu wameshaanza mara moja, lakini sisi hiyo kupata *raw materials* lazima mchakato pia uwepo wa manunuzi unaochukua zaidi ya miezi mitatu. Unaporudi, unaanza kutengeneza bidhaa, unakuta ama imeshatoka kwenye soko au lile soko limeshakuwa *captured* na *private sector*. Kwa hiyo, hatuwezi kushindana na ndiyo maana unaona pia hakuna tija kwenye mashirika yetu.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri tukitaka kufanya bishara lazima tubadilike. Yale mashirika ambayo yanafanya biashara, tuwape uhuru wa kufanya maamuzi haraka. Tunaweza kukasimu madaraka kwenye bodi ili waweze kufanya maamuzi haraka ili wafanye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara haihitaji mchakato wa miezi mitatu na kuendelea, biashara haihitaji *theories,* biashara inahitaji maamuzi. Biashara ni maamuzi na biashara lazima uamue kwa sababu biashara ina-*determine* soko. Soko likipatikana leo, lazima upambane kulipata leo, huwezi kupambana kwa ajili ya kusubiri mchakato. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wako ulishakuwa umeisha, nilikuacha kwa sababu ni wewe ni mtu wa mwisho ili umalizie mchango wako. Kwa hiyo, nakupa sekunde 30.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi lakini naomba basi, niunge mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kikao chetu cha leo. Nitaje baadhi ya majina ya ambao tutaanza nao kuchangia mchana kwenye hoja hii. Tunaye Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Juma Othman Hija na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai na Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi kwa ajili ya kuchangia Taarifa za

Kamati hizi tatu ambazo zimewasilishwa katika Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja katika taarifa zote zilizowasilishwa na Kamati za *PAC, LAAC* na *PIC*. Pia nipongeze Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ametoa mazingira rafiki kuweza sisi wote kukaa hapa katika Bunge lako Tukufu na kuweza kujadili taarifa za Kamati hii kwa ajili ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchovu wa fadhila nisipoipongeza Ofisi ya *CAG* ambayo kwa weledi na uzalendo imeleta taarifa zilizoshiba na sisi tukaweza kuzipitia na kudadavua na kuweza kutoa maoni kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba taarifa ya *CAG* tumeipitia, tumeiona, tumehoji Wenyeviti wa Taasisi na Maafisa Masuuli pamoja na wasaidizi wao. Katika maeneo hayo nitaomba nijikite katika eneo moja, dosari katika usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, tutaona katika maeneo haya michango mingi imejikita katika eneo hili. Ni kwa sababu gani? Kwa sababu eneo hili ni eneo ambalo linagusa maslahi ya wananchi moja kwa moja, ambapo Mheshimiwa Rais anatafuta fedha ili ziende kuleta thamani ya fedha katika miradi mbalimbali ya maendeleo lakini tunaona watu wachache, wanaweza kufanya utendaji wa uzembe, usiozingatia misingi ya kanuni na sheria na kuweza kutumia hizi fedha kinyume cha taratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika mfano wa baadhi ya taasisi ambazo tunaona katika utendaji kazi wake zimeweza kwenda ndivyo sivyo. Nianze na Taasisi ya *TANROADS*. *TANROADS* ni taasisi ambayo imepewa dhamana ya kujenga miundombinu ambayo inagusa moja kwa moja maslahi ya mwananchi katika miundombinu ya barabara na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* wapo wataalam, wapo wanasheria wazuri, wapo viongozi ambao wamepewa dhamana na Serikali na ukiangalia wanajua sheria zote, lakini tunaona kwamba katika eneo hili badala ya kuzingatia sheria na kanuni zinazoongoza taasisi hiyo, watu wanatoa *certificate za* kumaliza kazi, siku zinaisha za kisheria 28, Mataifa ya nje 56 bado fedha hazijalipwa, Serikali inaingia katika hasara. Tunaona hasara ya bilioni 68.7.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakokotoa kwa ufupi kuona hizi fedha kwa bajeti yetu ya *TARURA* ile ambayo majimbo yetu tunapokea bilioni 2.5, majimbo 30 yote yangepata bajeti ya mwaka mzima, lakini hizi fedha zote zimehama kwenda kulipa riba kwa sababu ya kuchelewesha malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili haliwezi kuvumilika. Kwa hiyo kupitia Bunge lako tukufu niombe hawa watumishi ambao walitakiwa kufanya kazi kwa weledi wajitathmini na Bunge lako litakuja na mapendekezo ambapo niombe Wabunge waniunge mkono ili iweze kuingia kama moja ya maazimio ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la Mkataba wa Mradi wa *REA I, REA II, REA III* ambao kwa uchache tu *CAG* ame-*spot* Mkoa wa Mara. Kwenye *scenario* hii

unaona kampuni moja tu inaweza kutumia milioni 329 za Serikali haiguswi, haisemwi chochote, haichukuliwi hatua. Ukiangalia mambo mengine kwa kweli yanaumiza. Hii kampuni ya *Derm Electrics Tanzania Limited* hizi pesa ilinunua vifaa vya kuweza kusimamisha miundombinu ya umeme. Miundombinu haikusimamishwa, watu zaidi ya 4000 hawakupata huduma. Hivyo vifaa badala ya kuvikabidhi *TANESCO,* imebaki navyo na mpaka leo hakuna hatua yoyote ya kisheria ambayo imechukuliwa. Sasa unajiuliza katika eneo hili hivi kiburi hiki hii kampuni inakitoa wapi?

Mheshimiwa Spika, watumishi ambao wanasimamia kampuni hii na miradi hii kiburi cha kutokuchukua hatua wanakitoa wapi? Niombe kupitia Bunge lako Tukufu. Tabia hii tukiiacha ikaendelea itaambukiza na watumishi wengine ambao ni wazalendo kwa nchi hii waweze kuiga matendo ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo niombe sana katika Bunge lako Tukufu tuweze kuchukua hatua ambazo baadaye nitapendekeza.

Mheshimiwa Spika, wakati roho yangu inaendelea kuuma na kusononeka kwa hujuma hizi dhidi ya Serikali, nikapitia hotuba ya mbeba maono wa nchi hii Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alivyohutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 April 2021. Naomba kunukuu. Katika eneo hili tukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ukurasa wa 32 amesema yafuatayo; "Serikali ya Awamu ya Sita kama ilivyokuwa Awamu ya Tano itaendeleza jitihada za kuimarisha nidhamu ya uwajibikaji kwenye Utumishi wa Umma. Tunakusudia kuimarisha taasisi na pia kuweka mifumo ya uwajibikaji ambayo itahakikisha kwamba viongozi na watumishi wa umma katika ngazi zote wanawekewa malengo yanayopimika. Mfumo uliopo wa sasa ikiwemo mikataba

kati ya kiongozi na walio chini yake pamoja na *OPRAS* tutaiangalia upya."

Mheshimiwa Spika, nitakuja kueleza kitu juu ya *OPRAS*. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais akaenda mbali akasema: "Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao na msisitizo akasema hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi, wabadhirifu wa mali za umma."

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Rais ameshatuwekea mambo kibla, tumsogezee kwenye 18 amalize kufunga mabao. Hawa wote ambao wamehusika katika kuhujumu fedha za Serikali, tumsogezee amalize kazi. Mheshimiwa Rais ahangaike kutafuta fedha, lakini usimamizi huu kupitia Bunge lako Tukufu, tuweze kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine, tunaona kwamba katika mapendekezo ambayo ningeomba kuleta kwenu, niombe kweli kupitia Bunge hili, Bunge liridhie watumishi wote waliosababisha hasara hizi na Maafisa Masuuli wote wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria pia mamlaka za uteuzi zinapoona yule aliyekosa na anahusika, ni suala dogo la Mheshimiwa Rais na viongozi waandamizi kuchukua hatua mara moja ili tutoe huu uozo uliopo ili tuweze kuleta watu wengine ambao wanaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo niombe Bunge lako Tukufu, kupitia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais kuna kipengele ambacho nimesoma anasema *OPRAS* tutaiangalia upya. *OPRAS* ni tathmini ya utendaji kazi ya watumishi wote wa umma, kuanzia Ma-*CEO* na wasaidizi wao. Ningeomba maboresho yanayoletwa yawahusu

Maafisa Masuhuli. Katika eneo hili nimeangalia vipengele nane vilivyopo katika *OPRAS* vyote hakuna kitu kinachoongelea suala la hoja za Serikali za *CAG* katika taasisi husika. Kwa hiyo unampima kiongozi wa taasisi, hii *OPRAS* ambayo ni kipimo cha kazi, lakini hakuna sehemu ambapo tunamuuliza kwa nini ulipata hoja hii? Kwa nini hukujibu hoja hii na kwa nini uliweza kupata hati isiyoridhisha? Hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kupitia Bunge lako Tukufu niombe katika vipengele nane hivi kiongezwe kipengele cha tisa ambacho kitasaidia kuweka kipengele cha hoja za *CAG* ili Mkuu wa Taasisi awe anatathminiwa na anayemtathmini akienda pale inabidi agote kidogo ili kuhakikisha kwamba yote ameya-*capture*.

Mheshimiwa Spika, katika pendekezo la mwisho na ombi kwa Bunge lako Tukufu, nikuombe, kwanza kabla ya ombi hili nikupongeze kwa kuwa wewe umekuwa mtu wa maono na kabla ya taarifa hii kuja ulituongezea muda wa kufanya kazi kwa hizi Kamati zote tatu, tangu tarehe 10 sisi tuko hapa, tunakaa mpaka usiku. Pamoja na muda na maono yako ya mwanzo tumeweza kupitia taarifa hizi chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachokuomba, kwa uweledi wako na maono, uangalie namna njema ambapo Kamati hizi zitaongezewa muda ili tuweze kupitia taarifa hizi kwa kina na kwa wingi. Hakika nakwambia kwa hili utakalolifanya kwa Taifa hili, tuko tayari kukujengea mnara mmoja ubandikwe Dodoma na mwingine tuupeleke Dar es Salaam kwa sababu utakuwa umefanya kazi ya kizalendo ambayo haijawahi kutokea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana haya mambo ni mema kwa ajili ya nchi yetu, tuungane pamoja kumsaidia Mheshimiwa Rais ili hizi fedha zisimamiwe vizuri, miradi ionekane kwa wananchi katika majimbo yetu yote na baada ya hapo Serikali itapongezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa nafasi na naomba kuunga mkono hoja taarifa zote ambazo zimewasilishwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Agness Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusiana na Kamati za *PAC, PIC* pamoja na *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye hoja ya *KADCO*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la *KADCO,* lakini wengi hawajaingia kwa ndani sana. Binafsi naomba niweze kuelezea kwamba *KADCO* ni mtoto mmoja aliyezaliwa tarehe 11 Machi, 1998 akiwa na wazazi wawili ambao ni, *Mott McDonald* aliyekuwa na hisa asilimia 99 na mtu mwingine anaitwa *Inter-Consult Tanzania Limited* akiwa na hisa asilimia moja. Kampuni hii ilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 kama shirika binafsi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Julai, 1998, *KADCO* waliingia makubaliano na Serikali pamoja na *McDonald* lakini alikuja kujiunga mtu mwingine anaitwa South

*African Infrastructure Fund* wakagawana *shareholders* kati ya Serikali na wale wamiliki wengine. Serikali ikachukua asilimia 24 ya hisa, *McDonald* wakawa na asilimia 41.4 ya hisa. *South African Infrastructure Fund* wakawa na asilimia 30 ya hisa, *Inter-consult* wakawa na asilimia 4.6.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Novemba, 1998, *KADCO* na Serikali wakaingia mkataba wa uendeshaji kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu kwenye uwanja wa *KIA* inaendelezwa kwa miaka 25. Mwaka 2006 baada ya miaka hiyo yote, Serikali ilikuja ikafanya tathmni ya *KADCO* kama inafanya kazi ipasavyo kulingana na *concession agreement* lakini baada ya tathmini Serikali ikasema kwamba tuangalie masuala yafuatayo:-

Je, *KADCO* inafanya kazi kama ilivyokubaliwa? Serikali ikagundua kwamba wanahisa wenzake ambao ni *Mott McDonald* waliokuwa na asilimia 41.4, *South Africa Infrastructure Fund* waliokuwa na asilimia 30 ya hisa, Serikali ambayo ilikuwa na asilimia 24 na *Inter-Consult Tanzania Limited* waliokuwa na asilimia 4.6. Serikali ikaja kuona kwamba hao wenzake wanahisa hawafanyi kazi vizuri. Serikali ikaamua kwamba, sasa umefika wakati wa kuchukua *KADCO* moja kwa moja na kununua hisa zote kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, kinachotushangaza, kinachonishangaza mimi kama Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, tumemwita Afisa Masuuli Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, tumemuuliza kuhusiana na hawa watu *McDonald, South Africa Infrastructure Fund* pamoja na *Inter-Consult Limited* hizo hisa zao zilikuwa na *value* kiasi gani? Hakuna jibu mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza tena, baada ya Serikali kuchukua hisa zote kwa asilimia mia moja, Serikali kupitia *TAA* ikaenda kukopa fedha kutoka *CRDB USD* million *5.3* kwa ajili ya kuwalipa wanahisa wenzake ambao wameshindwa kazi. Hata hivyo, tunachojiuliza hizo fedha zimelipwa kwa kigezo gani? Tumechukua mkopo ambao utalipwa na Serikali kupitia fedha za walipakodi shilingi milioni 5.3 *USD* kwa ajili ya kuwalipa watu ambao hatukujua hizo hisa zao zina *value* kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza vile vile, leo bado Serikali baada ya kununua hisa zote bado tuna *concession agreement* na *KADCO*. Huyu *KADCO* ni nani? Ni swali la kujiuliza huyu *KADCO* ni nani ambaye bado tuna *concession agreement* ya miaka 25 ambayo huuhishaji wake utaisha tarehe 16 Julai, 2025. Kama Serikali imesajili kwa mujibu wa mashirika ya umma huyu *KADCO* ni nani ambaye bado tuna *concession agreement* na yeye? fedha za walipakodi bado zinapotea kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninachojiuliza, kama ni *TAA* ilichukua mkopo kutoka *CRDB* shilingi milioni 5.3 Dola za Marekani, maana yake wao ndio wangetakiwa kusimamia Uwanja wa *KIA* na siyo mtu mwingine tena. Kwa hiyo nitoe pendekezo kama kweli tupo tayari kwa ajili ya kuisaidia nchi hii hatuhitaji kumsikia mtu anaitwa *KADCO,* labda waje watupe jibu hapa ndani kwamba *KADCO* ni nani ambaye sisi Wabunge wengine hatumjui. Kwa hiyo Uwanja wa *KIA* ukabidhiwe kwa *TAA* ili waweze kuendesha kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika kupitia ripoti za *CAG* kuna mtu anaitwa *DUWASA* hapa Dodoma, ambao wanatusaidia kusimamia miradi ya maji, kwenye

ripoti ya *CAG* tumeona kwamba *DUWASA* walichimba visima viwili Kongwa vyenye thamani ya Shilingi Billion1.5. Kitu cha kushangaza kisima kimoja baada ya Miezi Mitano hakitoi maji, kisima kingine hakijawahi kutumika kwa sababu maji yana chumvi, kuwauliza kwa nini? Wanasema tulikuja kuona kwamba yale maji yana chumvi. Kinachoshangaza kwani watalam wetu wanapochimba maji, tuna maabara ya maji, kabla ya maji kutumika ni lazima tupeleke kwenye maabara ya maji yakaangaliwe ubora wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumepoteza Fedha za wananchi kwa kuchimba visima, kisima kingine baada ya miezi mitano hakifanyi kazi, tumeishapoteza fedha na naamini ni fedha za walipa kodi. Suala lingine la kusangaza kwenye mradi huohuo ulikabidhiwa mitambo na kibanda ambacho kilikuwa na pampu lakini haijawahi kutumika hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, nishauri fedha hizi za walipa kodi zinalipwa na Watanzania nasi kama Wabunge tulipewa nafasi hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunazilinda hizo fedha ili zilete manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nigusie suala la *TRA* kwenye ripoti ya *CAG* kutoka Mwaka 2018/2019 mpaka 2020/2021, *TRA* imeshindwa kukusanya Shilingi Trilioni 6.78, lakini tunajua kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania tumewakabidhi jukumu la kuhakikisha kwamba wanatukusanyia fedha kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo. Kila Mbunge yupo kwenye Bunge hili na anataka maendeleo yaende kwenye Jimbo lake, lakini *TRA* Watumishi waliopo wamekuwa wanashindwa kukusanya mapato yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nishauri Bunge lako Tukufu, kuna mianya mingi ya rushwa kwa sababu ya *TRA*, ukijaribu kuangalia kuna makadirio ya chini ya kodi nyingi *in value* inaweza ikafika zaidi ya Billion 30 lakini kuna maeneo mengine wanashindwa kukusanya kodi. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 wameshindwa kukusanya Shilingi Billion 8.5 kwa mafuta yanayotumiwa ndani ya nchi. Kwa hiyo TRA wanatakiwa nao kusimamiwa kwa ajili ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwa Kamati zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii kwenye taarifa zilizopo mbele yetu kwa nia ya kutaka kulisaidia Bunge lakini pia kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee sana ninatoa pongezi kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kikisimamiwa na Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan ikiongozwa na Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa kwa kazi kubwa zinazofanyika Tanzania na maeneo mbalimbali kwenye Majimbo yetu na kila mtu anaona sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumepewa nafasi kubwa sana ya kuwasaidia Watanzania, kwa wale

wapenzi wa mpira wa miguu wanafahamu kuna wakati wanafika wanasema *the ball is on our court* yaani ukifikia pale nusu ya pili ya kutaka kumaliza mpira na nyinyi ndiyo mnakwenda vizuri mnalazimika kumaliza vizuri. Nipongeze sana taarifa hii iliyoletwa hapa na *CAG* kwamba yeye ametimiza wajibu wake wote pasipo kuacha nafasi yeyote. Pia Kamati mbalimbali ambazo ripoti zake tunazijadili hapa leo na wenyewe wamefanya kazi yao nzuri sana, sisi wengine sio Wajumbe wa hizi Kamati ambapo ripoti zake tunajadili tunatoka kwenye kamati tofuti. Lakini tupo hapa na mimi nitatoa mchango wangu nikiegemea kwenye taarifa iliyoletwa na Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, bila kumung'unya maneno kabisa kwenye Kamati ya *PAC* kwenye ukurasa wake wa kwanza kwenye maneno yake ya utangulizi *paragraph* ya pili, wanasema hivi katika taarifa hii Kamati imebainisha maeneo kadhaa ambayo taarifa za *CAG* zimebainisha uwepo wa changamoto ya matumizi mabaya ya Fedha za Umma. Maeneo hayo ni pamoja na Serikali kupata hasara ya Shilingi ya Billion 68.73 ambayo ni riba zinazosababishwa na Wakala wa Barabara *TANROADS,* kwa hiyo hapa Kamati wameamua kuimulika wazi kabisa *TANROADS* na jambo hili lipo kwetu kama Wabunge na wewe ndiye kiongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunao wajibu sasa wakumsaidia Mheshimiwa Rais, ripoti hii kuisaidia nchi hii pia, ripoti tunayoijadili tunategemea tuache yale mambo kama ambayo yalikuwa yanatokea labda tunaweza tukasema ya *business as usual,* tumepewa sasa nafasi yakusema wazi na ukweli na wewe kama Spika lazima uache historia ndani ya jengo hili, kwamba wakati wako uliitaka Serikali ilete taarifa ama za kuwawajibisha watu waliosababisha hasara hizi au wewe mwenyewe kuunda

Tume Teule za kwenda kuchunguza maeneo haya yanayotajwa sana ndani ya ripoti ya *CAG*. Hii ndiyo namna pekee ya kuweza kulisaidia Bunge letu na kuweza kulisaidia Taifa letu pia lakuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais, nikiangalia nia nzuri kabisa ya watu wa *CAG* wanataka kuona tunatoka hapa tulipokwama tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati fulani taarifa kama hizi zilizo wazi namna hii tulikuwa hatuzipati kila mara lakini leo taariafa inaeleza mapungufu makubwa haya tena tu kwenye baadhi ya maeneo ambayo yeye ameamua kuyataja na kuyakagua. Sasa kama hasara ya namna hii shilingi bilioni 68.73 inapatikana *TANROADS* peke yake, lakini *TANROADS* tunaamini wanayo Bodi, *TANROADS* ina viongozi wake wakiwemo Wakurugenzi Wakuu ambao bado mpaka sasa hivi wanatumikia nasi tuko hapa kama Wabunge, kwa niaba wa wananchi tunaona hasara hizi zinazoletwa na *CAG* amejaribu kufungua jicho lake na kutuelekeza mambo yanayotokea kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, tusitoke hapa mikono mitupu. Hakikisha mambo haya yanakwenda kukomeshwa katika maamuzi yetu tutakayoyafanya ili siku moja tukumbukwe kwamba tulisaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa SpikaNimetaja tu *TANROADS* peke yake lakini tunayo *MSD,* Mheshimiwa Tunza, jana wakati anachangia na yeye namshukuru kwa mchango wake mzuri, alieleza vizuri namna ambavyo *MSD* wameshindwa kutekeleza wajibu wao kwenye baadhi ya maeneo. Halmashauri yetu ya Wilaya ya Masasi *DC* peke yetu tuna karibia Shilingi Billion 180 ya dawa ambazo zinatakiwa zikateketezwe. Waliopeleka dawa hizi Masasi wanafahamika, waliokuwa wanazitunza kwenye bohari

zetu wanafahamika. *MSD* bado ipo, Bodi ya *MSD* nayo bado ipo.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia *TPA* kwenye taarifa ya *CAG* na pia kwenye taarifa hata hii ya Kamati na wenyewe wametaja, kuna ubadhirifu mkubwa uliofanyika kwenye Bandari ya Mwanza, kuna ubadhiru mkubwa uliofanyika kwenye Bandari ya Kigoma lakini pia na Bandari ya Mtwara kuna harufu za ubadhilifu. Sasa tuko hapa kusaidia kwa hiyo tunaomba wazi na tunaelekea mwishoni sasa kwa hiyo *TPA* nayo paundwe Tume au Kamati Maalum itayokwenda kufuatilia mambo haya ili tuweze Kwenda mbele kwa sababu kuna sehemu tumekwama. *ATCL* nayo imetajwa.

Mheshimiwa Spika, *KADCO* nayo Mheshimiwa Shangai, alichangia vizuri na ameeleza yeye anatoka eneo hili ni mtu anaefahamu vizuri historia nzima ya *KADCO* na mambo wanayoyafanya. Tuombe sana ili tuweze kusaidia nchi yetu tuondoke hapa tulipo simama.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo linasababisha labda wakati fulani hata *inflation* hii tunayoiyona tunaweza tukasema *it's a created inflation*. Kuna suala la madai ya wakandarasi *CAG* nalo wameliangalia, mwaka 2017/2018 Wandarasi wa ndani walikuwa wanadai *almost* shilingi trilioni tatu. Mwaka 2018/2019 trilionI 2.7. Sasa hivi 2019/2020 wakandarasi wa ndani wanadai zaidi ya shilingi trilion 3.1. Tunaitaka Serikali ilipe madeni haya yatakwenda kusaidia kupunguza nakisi ya upandaji wa gharama huko nje kwa sababu maisha siyo marahisi tena kama ambavyo tulizoea.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukumbuke Wakandarasi hawa na wenyewe wanakopa kwenye mabenki na kuna wanaofilisiwa huko kwenye mabenki wanapokopa ili kuendeleza hii miradi ya Serikli. Sasa kwa nini Serikali haitaki kulipa kwa wakati Wakandarasi wanapofanya kazi, hata kama wengine wameisha *raise* hizo *certificate* ili kuweza sasa namna ya kuona kuyafuta hayo madeni kwenye vitabu vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanakwenda siyo hapo tu. Mpaka sasa *CAG* anao uwezo wa kukagua Taasisi nyingi za Serikali, lakini nitoe mfano mmoja ambao nasisi tunaona kuna haja au kuongeza wigo, kuna maeneo mengine yanakaguliwa na watu wa *COASCO,* kwa mfano niseme masuala ya ushirika wanaokagua kwenye hivi Vyama vya Ushirika ni *COASCO*. Hata hivyo mambo yakiwa mazito sana Serikali huwa inaweka mkono wake na ripoti za *COASCO* siyo kila mara na sikumbuki kama mara ya mwisho ni lini zililetwa hapa ndani kwa ajili ya kuzijadili.

Mheshimiwa Spika, hapa karibuni tumeona Serikali imekuwa na nia njema sana ikaunda Tume ya Kamati ya pamoja ya manunuzi ya pembejeo, kuna malalamiko makubwa kwamba pembejeo hizi kwa wakulima hasa nitoe mfano kwa wakulima wa korosho hazijawafikia ama kwa wakati lakini wakati mwengine haziwafikia kabisa au zimefika zikiwa chache kiasi wao wanaona ni bora tukarudi kwenye ule mfumo wa zamani Serikali ikitoa pesa basi waende kutumia kwenye ruzuku badala ya kutengeneza hiki kikundi ambacho wanasema ni Kamati maalumu, kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana, sasa tuombe badala ya ukaguzi wao kufanywa na *CAG* peke yake ikiwezekana ukaguzi maeneo haya ufanywe na Ofisi ya *CAG* badala ya kuachia hawa *COASCO* peke yao,

ambao siku zote wamekuwa wanakaa na hawa watu wa vyama vya ushirika nakuona mambo wakati mwingine namna wanavyoweza kuyatengeneza ili yaweze kuwanufahisha wao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii ambavyo tunakwenda na Bunge tunakwenda sasa kuhitimisha nafikiri kesho tutakuwa tunahitimisha hoja zilizopo hapo hapa mbele yetu, niombe sana Kiti chako kiunde Kamati Teule kwenda kuchunguza maeneo haya ambayo Wabunge wote waliyosimama hapa wamechangia na wameyataja, ikiwemo *MSD, TPA, TPDC, ATCL, KADCO* pamoja na *TANROADS* tutakuwa tumetenda haki kwa ajili ya nchi yetu pia tutakuwa tumeweza kusaidia nchi yetu kuweza ku-*move* mbele.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanywa na Kamati ya *PAC,* kazi iliyofanywa na *LAAC* vilevile na kazi iliyofanywa na *CAG* ni kazi nzuri sana kuacha zikaishia hapa katika sisi tu kuzijadili na hatua zake zisionekane. Aache historia katika Bunge hili na aache historia katika Nchi hii kwa kuelekeza Serikali katika kuhakikisha haya yanayotajwa, hasara zinazopatikana kwenye vyombo mbalimbali vya Serikali pia ubadhirifu unaotajwa waziwazi kwenye maeneo haya ushulikiwe, nasi tuweze kujisifia kwamba kuna wakati tuliweza kuisaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ambazo zimeletwa hapa mbele yetu pia nisisitize kwa kifupi kwamba kuna haja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza maeneo haya ili kuweza kusema ukweli yanayojili ndani kwenye vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni na Mheshimiwa Juma Othman Hija ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza kwakunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani kwanza nianze kwa kuunga hoja zote tatu mkono.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anaendelea kututumikia Watanzania na tunaridhika na kazi nzuri anayoifanya. Vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhira nisipokushukuru na kukupongeza wewe kwa umakini, unaona kabisa kwamba kazi ya kuisimania Serikali kwa siku hizi mbili, tatu ukitoka nje ya Bunge lako hili wananchi wanaifurahia ni kwa sababu unatuelekeza vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kwenye hoja Mahsusi ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mimi ni Mjumbe wa Kamati. Taarifa ya CAG inaonyesha dhahiri kwamba dosari zote za matumizi mabaya ya fedha za Serikali yanatokana na mambo matatu:

(i) Kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma;

(ii) Kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa; tunaijua wote Sheria Na. 9 Sura ya 283 ya Mwaka 1982 na marekebisho yake;

(iii) Kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma. Hapo ndiyo msingi wa mambo yote

ambayo Wabunge wako hapa wamekuwa wakiyachangia katika nyakati tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza, hivyo sasa kama Bunge lako linakaa hapa tunatunga Sheria nikawa najiuliza inawezekana kwa sababu siyo Mwanasheria lakini wewe ni mbobevu kwenye hili eneo, hizo Sheria tunazozitunga kwenye Bunge lako Tukufu hili hazitoi adhabu? Sheria zinapaswa kusimamiwa na tunajua asiyetekeleza jambo lolote kwa mujibu wa Sheria husika, kwa maana anayevunja hiyo Sheria anapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa maeneo ambayo yanaonekana hayaridhishi naomba tu niseme mifano michache. Kwenye taarifa ya *CAG* imeonekana matumizi ya fedha mbichi, fedha ambazo hazikupelekwa benki kiasi cha Shilingi Billion 17 ambazo hizo ni kwa Mamlaka 147 tu, kwa maana *POS* zimekusanya lakini hizi fedha zimetumika mbichi. Jambo la kusikitisha siyo kwamba zimetumika kwa shughuli za maendeleo, hazijulikani!

Mheshimiwa Spika, hiyo imethibishwa na baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizotokea mbele ya Kamati. Eneo lingine ni Matumizi ya Fedha za akaunti ya Amana. Akaunti ya Amana siyo akaunti ya matumizi kwa Halmashauri za Wilaya lakini inaonekana Jumla ya Shilingi Billion 9.74 kwa Halmashauri 81 haya matumizi yake hayakusimamiwa. Inasikitisha, Mkurugenzi mmoja wapo kwenye Kamati alipoulizwa kwa nini ulitumia fedha zilizopo kwenye akaunti ya Amana zaidi ya Million 95? Alijibu kwa jibu ambalo linasikitisha bila kuogopa akasema hizo fedha za Akaunti ya Amana hazina rangi kwani fedha zina rangi? Maana yake nini? Maana yake

Maafisa Masuuli hawana uwoga na fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine limetajwa sana, hivyo wakati Watanzania wengi wanalalamika kwamba hakuna dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Ukiangaria ripoti ya CAG kwa miaka mitatu mfulilizo jumla yake ni Billion 12.362, dawa ambazo zimekwisha muda wake kwa kipindi cha Miezi Mitatu mpaka miaka 20, madhara yake dawa hizi pia zikiingia kwa watumishi wasio waadilifu Watanzania tutapata madhara. Hata hivyo taarifa ya *CAG* inasema anaona mapendekezo yake aliyotoa kwa miaka mitatu mfululizo hayajafanyiwa kazi. Je, Bunge napo linapofanya kazi yake ya kuisimamia Serikali bado yasifanyiwe kazi? Hayo ndiyo maswali ya kujiuliza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ile Sheria ya Manunuzi malipo ya bidhaa za huduma ambazo hazikupokelewa Billion 8.44 kwa Halmashauri 61. Ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi Billion 7.93 kwa Halmashauri 42, pamoja na hasara zinazopelekewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kama vile Mfuko wa Bima ya Afya, *MSD, GPSA, TEMESA* na zinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania kwenye maeneo mbalimbali kwa sasa wanalitegemea Bunge lako Tukufu. Wabunge wanafanya kazi yao ya kuisimamia Serikali, hivyo ninaungana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye Kamati lakini na Wabunge kwamba ni wakati sasa wa kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya wale wote wanavunja Sheria. Haiwezekani, kwanini tukae hapa Bunge litunge Sheria, lakini Sheria zinapaswa

kusimamiwa, lakini ziwe zinavunjwa halafu hakuna hatua zinazochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile Halmashauri chache tu ambazo zilitokea mbele ya Kamati inaonyesha kwamba ukiharibu Halmashauri 'A' unahamishiwa Halmashauri 'B'. Ukiharibu Halmashauri 'B' unahamishiwa Halmashauri 'D', sasa huo utaratibu huo ndiyo unazozifanya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutokufanya vizuri, ni kwanini? Kwa sababu hawana woga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa je, tutaendelea kwa utaratibu huu halafu tutasema tunamsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Hapana, inatosha! Kwa sababu, *CAG* ameonesha mapungufu hayo yote, na sisi tunayatambua hayo maeneo; jukumu letu hapa kwa kamati hizi na kwa taarifa hizi kwa kipindi hiki ni kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, mimi nadhani naomba nisisitizwe, kwamba hoja za Wabunge walizosema, kwamba sasa Bunge liazimie katika eneo lolote ambapo sheria ilivunjwa hatua stahiki zichukuliwe. Kwa utaratibu gani, Bunge liielekeze Serikali kwa sababu, lina wajibu wa kuisimamia. Hiyo itatuepusha sisi kurudi hapa kuja kusema kila mwaka tunarejea kwenye hoja zilezile ambazo kimsingi hazionekani kurekebishika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mifano hiyo unaona namna ambavyo Serikali inapata hasara. Sasa kumbe kwenye maeneo hayo yote iwapo usimamizi huo ungekuwa thabiti ina maana tungeweza kuikoa fedha ya Watanzania. Fedha hizi zingeweza kutoa huduma katika maeneo yetu mbalimbali tunayotoka na hivyo Watanzania pia wangeweza kuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia haya mapungufu ndiyo yanayowagonganisha wananchi na Serikali. Sasa mtu mmoja anapoamua kufanya hili huyo yeye achukuliwe hatua stahiki ili Serikali iwe salama kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na sasa ukiangalia mapendekezo ya *CAG,* ambapo kwenye maeneo mengi sana wajumbe wamesema, anashauri, anashauri; lakini kwenye maeneo mengine amebainisha kwamba mapendekezo anayatoa hayafanyiwi kazi. Tujiulize kuna nini? Hivi si kweli kwamba kuna eneo labda wale wanaofanya pengine kuna, mimi sijajua, lakini pengine kama Bunge tutafakari, kuna nini? Kwamba *CAG* anapotoa pendekezo, anaposhauri halifanyiwi kazi, mtu anahamishwa kutoka *Point A* kwenda *Point B* akaendelee kuharibu; kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wengine wanaweza wakatoa majibu ya haraka tu, hayo hayahitaji chuo kikuu. Mwingine atasema labda kuna kulindana, mwingine atasema labda sijui ni nini, labda ni mtoto wa fulani.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi hapa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Sisi hatuna cha mtoto wa shangazi, hatuna cha mtoto wa mjomba, sheria ifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja nikiamini kwamba hayo yote yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijamaliza, yale mapungufu yote kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuna Sekretarieti ya Mkoa pale. Mimi ninaomba niwashawishi Wabunge moja ya azimio liwe Serikali ifanye

tathmini ya kina nini kazi inafanywa na Sekretarieti za Mikoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, wakuu wa *section* wapo hapo, inakuwaje mpaka mwaka unaisha ndipo kunaonekana madudu mpaka *CAG* anaenda kufuatilia, wakuu wa *section* wapo? Wanasubiri Mkuu wa Mkoa aende kwenye ziara? Wanasubiri Waziri aende kwenye ziara? Wana jukumu gani pale? hilo ni suala la kufanyiwa tathmini ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Othman Hija, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji. Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga ajiandae.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni hii ili nami nitoe mchango wangu katika Kamati hizi tatu za *PAC, PIC* na *LAAC*. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati tatu hizi pamoja na wajumbe wao wote kwa namna walivyotayarisha na hatimaye kuwasilisha ripoti zao katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa. Mimi katika mchango wangu wa leo nitachangia kuhusu ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji kazi katika wizara, idara na mashirika yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba, baada ya miaka 60 yetu ya uhuru bado kuna idara zetu na mashirika yetu yanafanya kazi kwa kukiuka taratibu. Hasa inasikitisha zaidi unapoona

kwamba yanayofanyika na wanaofanya haya ni wale ambao wanatakiwa wasimamie utaratibu ule; ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, katika Ripoti ya *CAG* imeonekana kwamba *Lindi Regional Police Commander* walimkodia *OCD* wao ofisi kutoka *National Housing* kwa malipo ya 1,770,000/=. Katika hili polisi walikuwa wanalipa pungufu; 1,770,000/= wao walikuwa wanalipa 1,500,000/=. Kwa hiyo kulikuwa kuna bakaa ya kama 200,000/= kila mwezi. Hii ime-*accumulate* fedha jumla ya milioni 37 ambazo mpaka sasahivi hawajalipa.

Mheshimiwa Spika, lakini *issue* si hiyo, *issue* ni kwamba hakukuwa na mkataba baina ya Polisi na *National Housing,* mambo yalikuwa yanakwenda kihivihivi tu. Ndipo pale ninaposema kwamba inasikitisha zaidi kuona kwamba wale wasimamizi wa sheria ndio ambao wanavuruga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili utakwenda kwenye kutekeleza hoja za ukaguzi. Asubuhi hii kuna mjumbe mmoja, Mheshimiwa Tarimba, alisimama akaeleza namna ya dharau watendaji wetu wanavyodharau. Katika Ripoti ya *CAG* imeonekana kwamba, katika kipindi cha 2019 Jeshi la Polisi walipewa hoja 13 na *CAG,* lakini mpaka kufikia hii leo hapa tulipo wametekeleza hoja tatu tu. Kwa hiyo, hii ni ile dharau, kwamba wao wanadharau maelekezo hata ya *CAG.* Wamepewa hoja 13 wametekeleza tatu tu mpaka hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu na la mwisho ni kuhusu kutokutekeleza hata ile mipango yao wanayopanga. Katika uchunguzi wa *CAG* imeonekana kwamba *National*

*Housing* katika mipango yao ya 2015/2016, katika *strategy planning* yao, walijipangia wenyewe watengeneze kampuni tanzu ambayo itawasaidia kwenye mambo yao ya uendeshaji, lakini mpaka hii leo tuko hapa kampuni tanzu hii hawajafanya na zoezi hili bado linasuasua.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa haya yangu matatu niliyochangia naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mheshimiwa Zahoro Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati nikiwa kama mjumbe niliyetoka katika Kamati ya *PIC*.

Mheshimiwa Spika, kuanzia juzi tumekuwa tukijadili hoja za kamati tatu, ambapo tuna hoja ya *PIC, LAAC* pamoja na *PAC*. Bahati nzuri nashukuru sana kwamba kwa kila moja amechangia au tunachangia kwa mujibu wa kuweza kuishauri Serikali; na kwa kweli tunafanya kazi ya kuishauri Serikali vizuri sana na kuweza kusema kwamba, kuishauri Serikali pamoja na kutoa mawazo ambayo kila kamati maana yake yaliyokuwa yamo.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema kuna mambo mengi ambayo yamo katika zile ripoti, lakini mimi niweze kujielekeza zaidi katika Kamati yangu ya *PIC*. Kamati yetu ya *PIC* ni kamati ambayo ipo kama jicho la Bunge katika kusimamia uwekezaji wa mitaji ya umma. Pamoja na hayo katika uwekezaji wa mitaji ya umma suala ambalo

tunalitazama, tunaangalia vitu vitatu katika uwekezaji wetu wa mitaji ya umma. Kitu cha kwanza tunachokiangalia pale ni suala la ufanisi katika mashirika yetu; tunajaribu kuangalia suala la sheria kama zinafuatwa katika hali ya utaratibu katika ile mitaji ya umma katika mashirika yetu; na vilevile tunajaribu kuangalia suala la kibiashara.

Mheshimiwa Spika, sasa katika muktadha huo kamati yetu, kupitia katika uwekezaji wetu, tuna mashirika 237 ambayo ndiyo tunayoyasimamia kupitia hazina. Sasa katika mashirika hayo 237 kuna mashirika ambayo yana hisa chache, kuna mashirika ambayo yana hisa 100 kwa 100 na Serikali na kuna mashirika kama 10 yako nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mashirika hayo kuna mashirika ambayo ni ya kibiashara na kuna mashirika ambayo ni ya kutoa huduma tu kama kawaida, lakini yote yanatumia fedha za Serikali. Sasa kwa muktadha huo maana yake tujaribu kuangalia suala la fedha kwa sababu, sisi tunasimamia mitaji ya umma. Tukizungumzia mitaji ya umma maana yake tunazungumzia suala la fedha, suala la mali zote ambazo zinamilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa hap ani mahali pake. Nadhani kwamba wakati wa bajeti pale tunakuwa tunasema tu fungu limepita au limekubaliwa. Na kwa kweli mafungu mengi tumeyapitisha, lakini utakuta kwamba kwa wakati huu ambapo tunaishauri Serikali, tunapokuja hapa kwa kamati zetu tatu maana yake utakuta kwamba kila mmoja anakuja kuangalia mapungufu yaliyotokana na yale mafungu. Kwa upande wa mashirika ya umma sisi tutakuwa tunaangalia suala la ufanisi, kwamba kuna ufanisi gani, una tija gani katika

mashirika yetu? Tunaangalia je, sheria zilizopo maana yake zinafuatwa au hazifuatwi? Na vilevile yale mashirika kweli yanafuata taratibu za kibiashara?

Mheshimiwa Spika, na upande wa *LAAC* nao wataangalia upande wao kwa upande wa fedha zinazopelekwa katika taasisi za Serikali za mitaa; pamoja na *PAC* nao wataangalia fedha zile za umma zote kwa ujumla. Sasa leo hii tupo hapa kwa ajili ya kuishauri Serikali. Kuna ambao wanaweza kuishauri Serikali lakini wakati uleule kuna wanaoweza kuisema Serikali, kwa sababu kuna kuisemea na kuisema Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza kwamba, kuna kuisema Serikali? Ni kwa sababu wakati mwingine kunakuwa na ule ukiukwaji wa zile sheria au taratibu zinakuwa hazikufuatwa. Pale sisi Wabunge tutakuwa badala ya kuisema Serikali maana yake tutakuwa tunaisema Serikali kwamba hatua hazifuatwi wala hazichukuliwi. Sasa kwa hali hiyo maana yake utakuta kwamba Wabunge wote kila mmoja anapokuja hapa kaja na ukali wa namna ambavyo alivyoona katika ule ufuatiliaji wetu au katika kuona kwetu katika haya mashirika maana yake hayaendi sawa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nije kwa upande wa Kamati yangu ya *PIC* ambapo pale tumependekeza mambo 11. Moja katika mambo ambayo tumependekeza, mimi nije katika mapendekezo mawili. Pendekezo la mwanzo linahusu mchakato wa upatikanaji wa wajumbe wa bodi kwa wakati, lakini mimi

pale badala ya kwamba, kwa wakati nimeingiza neno la wenye weledi. Sasa kwa nini nimezungumza hili kwa kuingiza na neno weledi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, wakati mwingine mashirika mengi ambayo tumeyapitia humo, maana yake kuna mashirika mpaka hii leo yana kipindi cha miaka miwili yanakuwa hayana bodi. Sasa pale tukipima ufanisi wa shirika au ufanisi wa kampuni pale maamuzi yanakuwa si sahihi na ufanisi wenyewe unakuwa si mzuri. Na hata kibiashara kama shirika lile litakuwa ni la kibiashara maana yake biashara ile itakuwa inakwenda pasipo na maamuzi yaliyokuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa bodi zetu, kwa mujibu wa huo ushauri tulioutoa, ningependa sana kwamba, uangaliwe sana. Na ninajua kwamba, wajumbe wengi sana suala la wajumbe wa bodi wamelizungumza, kila mmoja kalizungumza kwa upande wake na kwa upana wake. Sisi kwa upande wetu tutaangalia kwamba, bodi nyingi zinapomaliza muda wake zisichukue muda, ziteuliwe bodi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan alipoizindua hii Taarifa ya *CAG* alisema wazi kwamba, kama kuna tatizo la bodi basi mimi sina tatizo hilo endapo tu nitakapoletewa katika meza yangu ndani ya wiki moja nitateuwa. Hapa inaonekana wazi kwamba inawezekana tatizo likawa liko katika zile taasisi zetu kuu, ikiwa ni pamoja na Wizara, maana hapo katika utendaji na ufanisi huo inawezekana pengine kunakosekana ufanisi na ndio maana hizo taarifa haziendi kwa Rais na inasababisha hata mashirika mengi yakawa yanachelewa kuteua bodi.

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu iko hapa; katika utaratibu wa kuendesha taassisi zetu hizi bodi ndiye msimamizi wa kila kitu katika yale mashirika, ikiwemo mali

pamoja na rasilimali zote za shirika au kampuni. Sasa ikiwa kama bodi au pengine taasisi haina mchunga maana yake hapo kitakachokwenda ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, kitakachokwenda hapo ni ubadhirifu katika shirika lile, au ufanisi na tija katika shirika lile inawezekana pengine usipatikane. Kwa mfano, wakati tulipokuwa tumekaa na mashirika yetu kuna Bodi hii ya Maji ambayo imekaa zaidi ya miaka miwili ambayo tunaita kwamba ni Bodi ya Mfuko wa Maji, bodi ile ina miaka miwili, utakuta kwamba anayekaimu nafasi ile ni Katibu Mkuu. Katibu Mkuu ana muda wake si zaidi ya mwaka mmoja, lakini bado mpaka leo taasisi ile, mfuko ule, hauna bodi, sasa hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ninaweza kusema kwamba, wakati mwingine hii tija au ufanisi tunaoutaka katika mashirika yetu unakuwa haupatikani vile inavyopaswa. Sasa kinachotokea ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, badala ya kuishauri Serikali kwa Wabunge kinachofuata ni kuisema Serikali. Kwa sababu, tutakuwa sasa hatuisemei Serikali, tutakuwa sasa tunaisema Serikali kwa sababu, kila mmoja atakuwa anasema kwa mujibu wa ukali na hatua zake.

Mheshimiwa Spika, sasa nije na suala jingine ambalo katika mapendekezo tuliyopendekeza, Serikali iweke utaratibu wa kuzipatia taasisi zinazojiendesha kibiashara vibali vya kuajiri wenyewe ajira za moja kwa moja. Hilo nalo limekuwa ni tatizo; kwa sababu, uajiri wa Serikali ikiwa ni taasisi ya shirika, ikiwa ni kampuni ambayo inamilikiwa na Serikali uajiri wake, vibali vyake mpaka vitoke utumishi. Sasa, ikiwa shirika ni la kibiashara na linajiendesha vizuri, maana yake kuna haja gani mpaka

kwamba vibali vile viwe na utaratibu? Pengine shirika lina mahitaji ya wafanyakazi zaidi ya 20 au 50 na uwezo wa kifedha wanao wa kuweza kuwalipa, kwa nini wanashindwa kupewa ile ruhusa ya kuweza kuajiri?

Mheshimiwa Spika, na tukikosa ufanisi huo wa wafanyakazi ambao ni rasilimali ya watu, maana yake tutakosa ufanisi wa ile kazi yenyewe, kwa sababu ufanisi wa rasilimali watu haupo. Sasa tukikosa rasilimali watu maana yake na tuna biashara na tunataka ufanisi, maana yake hapo ufanisi utakuwa haupo.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali, yale mashirika au zile taasisi tunazoziona zinajiendesha kibiashara na zina uwezo wa kujilipa au kuwalipa wafanyakazi ni vyema zikapewa ruhusa ya kuweza kuajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije na suala la tatu katika mchango wangu. Wajumbe wengi hapa wamechangia na kila mmoja kachangia hasa katika hali ya ufanisi wa Serikali. Katika suala la ufanisi wa Serikali kuna suala la ufuatiliaji. Hili suala la ufuatiliaji katika hizi taasisi zetu za Serikali linakosekana. Mashirika yetu haya yanaunda mpango kazi *(work plan)* wa miaka mitano au miaka kumi. Pamoja na kwamba kuna *cap eye* ziwekwa, lakini kunakuwa hakuna ufuatiliaji. Kwa hiyo, naomba sana suala la ufuatiliaji Serikali iandae *tools* ambayo siyo *unit,* iwe ni idara ya moja kwa moja ya *monitoring and evaluation* kuweza kuzifuatilia taasisi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona unaniangalia sana; baada ya kusema hayo nasema, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii taarifa ya Maguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)*. Kwanza, napenda nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuongea kwa niaba ya wana Mbogwe, kuhusiana na taarifa ya madudu yaliyooneshwa na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, hii taarifa ni ndefu, imebainisha vitu vingi. Nimejitahidi kadri ya uwezo wangu kuchambua madudu yaliyooneshwa na *CAG*. Anasema amepitia jumla ya taasisi za Serikali na mashirika 331, nikajitahidi kujumlisha hasara zinazooneshwa na *CAG* ambazo zinaonekana za mwaka 2020/2021 mwezi wa Saba japo zipo mpaka za mwaka 2018 na 2019.

Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue vizuri. Kwa vile imetajwa na Halmashauri yangu ya Mbogwe kwamba imo kwenye hati yenye mashaka. Napenda niliambie Bunge lako Tukufu kwamba haya mambo nilisema mapema kwamba nilikuwa siyajui hapo mwanzo, lakini kwa kuwa yamejirudia, naomba nifafanue vizuri ili wananchi wasiwe na hofu kwamba sasa msimamizi wao pamoja na Baraza la Madiwani imekuwaje tena?

Mheshimiwa Spika, ijulikane kwamba hizi taarifa zilizopita ni za siku nyingi. Kwa sasa hivi Mbogwe tuko salama. Nimeikuta Mbogwe ikiwa na mapato ya Shilingi milioni 700 lakini kwa sasa hivi tuko kwenye bajeti ya Shilingi bilioni tatu. Kwa maana hiyo, kwa kifupi sisi tulipoingia tulibainisha na tukaazimia, kipindi hicho Waziri wa *TAMISEMI* akiwa dada yangu Mheshimiwa Ummy,

anajua ripoti ile ambayo tuliazimia Baraza la Mbogwe. Kwa hiyo, nimeona nifafanue tu kwa kifupi hapo.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye asasi. Nimeangalia wanakamati wa Wizara hii pamoja na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, wameongea kwa hisia kubwa sana. Rafiki yangu wa Magu jana nilimwambia usiwe na wasiwasi tiririka tu, nami huku naandika. Kweli nilikuwa naandika kabisa maana jambo hili ni kubwa. Jambo hili tukilifumbia macho litatuharibu. Naona aibu kufa kwenye meli ambayo naona inaenda kuzama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite kushauri, nimejumlisha hasara zote nikaona Shilingi trilioni 4,590 ni fedha nyingi sana ambapo nikifanya mgao kwa halmashauri zetu 184, tunaweza kujenga barabara kwa ile Ilani yetu yenye *page 303.* Tuna uwezo wa kujenga lami za kuunganisha Mkoa na Wilaya tukamaliza hiyo ahadi tuliyoitoa kwa kila Mbunge hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zimetajwa taasisi nyingi ukianza na ukurasa wa tatu, imezungumzwa *TANESCO* kwamba ililipa Dola za Kimarekani 153.43. Uki *calculate* kwa *rate* ya leo unapata karibia Shilingi milioni 360. Ukurasa wa pili huu imeonekana Shilingi bilioni 68 ambazo zimelipwa kupitia Shirika la Serikali hii *TANROAD,* kwa hiyo, naona aibu kwanza kuendelea kuwazungumza hawa watu kwa kuwa wameshazungumziwa na watu wengi, sasa nijikite kushauri tu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile jambo hili umelileta kwetu tushauri kwa niaba ya wananchi na mjumbe hauawi, naomba kabisa uchukue hatua kikwelikweli. Najua hakuna Mbunge ambaye hataazimia kwa kitendo hiki kilichofanyika. Sisi sote humu tunapigiwa kura, kuanzia

Waheshimiwa Mawaziri, huwa wanapitia kwanza kwenye hii michakato na baadaye wanateuliwa kuwa mawaziri huko. Kwa hiyo, katika maamuzi tutakayoyaazimia kesho, naomba tuungane kwa nia moja ili Taifa letu tuweze kulibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kumvumilia mtu ambaye anakula kodi za wananchi. Nikiangalia nilikotokea jinsi wanavyolipa kodi wale wafanyabiashara wadogo, ni jambo la kusikitisha, lakini unaona hapa kuna wafanyabiashara wakubwa hawalipi kodi, wanategemea kesi zao ziishie Mahakamani na walishajua hizi sheria zetu ni dhaifu, niungane na mwenzangu Mheshimiwa Tabasam, kuna kila sababu hizi sheria kuziboresha ziseme kabisa vizuri mtu anapoonekana na makosa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nitakuwa labda nje sana, sheria hizi zinatakiwa zitaje, endapo mtu anaonekana ana makosa ya kuhujumu uchumi, pesa za watu wanyonge waliojichanga ili kuisaidia Serikali mtu akazitafuna, zitamke kunyongwa kabisa. Huyo mtu akionekana anyongwe ili watu waogope, kwa sababu sheria tulizonazo sasa hivi watu hawaogopi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshuhudia Mawaziri wengi wanapiga kelele hata kwenye miradi. Unamwona Waziri anapiga kelele kabisa kwamba hapa hela zimepigwa, zimeliwa; akitoka Waziri, watu wanaendelea kula bia. Hata mimi mwenyewe Mbunge huwa najaribu kufuatilia sana; mimi ni mkali sana kwenye jimbo langu, maana najua likiharibika nimo mimi, itakuwa ni aibu ya hatari sana. Hawa wasomi walishasoma hizi sheria wakaona zina udhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atusaidie Wabunge kwa hilo, tuziboreshe sheria zetu zizungumze vizuri. Hapa hazijazungumza vizuri kwa sasa hivi, tutakuwa tunapiga kelele tu Waheshimiwa Wabunge, mwisho tutaonekana wa ajabu, Bunge tunapigwa vita, Bunge la ajabu, halina maamuzi. Sijui tufikie maamuzi halafu watu wasichukuliwe hatua, tutakuwa wageni wa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya tumesema watu wakamatwe, hawakamatwi, tunakutana nao mitaani, wanatutukana; tuna watoto wana watoto, tufanye nini?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, mimi nalishauri Bunge…

**SPIKA:** Mheshimiwa Nikodemas Maganga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Maganga kwamba Bunge lililopita, nadhani Bunge la Kumi na Moja, tulitoa maazimio humu ndani, Waziri wa *TAMISEMI* alikuwa Mheshimiwa Jafo, tukasema sheria ile inayolinda fedha za asilimia 10 ipo wazi. Mkurugenzi wa halmashauri yoyote ambaye atakusanya fedha halafu akashindwa kutoa asilimia 10 ya nne nne mbili achukuliwe hatua hapo hapo, kwa sababu fedha zitakuwa zimeshakusanywa naye amekula hizo hela, ajifute yeye mwenyewe kwenye cheo. Alizungumza Mheshimiwa Jafo humu ndani, lakini

mpaka leo kuna Wakurugenzi mia moja na kitu wamekula hizo hela na wapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nikcodemas Maganga unapokea taarifa hiyo?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo ya baba yangu kwa mikono yote miwili. Tusifanye vitu vya kuchekesha. Huwa namwangilia Waziri Mkuu anavyofanya ziara kwenye baadhi ya Mikoa na Wilaya, yuko *serious* kweli baba wa watu, lakini kila akifanya maelekezo sijui kama wale watu huwa wanakamatwa na sijawaona sijui wako Magereza ya nani? Aliwahi kuja kwangu nikiwa bado sijawa Mbunge, nilikuwa mfanyabiashara tu, akatoa maelekezo. Alipotoka tu watu wakaanza kunywa bia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sheria zetu naomba ziseme kabisa. Kwanza zimlinde Waziri Mkuu, akisema kitu, hiyo ni Serikali, aheshimiwe, huyo ni msaidizi mkuu wa Rais. Haiwezekani kila siku tuwe tunazungumza mambo yale yale kama ndugu yangu alivyonipa taarifa. Hivi tunamaliziana heshima. Ndiyo maana watu wengine huwa wanaichukia sana siasa, maana sheria hizi hazijazungumza vizuri. Yaani Mbunge wa Tanzania ni kama mpiga debe wa stendi, ulishaona wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya maneno kwa masikitiko makubwa sana. Haiwezekani Mbunge anahangaika hapa Dodoma miezi mingi anapanga matrilioni, ukiangalia hata kwenye akaunti zao sidhani kama kuna Mbunge ana Shilingi trilioni moja kwenye akaunti yake huko. Leo ndugu zangu wa Kamati

wamezungumza kwamba kuna *KADCO,* haijulikani ni ya nani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza, Wabunge, Bunge hili liseme kabisa, kwanza kuanzia hao mliokuwa mnakaa nao kwenye kamati, waanze nao. Mii nilishawahi kushuhudia pale Kahama, anakumbuka Waziri Mkuu, mwaka 2020 kuna wafanyabiashara walikuwa wanapunguza sukari kidogo tu, tena robo kilo kila mfuko; walishughulikiwa na Mkuu wa Mkoa peke yake. Watu walikuwa na vitambi, mabilioneam wakaishi pale Magereza ya Shinyanga, *discipline* ikapatikana. Leo watu waliomo ndani ya Serikali hawakamatiki jamani! Haipo sababu sasa ya kutengeneza Serikali! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namhurumia sana mama yangu. Jana nimeona tumesamehewa kama Shilingi bilioni 31, anajitahidi sana, lakini hizi fedha kama hazina ulinzi, pamoja na misamaha hii ambayo tunapewa na Mataifa, sisi wenyewe kama hatujisimamii, siku moja haya Mataifa yatatudharau, hayatatukopesha tena fedha. Kwa sababu tutakopeshwa na tutafika sehemu tusikopesheke, kila tunachokopwa kinaliwa. Wabunge tunarudi hapa hakuna kinachozingatiwa. Mwisho wa siku watoto wetu wataambulia nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia ukurasa wangu wa pili hapa unasema mikataba sijui ilikuweje, *TANESCO* hapa, hii kampuni ya *Symbion*, hawa watu wote wakamatwe mara moja. Hili zoezi ni dogo sana, ila ukilikuza linakuwa kubwa, lakini zoezi hili linaweza likamalizwa na mtu mmoja, tena Waziri wa Mambo ya Ndani, hili suala lipo ndani ya uwezo wake. Mara moja tu akitangaza kesho waripoti Dodoma hapa, kwani shida iko wapi? Waripoti wenyewe kesho, tuone trilioni zetu zote hizi, tukajenge

barabara, tukafanye na mambo mengine, maisha yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ukomee hapo, nisije nikayarefusha sana mwishowe nitavuruga, maana nikiwa na hasira huwa nashindwa kuchangia vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pia naomba kuwashukuru wenzetu wa Kamati zote tatu kwa taarifa nzuri zilizo chambuliwa kutoka kwenye taarifa ya *CAG* ambayo imewafanya Wabunge waweze kuzisoma na kuzielewa taarifa hizi vizuri kabisa. Kwa sababu *volume* ni kubwa lakini wamefanya kazi kubwa sana wenzetu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuishukuru Serikali, mwenzangu mmoja amezungumza hapa kwamba kwa kawaida taarifa hizi huwa hatuzipati mapema, halafu tukazipitia, kuzichambua na kuzichangia. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali yetu imeamua kwa makusudi kuheshimu misingi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo mawili; eneo la kwanza ni la *PAC*, lakini eneo la pili ni *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, wamezungumza wenzetu wengi sana hapa juu ya upotevu wa fedha za Serikali. Wenzetu wamezungumza hapa kwamba *TANROAD* imetutia hasara ya Shilingi bilioni 68.7. Vile vile kwenye ujenzi wa vihenge, *NFRA* tumepoteza Dola milioni 33. Kwanza naomba hapa tuelewane. Unapozungumza Dola milioni 33 unaweza ukaona kama ni kitu kidogo hivi, lakini ukizigeuza Dola milioni 33, tunakaribia kwenye Shilingi bilioni 72 na kitu. Kwa hiyo, tusichukulie kama ni fedha ndogo, ni nyingi sana ambazo zingeweza kusaidia kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha nyingine hapa, amesema kaka yangu Mheshimiwa Maganga, kuhusu upotevu wa Dola milioni 153.4. Hizi ni fedha nyingi. Tunazungumzia karibu Shilingi bilioni 300 na kitu zimepotea na hazina maelezo. Vilevile wako wajanja hapa wengine, mwaka 2021 lilipoungua soko la Kariakoo, tumeambiwa kwamba shilingi bilioni 3.56 hazijulikani zilipo na hazina maelezo. Halafu, taarifa itoshe hivyo, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, pia tumeambiwa kwenye *DART* kuna malipo ya usumbufu. Haiwezekani kwenye Taifa hili lenye Wabunge walioteuliwa wakachaguliwa na wananchi halafu mambo yakaenda kawaida tu. Siyo Bunge hili. Bunge hili limekuja kwa asilimia kubwa na wengi hapa na wengi wetu tunasimamia Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Moja katika ahadi zake *CCM* ni kupambana na mambo ya ubadhirifu wa fedha za Umma. Bunge hili ni lazima tuchukue hatua na lazima Chama chetu kilichotutuma kijue kwamba tumekuwa wakali kwenye hili. Kwa hiyo, asiondoke mtu kama ni *business as usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kidogo kwenye *LAAC*, wenzetu wa Kamati wanasema wametuletea taarifa hii ili kutushawishi. Naomba ninukuu: "Lengo la taarifa hii ni kulishawishi Bunge liafiki ushauri wa Kamati wa kuitaka Serikali ichukue hatua."

Mheshimiwa Spika, jana ulisema hapa, ulitupa moyo sana, kwamba kuna wakati wa kushauri na wakati wa kusimamia. Sasa hivi tunataka kusimamia kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza maelekezo na maamuzi ya Bunge hili. Kwa sababu hii ni mihimili mitatu; mhimili huu ndiyo unasimamia Serikali. Kwenye hili, wenzetu wa Kamati wala msipate taabu, siyo kazi yenu kutushawishi. Mmeweka *facts* kwenye meza, zimeonekana, na hizi mmezitoa kwenye taarifa ya *CAG,* tunawashukuru na tunakubaliana na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wenzetu wamesema, naomba kidogo niipongeze Serikali kwamba angalau imefanya kazi kubwa; ukilinganisha miaka ya nyuma na ya sasa, wanasema kwamba, katika maeneo ya halmashauri zilizofanyiwa utafiti, zilizokaguliwa ni halmashauri 178 ambazo ni sawa na asilimia 96.2, hii ni hatua kubwa sana. Naomba niipongeze Serikali lakini tuendelee, kwa sababu tunahitaji mia kwa mia, kila aliyepewa pesa zetu ni lazima akaguliwe, kwa sababu hii siyo *option,* ni lazima. Kama kuna upungufu wa watenda kazi, tunaomba wenzetu Serikali wahakikishe kwamba wataalam wa ukaguzi wanafanya kazi yao, kwa sababu hao wenzetu wameona upungufu kwenye maeneo kumi.

Mheshimiwa Spika, nitataja machache tu, kwanza, anasema, ni upungufu kwenye mifumo. Mifumo inatengenezwa na kudhibitiwa na binadamu. Mifumo hii inakuwaje? Maana yake huu ni mkakati wa makusudi

kuhakikisha kwamba fedha zinapita lakini katikati wako wajanja wanazichezea. Mifumo ni ya kwetu na wataalam tunao inakuwaje kuna kuchezewa kwenye mifumo?

Mheshimiwa Spika, vile vile wanasema kwamba kuna dosari kwenye matumizi na makusanyo. Tunaweza kufanya dosari ndogo kwenye makusanyo lakini kwenye matumizi hatuwezi kusema ni dosari bali ni makusudi. Kwa sababu tunapotumia tunazo Sheria za Fedha ambazo ndizo zinazotuongoza. Tuna Sheria za *appropriation* ndizo zinazotuongoza, tunakoseakoseaje? Wenzetu wamesema hapa kwamba ni mkakati wa makusudi kwa sababu sheria zimeonekana zina upungufu, wataalaam wanazijua, wanazichezea. Kwa hiyo, ningeomba hili kwa Wabunge wenzangu tukubaliane na mapendekezo ya Kamati kwa sababu Kamati ilifanya kazi kwa niaba yetu. Sasa sisi ni wajibu wetu kama Bunge kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, anasema kuna matumizi mabaya ya shilingi bilioni 9.74, amana za halmashauri. Sasa kwenye akaunti za amana bilioni 9.74 zinapoteapoteaje? Mbona hapa Kiswahili hakieleweki? Tokea tarehe Mosi Julai mpaka tarehe 30 Juni ya kila mwaka tunapoteza kwenye akaunti hii tu bilioni 9.74 kwenye akaunti nyingine ambazo hatuna taarifa nazo inakuwaje? Kwenye hili, pamoja na kwamba wenzetu tunawakubali wanafanya kazi, lakini waongeze kasi kwenye hili. Wenzetu wanafanya kazi kwa sababu wameona kuna upungufu kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nielekee kwenye ruzuku za miradi ya maendeleo. Ukiangalia pale kwenye pesa za ruzuku zinazokuja kwenye halmashauri utagundua mambo yafuatayo na Kamati imetusaidia. Kuna halmashauri ambazo zimepewa zaidi ya asilimia 52 ya

fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge. Ukiangalia kwenye mtiririko wa jedwali lile namba moja, utakuta kwamba kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2021 kuna halmashauri zimeongezewa 52% ziada.

Mheshimiwa Spika, suala langu liko hapa, Bunge hili tunakaa miezi mitatu kwa ajili ya kupanga bajeti, kuangalia maeneo gani tupeleke, maeneo gani tupunguze, tukimaliza tunaidhinisha ziende. Kama kuna dharura ni wajibu wa Serikali kutuita Bunge hili kwamba kuna fedha za ziada. Sasa naomba wenzetu watusaidie, unawezaje kuongeza mahali 52% ziada tena sio Sh.2000/=. Kwa mfano, kwenye jedwali namba moja, utakuta ziada ni Shilingi 41.787 bilioni, nani katoa kibali hiki? Mwingine amepewa ziada ya 30% Shilingi bilioni 20, nani katoa mamlaka ya hili? Kwa sababu mamlaka inayoidhinisha fedha ni Bunge hili. Sasa nadhani wenzetu waje watusaidie hapa, kwa sababu kwa kawaida kama kuna bajeti ya ziada ni Bunge hili ndilo linaloombwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi pale, nilisema kama Mabunge mawili yaliyopita hivi, kwamba tunalo tatizo kwenye sheria zetu na nilishauri na naomba niendelee kushauri kwamba, Bunge hili bado halijafanya kazi yake. Kuna kitu kinaitwa *Appropriation Committee,* Kamati hii ndio inatakiwa ifanye kazi mkono kwa mkono na Serikali ili kile kinachokusanywa kipelekwe kwa maelekezo ya Bunge hili si vinginevyo. Hatuwezi tunakutana hapa tunapanga, tunaamua, halafu mwingine kwa matashi yake tu anaamua wakati Bunge lipo na linaweza kuitwa wakati wote kama kuna dharura likafanya maaamuzi. Halafu mmoja anamua kwa sababu sheria zina nafasi, zinamruhusu au sisi kama Wabunge hatujaamua kufanya kazi kama wabunge?

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 11 kuna vitu vidogo sana, ukivisoma unaviona ni vyepesi sana. Anasema, ununuzi bila idhini ya bodi zinazohusika. Bodi za zabuni, watu wametumia shilingi bilioni 7.9, tuko wapi? Bunge liko wapi? Hao wenzetu wa Serikali wako wapi? Fedha hizi zinapotea mpaka tunakuja kuletewa taaarifa na CAG sisi kazi yetu nini?

Mheshimiwa Spika, ununuzi usiozingatia mpango wa manunuzi. Tumepoteza shilingi bilioni 3.84 kwenye halmashauri 24. Hii ni aibu kwetu. Narudia ni sisi kama Bunge hatujafanya wajibu wetu, ndio maana watu wanaona Bunge liko legelege, kwa hiyo wanaweza wakalichezea tu. Hili sio Bunge legelege. Hili ni Bunge ambalo likiamua kufanya maamuzi linafanya. Kwa hiyo ningeomba tufanye maamuzi ili kila mtu akae kwenye mstari wake.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kuna mtu mmoja anasema amelipa malipo ya ununuzi bila ya kuzingatia taarifa za mapokezi. Huyu amepoteza shilingi bilioni 2.02.

Mheshimiwa Spika, naona tabu hata kutaja hizi namba kwa sababu ni kama vile unajichoma kisu. Maana yake ni dhambi yetu sisi kama Wabunge. Sasa ningeomba niseme haya kwa sababu ni mengi sana. Kule kwetu Waswahili husema *mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe*. Sisi hapa wengi wetu tumeletwa kwa heshima na kibali cha Chama Cha Mapinduzi lazima tukithibitishie Chama chetu kwa sababu Serikali ina wenyewe. Wenye Serikali hii naomba niseme kwa sasa ni Chama Cha Mapinduzi. Haitozidi mwezi mmoja tutakwenda kuulizwa pale mlitusaidiaje kama Chama cha Mapinduzi kuisimamia Serikali? Kwa sababu Serikali ni ya kwetu na chama kimetuingiza kwenye Bunge hili ili

tuisimamie Serikali. Sasa ningeomba kushauri haya yafuatayo; pamoja na mengine waliyoshauri wenzangu nakubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, kwenye *PAC* na *LAAC;* ningeomba tuhakikishe kwamba uchunguzi wa kina unafanyika ili kila aliyehusika abebe msalaba wake.

Mheshimiwa Spika, kwenye manunuzi, waliohusika sheria zitumike kwa sababu hawa ni watendaji wetu. Sheria zipo wanazijua, kanuni zipo wanazijua lakini kwa sababu wanajua *loophole* za sheria, wanafanya wanavyotaka. Kwenye hili naomba sheria, kanuni na taratibu kwa watumishi hawa zifanye kazi wala tusioneane huruma.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningeomba tupitie upya Sheria ya Manunuzi inayoonekana ni dudu lisilowezekana. Sheria ya Manunuzi inatuumiza sana. Kama mtakumbuka miaka michache nyuma, alikuwepo Rais wetu aliyetangulia, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alisema Sheria za Manunuzi zina mapungufu mengi, mtu anaweza akafanya mazuri lakini sheria ikamkamata kwa sababu hakufuata taratibu na mtu anaweza akafanya madudu lakini kafuata sheria, huyo anaweza akawa *free*. Naomba tupitie sheria zetu za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Philip Mwanyika na Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia

hoja zilizopo mezani. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja zote zilizopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze zaidi kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hasa katika Bodi ya Mikopo. Mwalimu Nyerere alitueleza kwamba maadui wakubwa kabisa katika nchi hii ilikuwa kwanza, ni ujinga na wengine wakafuata. Akaweka mifumo ya kufuta huu ujinga kwa maana ya kumtokomeza kabisa huyu adui. Pia Mwenye hekima mmoja Jeff Rich alisema:

"*If you think education is expensive, then try ignorance*"

Mheshimiwa Spika, anamaanisha, kama unafikiri elimu ni gharama, basi jaribu ujinga. Kwa muktadha huo tunamshukuru sana Rais Wetu Mama Samia Suluhu Hassan ambaye amejipambanua vizuri kabisa kuhakikisha kwamba anaondoa ujinga katika nchi hii. Tumeona mwaka jana alianza kutoa fedha nyingi ili kujenga madarasa ili Watanzania wengi wapate fursa ya kwenda kusoma na kuweza kufuta ujinga. Hata hivyo mwaka huu tena tumeona bilioni 160 zimetolewa ili madarasa 8,000 yakejengwe ili Watanzania wakaweze kusoma. Tunamshukuru zaidi kwenye kuongezea fedha kwenye Bodi ya Mkopo mpaka kufikia bilioni 570. Kwa kweli anajitahidi na anafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya CAG inaonesha kwamba kwa kipindi cha miaka mitano ambacho amefanya ukaguzi ni 72% tu ya wanaostahili kupata mikopo ndio wamekuwa wakipata mikopo. Pia imeonesha kuna wanafunzi 492 ambao wao walishindwa kuendelea na masomo kwa sababu walishindwa kupata

mikopo hali ya kuwa wao ni watoto wanaotoka kwenye familia maskini. Hivyo walishindwa kuendelea kusoma.

Mheshimiwa Spika, inaonesha vile vile kuna kiasi cha fedha Sh,1,768,000,000 ambapo katika mwaka 2017/2018 wanafunzi wapatao 5,650 walipokea mikopo ambayo hawakustahili. Tena aliendelea kutaja kwamba kumekuwa na changamoto kubwa kwamba mifumo haisomani. Wanafunzi wanapata shida wanapokwenda kuomba ili wapate mikopo. Kwa mifumo kutoka Baraza la Mitihani ukiangalia pia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini pamoja na Mamlaka ya Usajili wa Vitambulisho vya Taifa, hii mifumo haisomani. Kwa hiyo, kumekuwa na changamoto kubwa kwa wanafunzi kupata shida katika kuomba waweze kupata nafasi ya kupewa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, imeoneshwa pia kwamba Bodi kwa muda mrefu kwa kipindi hiki cha miaka mitano imekuwa ikitoa kiwango cha chini cha mikopo kwa kila anayekuwa akiomba. Pia kwa kiwango cha juu kwa kati ya Sh.3,100,000/= kwa wanafunzi kati ya 896, zote hizi ni chanagamoto ambazo *CAG* amezionesha. Hizi ni chanagamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa imeonesha katika kipindi cha mwaka 2018/2019, kuna wanafunzi wapatao 6,183 ambao walipangiwa mikopo kwa kiwango cha juu zaidi ya vile walivyostahili ambapo kiasi cha Sh.5,668,843,000/= kilitumika, lakini pia kuna wanafunzi 2,852 walipata kiwango cha chini cha uhitaji wa mkopo kiasi cha Sh.1,147,000,000/=. Kwa hiyo kunaonekana kwamba kuna fedha nyingi ambazo zimekuwa zikitolewa nje ya utaratibu. Kwa hiyo kwa miaka mitano inaonesha kwamba kuna jumla ya Shilingi bilioni 13.7 ambazo zimetolewa kwa watu ambao hawakustahili, ambapo

kiasi hiki kingeweza kutosheleza wanafunzi ambao walipata mikopo ya chini kama 10,075 ambapo pia kingeweza kulipia wanafunzi wengine wapya ambao waliomba kama 3001. Kwa kweli changamoto ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuchukua kipande hiki kwa sababu nimekuwa nikipokea malalamiko mengi ya watoto ambao hawana uwezo, maskini kutoka katika Jimbo langu la Kalenga na majimbo mengine ambao wamekuwa hawapati mikopo kwa kukosa umakini kwa hawa wenzetu ambao tumewapa dhamana.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi katika kipindi hicho cha miaka mitano, umeonesha kuna wanafunzi 756 ambao waliostahili kupata mikopo lakini hawakupata. Ni mambo mengi yamekuwa yakiendelea. Vile vile tunaoneshwa kuwa kuna ambao walistahili kupata mikopo kiasi cha 192,039 lakini ambapo walitakiwa wapate kiasi cha Sh.569,313,000,000/=, sasa hili sio tatizo la watu wa Bodi ya Mikopo kwa sababu ni uwezo wa Serikali kuwapa hiyo mikopo ulikuwa mdogo kwenye hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, tumeona sheria na miongozo katika Bodi ya Mikopo ambayo inawataka wanafunzi ambao wako katika uhitaji wa juu wa mikopo, kwa mfano, wale ambao wanatokana na kaya maskini ambao wanatakiwa wapewe mikopo, kiasi cha wanafunzi 22 hawakupata mikopo hiyo. Hii ni kati ya kipindi cha miaka miwili 2019/2020 na 2020/2021 kiasi cha Sh.84,000,000 zilitakiwa zitolewe lakini hazikutolewa. Pia inaonesha kuna watoto 95 ambao wanatoka katika zile familia za yatima (baba na mama wamefariki) na mwongozo unaonesha kwamba ni lazima wapewe, lakini hawakupewa. Walipoulizwa wanasema kwamba, mfumo hautambui kwamba wale watoto wanaotoka

familia maskini au yatima ndio wanaotakiwa kupewa kwanza. Hayo ndiyo majibu ambayo bodi iliyatoa. Hii nayo tunaiona ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo bodi wamekuwa wakiipata ni kwamba, wakishapeleka fedha kwenye taasisi zile za juu kwamba kuna wanafunzi 100 katika pengine Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walitakiwa kupewa mkopo, bodi inapeleka, ikishapeleka kule, wale wanafunzi wasipopewa ndani ya siku 30 mwongozo unasema zile fedha zinatakiwa zirudi kwenye Taasisi ya Bodi ya Mikopo ili waendelee kuwakopesha wengine. Sasa imetokea tatizo kwamba kumekuwa na ucheleweshaji. Kwamba hawarudishi kwa wakati ndani ya siku zile 30, kwa hiyo, kunainyima furs ana uwezo Bodi ya Mikopo kuendelea kukopesha wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja na mapendekezo kulingana na yale ambayo nimeyaona, niombe wenzangu wa Kamati, najua walikuja na mapendekezo yao, naomba wapokee na hii nyongeza ya mapendekezo ambayo nimeona kutokana na kile ambacho nimekisoma kutoka kwenye Taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kwanza, niombe taasisi zote ambazo zinahusiana na usajili wa wanafunzi yaani mifumo yake iweze kusomana. Nikimaanisha Bodi ya Mikopo, Vitambulisho vya Taifa pamoja na Usajili, Ufilisi na Udhamini mifumo yake isomeke ili iwe rahisi kuondoa matatizo yanayotokana na *forgery*. Pia bodi ihakikishe wale wanaopewa mikopo ni wale wanaostahili kupewa mikopo kama wale watoto maskini kutoka katika kaya zile zinazohudumiwa na Serikali, watoto yatima, ihakikishe kwamba wanapewa. Wanachotakiwa kufanya ni kubuni tu mbinu za namna gani ya kuwasaidia, wanaweza

wakawa pengine na dawati maalum la kuweza kuwasaidia hawa, kama mfumo hauwatambui, basi waweze kuandaa dawati maalum la kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, pia tufanye tafiti kuona nchi nyingine zinafanya nini kusaidia Bodi hizi za Mikopo na taasisi nyingine ambazo zinasaidia watoto kusoma, kuona vyanzo vyake vinatoka wapi ili tutafute vyanzo vingine, lakini tunaweza kujifunza kutoka nchi nyingine. Pia taasisi za elimu ya juu kwa maana ya vyuo vikuu zihakikishe kwamba wanafuata mwongozo wa Bodi ya Mikopo kwa maana kwamba zile fedha ambazo hazijaenda kwa wanafunzi waliotakiwa kupewa na hawakupewa ndani ya siku zile 30 basi zirudishwe ndani ya wakati kama mwongozo unavyosema, ndani ya siku 30.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine, naomba uchunguzi ufanyike kulingana na haya makosa ambayo yameainishwa ni mengi mno. Uchunguzi ufanyike ili waone kama ilikuwa ni maksudi ya kuibia Serikali ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa haraka. Pia kuwe na kitengo maalum kama huduma kwa wateja cha kusaidia kupokea na kutoa ufafanuzi pamoja na kutatua changamoto kwa wakati ambazo zinaikabili Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kwamba TAKUKURU watumie hii ripoti ya CAG kuhakikisha kwamba wanafuatilia na kuhoji hizi Taasisi za Serikali Bodi ya Mikopo ikiwa mojawapo na nyingine ambazo zimetajwa na kazi yao iwe ya muda mfupi kwa sababu wamerahisishiwa. Suala la TAKUKURU kuchukua miaka miwili miaka mitatu, wakati taarifa hizo wameshatafuniwa hiyo inatia mashaka, kwamba inaweza ikawa kuna

*coalition* pia hata huko ndani ya TAKUKURU pia kwa sababu nao pia ni binadamu.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tuombe kwamba ripoti hii waifanyie kazi kwa muda mfupi, hatutaki kusikia miaka miwili miaka mitatu, unachunguza nini wakati tayari umeshatafuniwa. Kwa hiyo, naomba TAKUKURU hili walifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi niliomba nichangie hayo kwa uchache, ni eneo hilo moja tu, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae. Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia kwenye taarifa hizi za Kamati ambazo zimewasilishwa kwetu Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Ni Mwanamama jasiri na shupavu kweli kweli! Na hii ni namna ambavyo miradi inaweza kutekelezwa katika maeneo yetu, nasi tumekuwa mashahidi hasa fedha za miradi zinavyokuja kwa wingi kwenye maeneo yetu kwenye Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona fedha hizi zinavyokuja kwa wingi na taarifa ilivyokuja hapa, hii ni taarifa ambayo imewasilishwa na kamati inaonesha taarifa ya mwaka 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 na tumeona madudu yaliyomo ndani ya taarifa hizi. Ni fedha nyingi sana ambazo zimeonekana kupotea na sijajua mwarobaini wake hasa ni nini? Hasa katika nchi zetu za kiafrika na sijajua labda ndiyo tumeumbwa tuwe hivyo sijaelewa, maana yake kila anayeweza kupata fursa ya kufanya kazi katika eneo lazima aongeze yeye anapata nini, hata kama kuna mshahara ambao utamwambia auchague yeye mwenyewe utamlipa Shilingi ngapi, lakini kwenye akili zetu tunaongeza ninapataje fursa ya kuiba zaidi ya hiki ambacho napatana na huyu mtu. Kwa hiyo, imekuwa ni dhana ambayo ipo, nafikiria hata mfumo wetu wa elimu kila siku tunataka tuungalie upya kuanzia chini *nursery* huko kuja Sekondari mpaka Vyuo Vikuu. Hata mtu anayesomea fani mbalimbali anasoma lakini anawaza akipata fursa abutue, akipata fursa achukue chake, sasa hii imekuwa ni gonjwa kubwa sana, ugonjwa si wa Taifa ni ugonjwa wa Afrika nzima, ndiyo maana maendeleo yanachelewa sana unaweza kushangaa nchi tulizopata uhuru miaka ya 1960 za Asia na ukichukua nchi za Afrika zilizopata uhuru miaka ya 1960 na maendeleo yaliyokuwepo kwa kipindi hicho na ukiangalia maendeleo yaliyopo sasa hivi ni vitu viwili tofauti kabisa, ni kama vile wenzetu waliwahi zamani kupata uhuru kuliko sisi, kumbe nadhani kuna mahali tumekosea ni lazima tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG kila mahala ni wizi, hata ukisoma taarifa ya ukaguzi wa Halmashauri zetu, unaona kuna *POS* ambazo zipo zenye namba za kufanana. *POS* za kukusanyia mapato, sasa mpaka *POS* zenyewe kwenye Halmashauri ziko zaidi ya 100 zina

namba moja zinafanana maana yake nini hapa? Usajili wake na taarifa zake maana yake kuna wizi wa fedha za Serikali za wananchi zinapotea kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii inatupeleka kurudi nyuma, kama tunaweza tu kukuta kwa miaka hii tumepoteza kwa fedha hizi karibu Trilioni Nne, bajeti yetu kwa mapato yetu ya ndani ni Trilioni 20 kwa mwaka, Je, ni miradi mingapi ambayo fedha hizi zingedhibitiwa tungeweza kupiga hatua kubwa kama Taifa? Sasa iko haja ya kuangalia pamoja na kuwa tunachangia, tunaonesha maeneo na kumekuwepo na watumishi wanahamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, imekuwa kama desturi, kasumba na kama tabia yetu.

*Mheshimiwa Spika, tufike hatua tubadilike, wenzetu China ukikutwa na hatia ya kukamatwa na rushwa unanyongwa, wengine wanapigwa risasi unauawa, sisi huku tuna roho za kibinadamu, aah! muache, msamehe, sheria iko wazi lakini hatua hazichukuliwi, hizo ni sheria za nchi za watu. (Makofi)* **[Neno China Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, hiyo habari ya China hapo kwenye mchango wako hebu iondoe wewe mwenyewe halafu uendelee kumalizia hoja yako.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naondoa neno '*China*' ni nchi zingine hatua kama hizo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nchi yetu tunawalea hawa watu na tuko zaidi ya milioni 61. Ukiangalia idadi ya wasomi sasa hivi Watanzania imekuwa ni kubwa, kwa nini kusiwe na utaratibu wa hawa wanaokosea, hata wale

vyeti vyao vinaingia kwenye dosari na kuondolewa kazini, hata kama akienda kuomba tena nafasi nyingine ndani ya Serikali, alama inakuwepo ya kum-*identify* kwamba huyo alishawahi kuharibu sehemu fulani hapaswi kupewa nafasi tena sehemu nyingine. Hasa hii ya kumhamisha, ameharibu Igunga unampeleka Musoma, anaharibu Musoma unampeleka Dar es Salaam, anaharibu Dar es Salaam *as if* nchi hii haina wasomi, tunao wasomi wengi?

Mheshimiwa Spika, ifike mahala mtu anapoharibu na kazi yake inakuwa imekoma hapohapo, siyo hadithi ya kusema unamhamisha akajirekebishe sehemu nyingine, kama tu mwizi wa kuku anapelekwa mahakamani, kuku ni shilingi ngapi? Kuku ananunuliwa shilingi ngapi? Shilingi 5,000, shilingi 7,000 mtu anaenda kuhukumiwa miezi Sita. Leo ni mabilioni ya fedha kwenye ripoti za *CAG* yamepotea, yanapotea au yataendelea kupotea lakini je adhabu wanazozipata hawa watu zinafanana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nikuambie Wabunge tunalalamika hapa lakini wananchi wanaenda kuwalaumu akina nani? Atalaumiwa Rais, atalaumiwa Waziri, atalaumiwa Mbunge, atalaumiwa Diwani, lakini wezi wapo kwenye mfumo na Mbunge ataondoka atakuja Mbunge mwingine, Rais ataondoka atakuja Rais mwingine, Waziri ataondoka atakuja Waziri mwingine, mfumo bado unawabeba wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wezi wanahama *phase* tu wanatoka *phase* ya Mheshimiwa Jakaya anakuja *phase* ya Mheshimiwa Hayati Magufuli, mwizi yupo tu, anatoka mwizi huyo *phase* ya Hayati Magufuli anaingia Mheshimiwa Mama Samia mwizi yupo tu anaendelea kwenye mfumo, anaendelea kunyonya Taifa. Kwa nini

huu mfumo tusiufumue uende sawa? Kama tunatumbuliwa na wananchi wakati wa kura, kwa nini na sisi tusiwatumbue hawa watu kwenye ajira zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike hatua tuwaonee huruma Watanzania, fedha hizi zilizoainishwa humu na Kamati imechambua kwa kina, kuna haja gani ya kukaa tunabembelezana kwamba huyu mtu tumuache aende sehemu nyingine, umeshaharibu hata kama ni kidogo umeharibu pisha kazi aingie mtu mwingine italeta heshima. Hizi taarifa za *CAG* zitapungua kuja na makosa makubwa ambayo leo tunayaona. Kila siku hasara inaongezeka hazipungui yaani taarifa za fedha zinazokuja kutokana na hasara kutokana na fedha zinazopelekwa kwenye miradi na zinazopotea hazipungui bali zinaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ilikuwa Trilioni Mbili, mwaka huu utaambiwa ilikuwa Trilioni Sita, mwakani itakuja Trilioni 15, ndiyo tunakusanya tunafanikiwa kukusanya lakini bado mianya ya kupotea kwa fedha zetu umekuwa ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewasikiliza Wabunge wenzangu hapa kila mmoja analia, zimezungumzwa zile taasisi, zimezungumzwa Halmashauri zimetajwa na majina; Je, hatua tunazoenda kuzichukua zinaenda sambamba na taarifa zilizoletwa humu ndani? Ifike hatua wakati mwingine walikuwa wanawajibishwa Mawaziri hapa, lakini ndiyo *solution* kwa sababu bado hata ukimwondoa anayekuja mfumo ule wa wizi upo tu unaendelea, kwa hiyo lazima tuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Sheria ya Manunuzi ya Umma, hii Sheria imekuwa tunailalamikia kila

siku tunasema inashida, alikuwepo Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli alizungumza sana juu ya Sheria hii ya Manunuzi, amekuja Mheshimiwa Mama Samia anazungumza juu ya hii Sheria ya Manunuzi, hivi kuna ugumu gani hii Sheria kuletwa humu Bungeni tukaibadilisha? Tumekwama wapi? Ni nani ambaye anatakiwa ailete hii Sheria humu ndani tuiboreshe? Maana imekuwa ndiyo gonjwa na limekuwa eneo ambako majizi yamejificha huko, sasa tumekwama wapi?

Mheshimiwa Spika, nafikiri katika maazimio yetu moja wapo iwe katika kuboresha hii Sheria ya Manunuzi ya Umma, inawezekana tukiboresha hii italeta ufanisi wa miradi yetu lakini ufanisi wa mapato yetu na matumizi yetu ya fedha ambazo tunazipeleka kwenye miradi mbalimbali. Inashindikana vipi hii sheria kuletwa hapa, imefeli wapi mbona sheria zingine tunazibadilisha? Mara ngapi tunabadilisha sheria hapa? Lakini hii Sheria ya Manunuzi sijaelewa sijui kuna jini gani anashindwa kuletwa hapa! Tunaomba hiyo Sheria ya Manunuzi ile tuibadilishe kwa sababu ni kichaka cha watu kula fedha za Serikali au fedha za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha zinazopotea hizo mbichi kwenye Halmashauri ni jambo ambalo lipo kila maeneo, ukikagua leo utakuta, hata ukija kukagua kesho utakuta, hata sisi pale Igunga hivyohivyo fedha zinaliwa na ushahidi upo! Lakini sasa ndiyo mwisho wa siku taarifa inasomwa inaendelea na mwakani, rekebisheni, wanarekebishaje wakati tayari wanakuwa wameshaiba, yaani unamwambia mtu arekebishe au unamwambia haya rudisha taratibu, kama vile kuna mapatano kati ya mwizi na anayeibiwa, tumekubaliana turekebishe zimeshaonekana kumepotea fedha hatua zichukuliwe tu, hamna sababu ya kusema

eti kwamba mnatakiwa mzifute hizi, maana yake kuna kufuta hati chafu, au kusafisha hati chafu au kurekebisha yale maazimio ambayo yametolewa aidha na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, hata hili la Mwenyekiti wa Halmashauri kusaini *document* au mikataba na lenyewe lina ukakasi. Ni kweli Mwenyekiti wa Halmashauri ndiye mwangalizi, sasa akiingia kwenye utendaji inaleta mgongano wa kimaslahi, hili lazima tuliangalie kwa mapana yake lakini kuunda Bodi kwa ajili ya kusimamia *management* tena kusimamia itakuwa ni mzigo mwingine, hizo fedha tunazitoa wapi kwa sababu mnaangalia tu fedha za kuwalipa Madiwani, fedha za kulipa posho ya vikao za Madiwani hazipatikani lakini tukienda kuunda tena Bodi nyingine naona kama tunaongeza mzigo Zaidi.

Mheshimiwa Spika, tutengeneze njia ya kuboresha Sekretariati zetu za Mikoa katika kusimamia hii mikataba yetu katika *level* za Halmashauri, katika miradi yetu ya kwenye maeneo, lakini Mwenyekiti wa Halmshauri kusaini mikataba ya kazi za Halmashauri hii ni *conflict of interest,* mimi nashauri Mwenyekiti wa Halmashauri kama ni Sheria iletwe humu Bungeni tuirekebishe, Mwenyekiti wa Halmashauri aondoke kwenye sehemu ya kusaini mikataba ya kazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya nchini, pia kwa jambo kubwa ambalo juzi amezindua la kuhakikisha kwamba anaendelea na kazi ya kumtua Mama kuni kichwani, amekaribia kumaliza ndoo kichwani sasa anaendelea kuni kichwani ili akina Mama na akina Baba watumie Nishati safi kwa ajili ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba nikupongeze sana wewe mwenyewe hasa kwa mjadala huu wa ripoti hizi za ukaguzi kwa kweli umeonyesha umadhubuti na nikiangalia michango inayotokea hapa mikali mikali sijaona ukisema wewe kaa chini, wote waseme kadri wanavyoweza, tunakupongeza sana na sisi tupo na wewe kwa sababu tunajua hili ndio jukumu lako kubwa la msingi kuhakikisha kwamba unalinda maslahi ya watanzania kupitia rasilimali zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza michango ya wenzangu mingi, kama kawaida yangu huwa napenda kukaa upande tofauti kidogo kama kioo. Sasa nikianzia na suala hili la *TANROADS* kufikia malipo ya Bilioni 68. Kwa ajili ya riba kwa makandarasi, nikasema sawa ni *TANROADS* wamefanya hivyo lakini kitovu cha suala hilo kiko wapi? Kitu gani kinasababisha wanashindwa kuwalipa hawa makandarasi kwa wakati? Kwa sababu ni lazima tukubali pia upande wa ufanyaji kazi, mtu yeyote yule anayefanya kazi yako na wewe akishakugundua kwamba huna tabia ya kulipa kwa wakati anajilinda, kujilinda anaweka kipengele kwamba ukichelewa kunilipa itabidi na mimi nipate riba kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninachouliza, kwa sababu kama ni barabara ili zitangazwe ina maana tunakuwa tumeshatenga bajeti kwa ajili ya kazi hiyo, kitu gani kinasababisha hatulipi kwa wakati? Ni *TANROADS* wanakuwa na fedha hawataki kulipa? Au hizo fedha wanazipata kutoka maeneo mengine kiasi kwamba yale maeneo hayawapatii fedha kwa wakati? Kwa hiyo, nataka hili tunapotibu tutibu mstari wote mpaka mwisho tupate jambo ambalo ni la uhakika badala ya kuanzia na sehemu tu iliyotokea tatizo tukaacha mzizi ulikoanzia. Kwa hiyo, nadhani hata watu wa Hazina wanalo la kuzungumza hapa kwa maana Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, suala la pili napenda kuzungumzia hizi Halmashauri zetu. Kuna Halmashauri za matajiri na Halmashauri za makabwela, mimi binafsi natoka kwenye Halmashauri za makabwela ambayo kipato chao ni kidogo sana kutokana na makusanyo yao. Sasa kuna hili suala la kula fedha mbichi, siungani kabisa na Halmashauri katika suala la kula fedha mbichi, lakini yawezekana kichochezi cha kula fedha mbichi ni pamoja na mifumo yetu wenyewe tulivyojiwekea. Kwa sababu, kwa mfano tukimaliza kujadili Bajeti yetu mwezi Juni, tunapoingia mwezi Julai mpaka mifumo kuweza kufunguka na kuruhusu Halmashauri kuanza kutumia fedha inachukua muda mrefu wakati mwingine mpaka miezi miwili mifumo haijafunguka.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna Sheria zinagongana ukipata msiba wa mtumishi inabidi umsafirishe, umzike, kwa kutumia taratibu zilizowekwa kwenye Sheria. Wakati huo hakuna fedha, Mkurugenzi unategemea atachukua fedha za mfukoni mwake? Ataenda kula hela mbichi kwa kutumia wale watu wake ili mradi aweze kwenda kuzika. Kwa hiyo, nadhani pia na taratibu hizo za kuchelewesha

kufungua mifumo ziangaliwe au Halmashauri ziwekewe fedha kidogo za kutumia wakati mifumo hiyo inaendelea labda na taratibu za kiuhasibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia suala la Kamati katika ukurasa wa romani ya pili ya *summary* yao ambayo imeshauri kwamba Serikali iongeze mtaji kwa Mashirika kama *TANESCO, TPDC* na *STAMICO,* hilo ninawapongeza sana wameliona, hatuwezi kwenda tunalalamika tu lazima tena tushauri na mambo mengine ambayo yanafanya haya mashirika yetu tunayoyategemea yafanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *TANESCO* na *TPDC* ni ndugu hawa, wako katika Kamati moja ya Nishati na Madini, lakini unakuta huyu *TANESCO* kwa sababu anawajibu wa kuhakikisha umeme unapatikana anamkopa ndugu yake *TPDC*. *TPDC* naye kwa kuogopa kwamba nitasema nini kwa sababu anategemea ruzuku kutoka Serikalini anaruhusu madeni ya kukopwa na *TANESCO,* kwa hiyo unakuta ni Shirika moja linamtafuna mwenzake lakini wote wanatekeleza majukumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mazingira kama hayo iko haja wakati mwingine tunapoona ukweli na hali halisi Serikali yenyewe ichukue hayo madeni, deni kama la *TPDC* ichukue yenyewe halafu ile fedha ambayo inalipwa kidogo kidogo na Shirika kama la *TANESCO* ilipwe Hazina baada ya Hazina kuwa imeshachukua deni lake na imeshamrejeshea *TPDC* fedha zake ili iweze kuendelea na shughuli zake zinazohitajika hasa za kiutafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tunayo changamoto kubwa ya kuhama kutoka kwenye nishati ambayo inaitwa nishati isiyosafi kwenda kwenye nishati safi. Tunategemea utafiti mwingi ufanyike, tunategemea mambo makubwa ya haraka ya kuhakikisha kwamba tunasonga mbele kiteknolojia na kiujuzi kwa ujumla yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa unakuta Mashirika kama *TPDC, TANESCO* na *STAMICO* wanakosa fedha za kutosha. Kwa mfano, ukiangalia kazi za *STAMICO;* na hapa niwapongeze kwa kutimiza miaka 50 tangu kuanzishwa kwao; wanatakiwa kufanya tafiti mbalimbali kwenye nchi. Maeneo mengine hata hayafikiki kiurahisi, hakuna barabara, kwenye misitu, tunajua kuna rasilimali kama za madini, lakini vifaa wanavyotumia ni duni sana; magari sehemu nyingine hayafiki. Walitakiwa watumie hata ndege au helikopta ziwafikishe huko wafanye kazi za utafiti, lakini unakuta hakuna, kwa hiyo tunazungumzia kugawana gawana kilichopo. Tujipange sasa ili tuweze kupata fedha za kutosha ili taifa liweze kupanga matumizi yake bila kutegemea sana mikopo.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo mimi naungana na Kamati iliyopendekezwa kwamba haya mashirika matatu ya kimkakati waongezewe fedha ili waweze kutimiza wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine ambalo limezungumziwa, mradi wetu mkubwa sana wa maji wa Mwalimu Nyerere. Mimi nimeamua kuwa balozi wa kujitegemea kwa mradi ule. Nasema hivyo kwa sababu mradi ule Watanzania wote wanauangalia. Mradi ule wote tunajua kwamba tukifanikiwa Tanzania itakuwa imepiga hatua, itakuwa pia imeshiriki kikamilifu katika

kupunguza nishati zinazochangia hewa ukaa na kuwa kwenye nishati safi.

Mheshimiwa Spika, Mradi ule mashine yake moja itakayowashwa ambayo itakuwa inatowa *mega watt* 235, haifanani hata na mashine nyingine zote zinazozalisha maji katika nchi hii. Mradi ule kweli umechelewa lakini unakwenda vizuri; na hivyo nataka Watanzania waelewe hivyo, mama Samia amejitahidi. Hata leo Marehemu Mzee Magufuli angefufuka angemkumbatia dada yake mama Samia, kwamba kazi umeiweza, kazi inaendelea, mradi unaenda vizuri. Sasa, katika kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli kuna mmoja wapo lazima akubali lazima kasababisha, sababu ni nini? Na hiyo hatuwezi tukafumba macho, kumbana aliyehusika katiaka kuchelewesha. Hata hivyo tunasema ni bora kuchelewa lakini tupate kazi iliyo sahihi, kwa sababu ule mradi ni *very sensitive*. Sasa, nilikuwa nasikia hapa kwa nini watoe riba kwa ajili ya kulipa fedha hizo za dola; lakini jamani si ni jambo la kawaida? Hivi leo wewe ukienda kununua dola yako *exchange rate* kama ni shilingi 2,000 kesho ukaikuta 2,500 utaipata dola kwa shilingi 2,000? Ni jambo lipo. Kwa hiyo mimi najaribu kusema tu kwamba sisemi ufanyike ubadhilifu, isipokuwa sitaki sisi Wabunge tuishi kama mambumbumbu wa kusema dola ukiinunua jana lazima leo itakuwa bei ile ile, tutakuwa hatujitendei haki, lazima tuwe wakweli kwatika haya tunayoshauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba katika hilo hakuna ambaye atakuwa mzembe, aseme kwamba hela yake basi yeye alipwe kwa hasara, hilo jambo halipo jamani, tuambizane ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa misingi hiyo tunapozungumzia kuchukua hatua, kwa maeneo yale ambayo tunasema kwamba yamekuwa na ubadhilifu, basi tuhakikishe uchunguzi wa kina unafanyika na wale wanaostahili wachukuliwe hatua; na si tu kusema halafu tukamgusa ambaye hausiki. Nasema hivyo kwa sababu nimesikiliza michango hii tangu mwanzo, wengi wao wanaongea kwa ujumla jumla, angalau mmoja aligusa akashauri kwamba labda pengine Katibu Mkuu wa Wizara fulani, lakini wengi wanasema tuchukue hatua kwa ujumla jumla. Kwa ujumla jumla tunamchukulia hatua nani?

Mheshimiwa Spika, Kamati mnaficha nini kutuambia ni fulani na fulani? Kwa nini tunaenda kijumla jumla? Tunamwaogopa nani? Kama hatuwezi kusimama tukasema ni fulani na fulani wamehususika basi tusiseme haya ya kujaribu tu kuzungumza kwamba Wabunge tumesema, hapana. Hapa tungekuwa sasa hivi tunazungumza kauli moja, kwamba katika hawa wote safari hii hapana, lazima tuchukue hatua. Lakini sasa kwa sababu tunaongea kwa ujumla tutajikuta kwamba tumeongea tunatoka, hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naungana na wanaosema ikiwezekana uunde Kamati Teule ifuatilie kwa kina katika yale maeneo ambayo yamezidi ubadhilifu, ikiwemo hiyo *KADCO* na maeneo mengine ili tuchukue hatua ya ukweli bila kusingizia na bila uoga, haki haina uwoga. Ahsante sana

**SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya hebu tusaidie, hapo kwenye jumla jumla ndio sijaelewa hapo. Kwenye, kwamba Wabunge walikuwa wanachangia jumla jumla, hebu fafanua kidogo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ingekuwa ni mimi ninaposema tuchukue hatua; kwa mfano kwa Shirika kama *TANESCO*, nitasema kabisa. Katika eneo hili ubadhilifu umefanyika *either* na Mkurugenzi au na Mhandisi fulani au timu fulani ambayo yenyewe inajulikana kabisa ilihusika na hiyo kazi yaani nisingefichaficha. Ili tunapoenda kushughulikia sasa wa kuwaadhibu tunawapa. Sasa *CAG* taarifa yake haijamtaja mtu, unakuta huku hivyo hivyo na sisi tunachangia vilevile, lakini ubadhilifu unaonekana. Sasa, mimi naona kidogo hiyo inaleta uzito namna ya kushughulikia hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Sawa, sasa Waheshimiwa Wabunge, kesho tunaenda kutoa maazimio. Hizi taarifa, sijui, nataka kuamini kwamba watu wote mliochangia hapa mmezisoma. Ukisema hati imepatikana mbaya wilaya fulani na ni ya mwaka 2020/2021 waliokuwepo hapo si wanajulikana? Ama ni mpaka tuseme Mhandisi Manyanya ndo alikuwa *DC* ama tuseme Mheshimiwa Kuchauka ndiyo alikuwa Mkurugenzi, ndio itakuwa imeeleweka vizuri? Nadhani Serikali tutakapo kuwa tunatoa maazimio kesho zile taarifa ninyi mnazo, Rais mwenyewe alikabidhiwa. Kwa hiyo tutakavyokuwa tunatoa, hakuna kusema mlisema jumla hatukuelewa mnamsema nani. Hawa watu wanajulikana, waliokuwepo kwenye hizo nafasi 2020/2021 wanajulikana hakuna haja ya kuwapigia chapuo humu ndani kwa kuanza kutaja taja majina yao. *(Makofi)*

Majina yao yanajulikana yaendelee kubaki huko na sisi Wabunge hatuna haja ya kuanza kutaja majina yao

humu ndani ili na wao waonekane kuna Mbunge fulani hivi amewataja. Wakishatajwa hivyo wanajulikana ni kina nani. Kwa hiyo, nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Manyanya, mwaka huo wanajulikana waliokuwepo; na hata *TANROADS* naona imesemwa semwa sana hapa na wewe umesema kidogo, lakini inajulikana 2020/2021 nani alikuwepo, nani kafanya nini, kama yatakuwepo makosa. Kama hayapo hilo ni suala lingine. *(Makofi)*

Nataka niwatoe wasi wasi wananchi lakini pia na Bunge, kwamba hakuna jambo la jumla hapa, watu wanajulikana, waliofanya makosa, awe ni halmashauri awe ni Afisa Manunuzi awe ni nani, wanajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migila, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nami niweze kuchangia taarifa hizi za Kamati juu ya ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, nimeona Wabunge wengi wamezungumza kwa uzito ambao unastahili kabisa juu ya madhaifu yaliopo kwenye ripoti hii ya ukaguzi na hasa hatua kutochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Ningependa nizungumzie eneo la utaratibu mrefu wa manunuzi ya umma. Nitatoa mfano mmoja; kwenye miradi ya maji au miradi ya barabara, unakuta ule mlolongo wa kufanya taratibu za manunuzi unapishana na Mwaka wa Fedha wa Serikali. Tarehe moja mwezi wa saba, mpaka tarehe 30 mwezi June mwaka unaofuatia Serikali inakuwa imepanga mipango

yake, lakini unakuta sheria ya manunuzi inakwamisha baadhi ya michakato. Kwa mfano, halmashauri inaweza ikawa imepewa mradi wa maji au mradi wa barabara. Ni na mfano mmoja kule kwangu Mawengi kuna mradi wa maji ambao mikataba imesainiwa mwezi wa pili, lakini mpaka leo tunakwenda Disemba msamaha wa kodi kwenye ununuzi wa mabomba haujatoka. Kwa hiyo sasa tuangalie hizi sheria pia zisiwe zinatukwamisha katika kukamilisha miradi mbalimbali ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunakwenda kule tunawaeleza wananchi kwamba Serikali imeleta mradi huu hapa Mawengi lakini utaratibu wa kupata ule msamaha, kwa sababu sheria inataka miradi ya maji vile vifaa vipewe msamaha wa kodi. Tangu mwezi Februari mkataba unaingia mpaka Novemba *exemption* hiyo haijatoka. Kwenye miradi ya barabara pia hizo *exemption* zinachelewa sana. Kwa hiyo ukija kuangalia kwa mikoa yetu ile mvua zinaanza mwezi Oktoba mpaka mwezi Mei mwaka unaofuatia; kwa hiyo unakuta mkandarasi anakuwa na miezi miwili tu ya kufanya kazi. Anakuwa na mwezi Juni, Julai halafu hapo mwaka mwingine wa fedha unaanza. Kwa hiyo unakuta kuna kuwa na miradi mingi haikamiliki kutokana na sheria zetu kuwa na urasimu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri sana Serikali, ili kupunguza baadhi ya hoja tuangalie pia sheria yetu ya manunuzi na kuweza kuifanyia marekebisho. Hii inapelekea sasa miradi mingi; nitatoa hapa mfano mwingine; katika Kamati ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa tuliona kwamba kuna halmashauri 147 hazikupeleka fedha benki. Halmashauri 83 hazikuchangia bilioni saba kwenye vikundi vya wanawake, lakini kuna halmashauri 21 ambazo miradi yake ilikuwa imetelekezwa. Ukija

kufuatilia sababu za kutelekeza hii miradi na hayo mengine yote niliyoyasema, Serikali imeweza kupoteza jumla ya shilingi bilioni 74.

Mheshimiwa Spika, vitu vingine tunaweza kuwalaumu watendaji lakini hata sheria zetu nazo; naona Mwanasheria Mkuu anasikiliza vizuri, hiyo imenipa moyo kidogo; kwa hiyo tuangalie sheria zetu za manunuzi yale maeneo ambayo yana urasimu, yanatuchelewesha kukamilisha kazi kwa wakati, yanatuchonganisha Serikali na wananchi, tutuyafanyie kazi ili wananchi waweze kuwa na miradi ambayo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna changamoto moja ya kutokuwa na watumishi wa kutosha kwenye halmashauri zetu. Kwa mfano, Serikali inaweza ikawa imepeleka fedha labda bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la halmashauri au majengo ya hospitali. Anayeandika makisio ya gharama za ujenzi unaweza kukuta *sometimes* hana sifa. Tumeona kwenye taarifa humu, mtu ni *technician* anaandaa *BOQ* ambayo inahitaji mtu mwenye weledi mkubwa kitaaluma. Nishukuru mwaka jana, tulishauri TAMISEMI waliweza kupata wahandisi, hata mimi pale Ludewa nililetewa Mhandisi angalau mambo yanaanza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo utakuta ile *BOQ* mtu anakisia *materials* ambayo fedha nyingi inatumika kununua *materials* ambayo hatimaye yatabaki na mradi haukamiliki. Pia, tuangalie hizi fedha tunazopoteza; namuona Waziri wa Utumishi ananisikiliza; ile tuanita *wage bill*, tuangalie hizi fedha ambazo zinapotea huku. Tukija kuzijumlisha zote, hiyo ni mshaara wa watumishi wengi sana. Tutaweza kutatua tatizo la vijana wetu ambao wanalalamika ajira kila siku. Ukiweka *QS* pale, suala la

kuandaa *BOQ* mtu anakaa darasani anafundishwa na anafanya mazoezi ya kutosha, sio kila mmoja anaweza akaandaa hiyo *BOQ*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta Serikali inapeleka fedha nyingi kwenye halmashauri zetu, kwenye taasisi mbali mbali za umma; lakini kutokana kuwepo na baadhi ya watumishi wasio na weledi wanaopewa kazi hizo za kuandaa hayo hesabu tunapoteza fedha nyingi ambayo ingeweza kusaidia Watanzania wengi, ambapo sasa hivi kuna *crisis* ya ajira.

Mheshimiwa Spika, tukienda hata kwenye zile ofisi za mikoa (*RS*) nazo tuziangalie vizuri. Ukiona kuna mtumishi halmashauri msumbufu, mkorofi ana changamoto nyingi ndiyo sasa tuanamuhamishia tunampeleka *RS*. Kumbe *RS* ndiyo zina wajibu mzito, zina wajibu muhimu wa kusimamia halmashauri au Mkurugenzi muda wake umefika wa mwisho ametenguliwa uteuzi wake tunampeleka pale. Halafu hatuna watumishi wa kutosha kwenye hizi *RS*. Kwa hiyo tutawalaumu ma-*RAS* na Wakuu wa Mikoa, lakini hawana watumishi wa kutosha na wenye weledi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeiomba sana Serikali, ili kuokoa hizi fedha, kutoa thamani kwenye fedha hizi ambazo tunapeleka kwenye halmashauri na taasisi mbalimbali tungepeleka pia wataalamu wa kutosha na wenye weledi. Tunaweza tukaziongezea uwezo hizi *RS* ili ziweze kusimamia vizuri miradi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Ofisi ya *CAG* ina jukumu la udhibiti. Kuna Waheshimiwa Wabunge wamesema hili jukumu la uthibiti bado halijaonekana sawa sawa, zaidi wanakuwa kama polisi kama TAKUKURU, ambao wakati

mambo yamesharibika ndipo wanakwenda. Kumbe wana jukumu lingine la kuthibiti, kuzuia matatizo yasiweze kutokea. Tunaweza tukapunguza hoja nyingi sana eneo hili. Kwa hiyo ningeomba sana wale wataalam Ofisi ya *CAG* wajengewe uwezo ili wasiendelee kuwa tu kama mapolisi kwenda kukamata mwishoni watu wakishaharibu mambo.

Mheshimiwa Spika, wanaweza wakafanya ule ukaguzi wakati miradi bado inaendela kujengwa. Umepeleka fedha, msingi umejengwa waende wakague pale, watoe taarifa wataokoa fedha nyingi sana au wale wakaguzi wa ndani kule tukiwajengea uwezo mradi tusisubiri mpaka uishe mambo yaharibike zaidi, ndipo tunakwenda kukagua. Wangekuwa wanafanya ile *real time audit*, mradi unapokwa unaendelea mara kwa mara wanafanya ukaguzi na kutoa ripoti. Sasa mradi umekamilika mwaka huu *CAG* anakwenda mwakani tunapoteza sana fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu kufanya ni kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani hasa Mameya na Wenyeviti wa halmashauri, nao wana nafasi kubwa ya kuweza kuzuia na kupunguza hizi hoja za ukaguzi, hasa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kila mwezi taarifa ya mapato na matumizi inapelekwa kwenye Kikako cha Kamati ya Fedha, uongozi na mipango. Kwa hiyo, laiti wangekuwa wajengewa uwezo kuweza kusoma zile taarifa vizuri, kuzichambua vizuri na ukaguzi wa miradi, Kamati ya Fedha inafanya mara kwa mara; wajengewe uwezo, kama hawajengewi uwezo maana yake watakuwa wanapelekwa kwenye miradi kwenda kutembea na ku-*justify perdiem*. Tukiwajengea uwezo wataweze kubaini

kama dosari zipo eneo na kuweza kuchukua hatua kabla hata CAG hajaweza kwenda kuona hizo changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unakuta tunapoteza fedha nyingi sana ambazo zingeweza kwenda kwenye maeneo mengine. Pia, nimeona baadhi ya Wabunge wamechangia kuhusiana na bilioni 68 ambazo zimelipwa kama *penalty*. Hii ni fedha nyingi sana ambazo tungeweza kuzuia zisilipwe kama *penalty* na zingekwenda kutengeneza hata kilometa 100 za lami. Sisi kule Ludewa tunahangaika sana kipande kile cha kutoka Mawengi mpaka kwenda Manda, Mlima Kimelembe tumekuwa tukihangaika na bilioni 6 tu. Fedha hizi wananchi wanavyosikia itawatia uchungu sana. Naungana na Wabunge wote ambao wamesema tuchukue hatua kuzuia haya mambo kabla hayajatokea.

Mheshimiwa Spika, pia hii tabia ya kuchelewa kulipa wakandarasi tuiangalie kwa umakini sana. Jana nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wale wakandarasi waliopewa jukumu la kusambaza mbolea yaani wanafanya kazi wengine wanachuki kwa sababu kuna malipo ambayo nao wanadai kwa muda mrefu. Sasa, unakuta wanapaki lori kwa wananchi, anawalazimisha wananchi wote siku hiyo ndiyo waende kuchukua mbolea. Wananchi wanafika pale asubuhi na mapema, lori linafika usiku, wanakaa na njaa. Hii imetokea jana pale Lugarao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuangalie kwa makini sana. Hawa, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, walitakiwa wawe na maghala wameyafungua. Kwa sababu muda wa mwananchi kupata fedha haufanani; si kwamba wananchi wote watakuwa na fedha siku mmoja au wakati mmoja. Mwananchi akishahangaika

akiuza ulanzi wake na komoni akipata fedha ya mfuko mmoja aweze kuipta pale, na si kusubiri mpaka lori lije lipaki pale, wananchi wanateseka sana. Nashukuru jana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliweza kuchukua hatua; nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wale wandarasi wana kinyongo kwa kuwa baadhi ya madai yao hawajaweza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu jioni ya leo, kuwa nami ni miongoni mwa wanaochangia hotuba zilizopo mbele yetu kuhusu hizi Kamati zetu tatu. Tena nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai mpaka leo nipo humu ndani ya hili bunge.

Mheshimiwa Spika, nikiwa mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* ambapo umenitua hivi karibuni, ninakushukuru sana wewe kunipeleka kwenye hiyo Kamati, kiukweli ninashuruku sana.

Mheshimiwa Spika, nikiwa mjumbe wa Kamati ya *LAAC* ambao umenitua hivi karibuni, ninakushukuru sana wewe kunipeleka kwenye hiyo Kamati, kiukweli ninashuruku sana kwa sababu ninaenda kuifanyia kazi nchi yangu ambayo wananchi wamenituma.

Mheshimiwa Spika, kwenye kamati yetu kuna mambo mengi sana ambayo tumeyapitia, hasa hizi hoja za *CAG*. Ni mambo mengi sana yanasikitisha, *very very sad stories* hasa yanayofanyika kwenye hizi halmashauri zetu. Tumeangalia hoja nyingi ambazo kiukweli kama tutazifumbia macho, halmashauri zetu nyingi zinakwenda ku-*collapse*. Mbaya zaidi, wanaofanya yote haya yatokee mpaka sasa hivi wako ofisini wanakula kiyoyozi lakini bado wanatembelea *V8* zetu na mafuta yetu wanatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwenye 10% ya mapato ya ndani. Hili ni eneo ambalo halmashauri nyingi wanatumia kama mwanya wa kupiga hela za wananchi wetu. Serikali ilitunga hii sheria ili kuweza kuyasaidia haya makundi matatu ambayo hayana uwezo wa kukopesheka katika benki zetu. Kuna kundi la wanawake ambalo ni kubwa sana, haliwezi kukopesheka na wala hawana dhamana, kuna kundi kubwa la vijana, na kundi la walemavu. Hata hivyo, halmashauri zetu zilizo nyingi, kwa masikitiko makubwa zinatumia kama mwanya wa kuweza kuyaminya haya makundi yasiweze kupata hizi fedha kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ukipiga hesabu, hizi fedha kama zitasimamiwa vizuri, Shilingi bilioni 75, ni nyingi sana ambapo zingeenda kuwasaidia akina mama na vijana wakaondokana na umasikini. Katika hali ya kusikitisha, mfano hapa tukiangalia kuna halmashauri 17. Hizi halmashauri 17 zilitoa mikopo ya Shilingi 3,260,000,000/= bila kuzingatia uwiano. Tunajua kabisa sheria inasema ni 4:4:2 lakini wao kuna kundi moja wanalipendela zaidi. Tuangalie kabisa hili kundi ambalo linapendelewa lina athari kiasi gani na ambalo halipewi lina athari kiasi gani katika maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kundi la vijana; vijana sasa hivi ni wengi sana, *graduates* ni wengi sana, wako huko mitaani, hawana mikopo wanahangaika na bahasha kila kukicha. Bado hili kundi halipewi fungu lake kama inavyotakiwa. Kwenye ripoti ya *CAG* inaonesha kwamba vijana ndio hawapewi fedha kwa kiasi kikubwa kwa kigezo cha kwamba wana-*misuse* hizi fedha. Cha kushangaza, kwani ni lazima hawa vijana tuwape fedha? Ni ukweli kabisa kwamba ukiwapa vijana fedha, wanaweza wakazitumia ndivyo sivyo, lakini kwanini tu-*stick* katika aina moja tu ya mikopo?

Mheshimiwa Spika, kwenye halmashauri nyingi ukitembelea kule, hii mikopo kwa ajili ya vijana, unakuta ni boda boda tu; hivi hakuna *creativity* nyingine ya kuwasaidia hawa vijana zaidi ya kuendesha tu bodaboda? Tumeona kuna halmashauri moja vijana ambao wamesoma mambo ya *medicine* wameweza kuji-*organize* wakapewa mkopo wakaweza kufungua hadi kituo cha afya ambacho kimeenda kuajiri na watu wengine, lakini hawa watu wetu wa Maendeleo ya Jamii wanakosa ubunifu, wanashindwa kutoa elimu kwa watu wetu, matokeo yake vijana wetu wote wanakomalia mradi mmoja tu wa bodaboda. Kila siku ni bodaboda, mwisho wa siku zinakosa thamani huko kama vijijini, hata abiria hawapati na wanashindwa kupeleka marejesho. Matokeo yake kipengele cha kupeleka marejesho hakipo. Tunakuwa tunatoa hizi fedha, lakini mwisho wa siku hazirejeshwi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia pia *nature* ya utoaji wa hii mikopo, tunawapa *for free,* wanafikiria hizi fedha ni kama za *TASAF*. Kwa hiyo, hata kusema kama kuna *mechanism* ya kusaidia hizi fedha zirudi, na hizi fedha ni

*revolving,* hakuna. Kwa hiyo, ifikie mahali sasa Wizara iweke mkazo kuhakikisha kabisa hizi fedha zinakwenda kuwa ni zenye manufaa kwa vijana, akina mama na watu wenye ulemavu. Isifikie kwamba hizi fedha ni kama za *TASAF*, wanapewa *for free,* hakuna cha kurejesha. Ni lazima uwepo mkakati wa kuhakikisha hizi fedha zinarudi ili watu wengine waweze kukopesheka. Pia hizi fedha ziende zikawafikie hadi watu wa chini kabisa huko.

Mheshimiwa Spika, taarifa inaonesha wanaopewa hasa ni vijana na akina mama wa mijini. Kwani huko vijijini kwetu akina mama hawahitaji mikopo? Wanahitaji. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kupitia TAMISEMI, wahakikishe wanawasimamia na kutoa amri kwa hawa watu wa Maendeleo ya Jamii kuhakikisha hii mikopo inakuwa ni yenye tija kwa vijana wetu, akina mama na watu wenye ulemavu, na isiwe tu inaingia kwenye mifuko ya watu.

Mheshimiwa Spika, kuna halmashauri nyingine hata kutenga, hawatengi, na pia hawasimamii urejeshaji. Hicho ndiyo kinatumika kama kichaka. Unakuta watu hawarudishi, hawatengi au wanachukua zile zilizorudi kidogo ndiyo wanaenda kutoa kwenye awamu inayofuata. Hapana, hilo halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu uwekezaji wa mitaji ya Umma katika miradi ya halmashauri. Ni kweli kabisa ili halmashauri zetu ziweze kuendelea ku-*exist* ni lazima basi ziweke miradi ya aina mbalimbali ambayo itazifanya halmashauri zetu ziweze kupata mapato mengi na ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaona na ripoti inaonesha halmashauri nyingi sana zinafanya uwekezaji ambao hauna maana, unakwenda kuzitia halmashauri zetu

hasara, na yote haya yanasababisha hazifanyi upembuzi yakinifu vya kutosha, hata maandiko ya miradi hawafanyi. Unakuta kila halmashauri sasa kama ilivyosema ripoti, wanafaya uwekezaji kwa kuiga. Leo hii kila halmashauri ukienda ni soko na stendi. Sasa kama kila halmashauri kutakuwa kuna soko na stendi, leo hii hata bei za nauli zimepanda kwa sababu kunakuwa kila mahali kuna stendi.

Mheshimiwa Spika, leo dereva kila akiingia stendi lazima aache *tax*. Sasa huyu anayeendesha biashara ya mabasi, yeye atapata nini? Kwa maana hiyo lazima wampandishie nauli huyu mtumiaji wa mwisho, ambaye ni abiria, lakini yote haya ni kwa sababu tu tuna miradi ya kuigana. Kwa nini tusiwe na miradi ambayo itakuwa ni tofauti na ambayo inakwenda kuzalisha?

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaona kuna masoko hayazalishi chochote. Mfano Soko la Ndugai pale, ni *white elephant*. Tuna soko pale la Machinga *Complex,* ni *white elephant*. Sasa hivi eti imefikia, Soko la Ndugai limelazimishwa sasa daladala zote ziende zikashushe watu kule Ndugai. Hivi tuliandaa lile soko kwa ajili ya kupeleka abiria kule au wanunuzi? Yaani tunafanya fanya ilimradi ionekane kule kuna ka-*movement* ka watu. *Are we serious?* Hebu tu-*plan* vitu ambavyo vinakwenda kuliletea hili Taifa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la *NHIF*. Huku ndiyo kwenye majanga makubwa. *NHIF* ndiyo tunaiamini kama *tool* ya kutusaidia sisi wananchi tuweze kutibiwa pindi ambapo hatuna fedha. Jana tumeangalia tunakwenda kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo *NHIF* ndiyo atakuwa kingi wa kuweza kutuhakikishia afya zetu zinakuwa bora, lakini *NHIF*

imegundulika ina madudu mengi sana. Kwanza, inashindwa kurejesha fedha kwenye halmashauri zetu. Halmashauri zinatoa huduma kwenye vituo vyetu vya afya lakini yenyewe inashindwa kurejesha. Cha kusikitisha zaidi, ujazaji mbovu wa fomu unaofanywa kwenye hosipitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa watu wanafanya kazi *purposely* kurudisha nchi yetu nyuma au vipi? Kwa nini hawachukuliwi hatua? Wapo tu wamekaa ofisini, na mbaya zaidi tunaambiwa hapa; ukiangalia ukurasa wa nane pale unasema, yanafanyika hayo kwa sababu Serikali imeshindwa kuchukua haraka hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wanaobainika kuhusika na ubadhirifu. Serikali ndiyo chanzo cha haya. Tumeona watumishi wengi wanaofanya huu ubadhirifu Serikali ndiyo inawalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumehoji halmashauri nyingi. Watu wengi tunaowahoji; Maafisa Masuuli na Wahasibu, ukimwuliza anakwambia yuko pale kwa miezi miwili, mwaka mmoja au miaka miwili. Kwa maana hiyo, ni kwamba kuna kamchezo kanaendelea huko kwenye Serikali hasa TAMISEMI. Wanamhamisha mtu, wanampeleka sehemu nyingine. Huyo mtu ameshaharibu. Leo nemesema huyu mtu ni mwizi, ukimhamisha kutoka Halmashauri *A*, kumpeleka Halmashauri *B*, huo wizi atakuwa ameuacha? Kwa nini umhamishe? Kwamba mnakwenda sasa kumtoa kafara yule anayekwenda kwenye hiyo *post* au vipi? Kwa nini tuwalinde hao watu? Kwa nini Serikali isiwachukulie hatua?

Mheshimiwa Spika, eti hatua tunazowachukulia; tunamhamisha kutoka kituo *A* kumpeleka *B*. Tayari huyu

mtu ni mwizi, ni mbadhirifu, ataendeleza kufanya yale aliyokuwa anafanya Halmashauri *A*. Ifikie mahali tuonee uchungu hizi fedha. Wanapiga sana hizi fedha, lakini tunawalinda. Halafu mbaya zaidi juzi tunaambiwa kwamba, timu ya TAMISEMI imekwenda halmashauri fulani kuweka kambi. Siku zote mlikuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpaka madudu yafanyike ndiyo mnakwenda kuweka kambi. Kambi *for what?* Tunaweka kambi *for what?* Watu wameshapiga hela halafu tunawaangalia, tunawahamisha hamisha tu! Ifike mahali hawa watu walioiba fedha za Watanzania, fedha zinapotea, washughulikiwe. Siyo tu kuwahamisha kituo kimoja, watu wamepiga dili za mchongo sasa hivi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, kengele ilikuwa imeshagonga, lakini naona kuna taarifa hapa. Mheshimiwa Charles Kajege.

**T A A R I F A**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji, kwamba mkakati wa TAMISEMI kuhamishana siyo kwamba ni wajinga, hapana. Ni namna ya *protection*. maana yake ni kwamba anayeiba kwa sababu mkimbana kule wanaona dah, sasa tufanyeje? Wanamhamishia katika halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mifano mingi katika jimbo langu. Watu ambao ni wezi wamehamishiwa katika maeneo mengine. Nami nasema kesho, wale wote lazima wakamatwe. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa asilimia 100. Hawa watu tusiwachekee. Masuala ya kulindana tunamrudisha mama. Mama anahangaika kila kukicha, anatafuta fedha kwa ajili ya Watanzania halafu kuna watu wachache, tena Serikali eti inawalinda, wamrudishe mama nyuma, hatukubali kabisa. Tunaongea hapa, kesho tutashika shilingi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naona inabidi ajiandae bajeti ijayo, Shilingi imeshashikwa kabla hujaleta bajeti hapa ndani. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nawapongeze sana Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Wenyeviti wa Kamati zote tatu kwa kuleta ripoti hii ya uchambuzi wa kina kuhusu hii ripoti ya CAG.

Mheshimiwa Spika, naomba nitofautiane kidogo na Wabunge, wenzangu. Pengine utaniongoza; sijajua *role* yetu kama Wabunge ni ipi katika kuisimamia Serikali? Je, ni kuishauri Serikali tu na kuisimamia? Je, sisi kama Wabunge tuna hakika kwamba tunaisimamia vizuri? Ni nani asiyejua madudu yanayoletwa na sheria ya manunuzi kwenye halmashauri zetu? Nani hajui mwanya mkubwa wa fedha nyingi za nchi hii zinapotea kwa sheria ya manunuzi? Mbunge gani hajui? Tumefanya nini kwa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Wabunge wengi hapa wametoa mawazo kwamba twende tukawaazimie. Nitoe mfano mmoja, tunataka kumuazimia labda Mkurugenzi wa *TANROADS* kwa madudu mengi yanayofanywa, na ni kweli kwamba fedha nyingi zinapotea. Hivi ni kweli Mkurugenzi wa *TANROADS* amepoteza hizi fedha? Sisi kama Wabunge tunaamini Mkurugenzi wa wa *TANROADS* amepoteza hizi fedha?

Mheshimiwa Spika, unaweza ukamwita Mkurugenzi wa *TANROADS* akaja na *certificates* za wakandarasi tatu, nne au tano hazijalipwa. Nani awajibike? Nani anapaswa kuwajibika? Lazima sisi kama Wabunge twende mbali zaidi, siyo tu kuwalaumu watendaji. Wakati mwingine tukizungumza, watendaji wanasema, hawa Wabunge bwana, wanasiasa. Kwa sababu hawaoni tunachokifanya. Hawaoni kwa sababu haya mambo tunayazungumza kila siku.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapitia bajeti ya ujenzi hapa, hatukuona tumepitisha fedha kwa barabara zilizoisha? Barabara imeisha mwaka 2021 lakini tumepitisha fedha mwaka huu. Zinakwenda wapi?

Zinakwenda kulipa madeni ya Wakandarasi. Nani amezalisha madeni?

Mheshimiwa Spika, tuwe *serious* kuisimamia Serikali. Hivi ni nani hajui kwenye halmashauri zetu hakuna wahandisi wa kutosha? Katika kuchangia bajeti nilisema, halmashauri zetu hazina wahandisi. Tena wakati ule mimi nilijichanganya kati ya wahandisi na wakadiriaji majengo. Unaweza ukakuta kwenye halmashauri kuna mhandisi lakini hakuna mkadiriaji majengo? Nyumba ya kuingia bati 300, zinanunuliwa bati 400. Nyumba inaingia nondo 10, zinanunuliwa nondo 20. Hatuna mkadiriaji majengo, nani hajui? Nani awajibike?

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kumwajibisha Mwalimu Mkuu kwa sababu ujenzi wa shule hajausimamia vizuri. Tunakwenda kumwajibisha *DMO* kwa sababu kituo cha afya hakijajengwa vizuri, tuko sahihi? *Are we serious?* Tuna halmashauri ngapi zina wakadiraji majengo? Tuna halmashauri ngani zina wahandisi?

Mheshimiwa Spika, namwonea huruma sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi anayoifanya ni kubwa sana na dhamira yake ni njema sana na maono yake ni makubwa sana kwa nchi hii, lakini waliopata dhamana ya kumsaidia Rais wajipime. Kwa sababu akili yangu inakataal unakwenda kwenye halmashauri unakuta madudu.

Mheshimiwa Spika, halafu sasa ukiingia kwenye halmashauri kuna Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri anawajibika kwa Mkurugenzi. *Is it fair?* Yaani Mkurugenzi ampe mafuta na fedha kwenda kukagua mradi, aende akamkague; atampa? Mkurugenzi atampa usafiri Mkaguzi wa Ndani? Akishaenda kumkagua, hiyo ripoti

inasomwa wapi? Siyo sawa, kuna mahali tumepotea. Nashauri, Mkaguzi wa Ndani akae pembeni, awe ni taasisi inayojitegemea. Haiwezekani Mkaguzi wa Ndani akae chini ya Mkurugenzi, amkague Mkurugenzi, siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka *CAG* anatuletea madude haya, hivi ni kweli tunasema kwenye Wizara zetu hakuna wakaguzi? TAMISEMI, hakuna wakaguzi? Huku kwenye Maji hakuna wakaguzi? Ujenzi hakuna wakaguzi tumtegemee *CAG*? Haya madude yapo. Nasi kama Bunge siyo mara yetu ya kwanza kuyaona. Sio *CAG* peke yake ndio katuonesha! Haya madude yapo!

Mheshimiwa Spika, kuna shida mahali. Kama tuko *serious* kuna shida mahali. Tuchukulie mfano mwingine, kwenye majengo hayo hayo; hivi ni kweli *BOQ* ya kujenga darasa moja Dar es Salaam itafanana na ya Njombe? Ndiyo, tunataka majengo yetu yote yafanane kama vituo vya afya vyote; jengo linaweza kuonekana kwa ndani linafanana, lakini ile *BOQ* ya ndani ni kweli inafanana? Hivi Njombe leo unajenga darasa moja lina feni sita darasani. Umeshafunga mafeni, Njombe, ni kweli!

Mheshimiwa Spika, hayo madarasa yanajengwa Dar es Salaam kwenye joto, Njombe huwezi kuweka feni, lakini unaweza kukuta darasa limejengwa wanakwambia *BOQ* ndio inavyosema. Hivi Njombe unahitaji dirisha la futi sita kwa sita? Dar es Salaam unahitaji dirisha la futi sita kwa sita kwa sababu ya joto, kuna mahali tunakosea.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano kwenye halmashauri yangu, tumepewa milioni 470 kujenga madarasa. Juzi nilikwenda kukagua, madarasa yote yamekamilika, yote

yana feni zinafanya kazi wala umeme hatujui tutapata lini, lakini wamefunga mafeni na kila kitu, lakini hawajajenga choo, hela imeisha. Milioni 28 zimetumika kuingiza umeme kwenye madarasa lakini vyoo havijaisha. Mkurugenzi yupo, Mhandisi yupo, kila mtu yupo na hamna majibu. Ukiwauliza wanakwambia hiyo ndio *BOQ*, yaani usipofanya hivyo maana yake wewe kibarua chako kiko hatarini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umbali uliopo kutoka Liwale kwenda Dar es Salaam ambako wanatakiwa wakanunue vitu vya pamoja wamenunua mpaka *bulb*, wamekusanya kila kitu kiko stoo, lakini darasa haliwezi kutumika, shule haiwezi kufunguliwa, vyoo hakuna, jengo la maktaba hakuna, fedha zimeisha. Ukienda kuwakagua wametumia vizuri huwezi kuwashtaki. Ndio ile aliyosema kwamba mtu mwingine anaweza akafanya jambo zuri tu kwa nia njema likawa na faida, lakini kwa sababu hajafata Sheria ya Manunuzi akaadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, mwingine anaweza aka-*mess-up* akafanya madudu tu, lakini kwa sababu amefata Sheria ya Manunuzi anaoneka yuko *happy*. Sasa tufike mahali sisi kama Wabunge, sio tu kuishauri Serikali, twende tuisimamie na inaposhindwa kutekeleza maazimio yetu tuwe na la kufanya. Kama hatuna la kufanya, hapa tutakuwa kama tunapiga *story* tu, si sawa, kuna shida mahali.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, *MSD* inadaiwa na Serikali fedha nyingi tu, lakini halmashauri wanaidai *MSD*. Sasa ni wajibu wa Mkurugenzi *MSD* aamue fedha za halmashauri aendeshee taasisi yake, halmashauri wakose dawa au afanyeje sasa?

Mheshimiwa Spika, halmashauri wamepeleka fedha *MSD,* lakini Serikali hawajapeleka fedha *MSD,* Mkurugenzi atumie hela zipi kuendeshea ile taasisi? Shida ipo. Lazima kama tuko *serious* tufumue mifumo yote ya ukusanyaji wa fedha na utumiaji wa fedha, lazima tuwe makini kwamba, fedha tumekusanya kiasi gani, zinakwenda kufanya nini na anayetakiwa kuwajibika ni nani?

Mheshimiwa Spika, leo hii wakienda kumwajibisha Mkurugenzi wanawaonea tu, kule mahali kuna shida. Nimezungumzia Sheria ya Manunuzi, sasa narudi kwenye hoja za *CAG.* Nafikiri kama Bunge tufike mahali tuseme kama hoja imejirudiarudia ni mara ngapi na kwa muda gani? Tuweke kikomo. Lini hoja ifungwe? Tuweke kikomo na nani awajibike hoja isipofungwa? Vinginevyo *CAG* anakuja anakwambia hoja zisizofungwa za mwaka 2018 hizi hapa, hoja mpya ni hizi hapa. Nani ambaye amesababisha hoja hazijafungwa? Kwanza nani ameleta hiyo hoja ya ukaguzi? Kuna shida.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tunapopitisha bajeti lazima tuwe makini. Tunapopitisha bajeti Wabunge kama kweli tuko *serious* tuwe makini. Tunapopitisha bajeti ya miradi iliyokamilika lazima tuseme watuambie hizi hela zilichelewa wapi? Barabara imeisha 2018 lakini utakuta bado kwenye bajeti inatengewa fedha, ukiuliza deni la mkandarasi na haliishi, sisi Wabunge tunakubali tu. *GAG* akija kutustua tunakuwa wakali kwani hakuna kipya mimi ninachokiona hapo kwa *CAG* alichokileta. Vitu vyote ambavyo kila siku tunaviona, sisi tunabishana sana na Mheshimiwa Waziri wakati tunapitisha Bajeti ya Ujenzi tulibishana naye sana hapa. Akasema hizi fedha tulizopitisha mwaka jana hakuna mradi mpya

uliotekelezwa? Akasema hapana zile tumetekeleza mradi uliopita, hatukupitisha hapa? Sasa kitu gani kipya?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka kengele ya pili imegonga…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, asante.

**SPIKA:** Nisaidie mimi na wengine, nilikuacha umalize hoja yako ili utusaidie kufafanua, maana tunaelekea kuhitimisha hii hoja kesho na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu yuko hapa. Bunge hili na wewe ukiwemo humu ndani, ndio kazi tuliyofanya ama mimi sijaielewa vizuri hoja yako? Yaani kwamba bajeti ya ujenzi na uchukuzi iliyopitishwa na Bunge hili ilikuwa ni kwa ajili ya barabara ambazo zimeshakamilika? ndicho ulichosema ama mimi ndio nimekuelewa vibaya? Ndicho ulichokisema?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu hebu tusaidie.

**MHE. SELEMANI M. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, bajeti ambayo tuliipitisha mwaka jana, asilimia kubwa ya miradi haikutekelezwa na ndio maana Kamati ya Bunge ilileta na kulielezea Bunge kwamba miradi ambayo iliidhinishwa na Serikali na Bunge tukapitisha haikukamilika.

**SPIKA:** Sasa hapo maana hivyo ni vitu viwili tofauti, Bunge kupitisha bajeti na kutokutekelezwa ni jambo tofauti na kusema kwamba Bunge limepitisha bajeti kwa ajili ya mambo ambayo Serikali imeshakamilisha, hayo ni mambo mawili tofauti. Nataka kuelewa hapo kwamba Bunge na pia utusaidie ni hoja ya *CAG*? ili tuwe na uhakika pa kwenda kuipata hiyo taarifa kwamba tumepitisha barabara ambazo, yaani Bunge lilipitisha bajeti ya barabara ambazo zimeshakamilika tayari.

Mheshimiwa Kuchauka ni hoja ya *CAG* au ni hoja yako mpya?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ni hoja ya *CAG*. Nilichokuwa nazungumza labda sikueleweka. Nimesema hivi, hizi ripoti tunazozipata hapa za *CAG* siyo mpya. Kwa mfano, hiyo ripoti ukisema kwamba *TANROADS* wameingiza Serikali madeni ya riba, ni hoja ya *CAG,* lakini sisi kama Wabunge tumeliona hili kwa sababu mwaka jana wakati tunapitisha bajeti ziko fedha, nitoe mfano, barabara ya Mtwara-Mwivata kilometa 50 imeisha, lakini mwaka huu tunapitisha bajeti kuna fungu la fedha tumepitisha pale ukahoji wakasema ni za kulipa mkandarasi. Sasa iweje hoja hii ya *CAG* iwe mpya kwetu? kwamba sisi hilo deni limezalishwa kama vile hatujui kama Wabunge, hayo madeni yanavyozalishwa kama vile Bunge hatujui mpaka kuja kumwajibisha huyo Mkurugenzi wa *TANROADS* wakati sisi wenyewe tumeona.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC TANROADS* walikuja mbele ya Kamati ama hawakupata nafasi ya kuja mbele ya Kamati? Haya mmesimama Mwenyekiti na Makamu nani anataka kuzungumza, haya Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA- MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, *TANROADS* tuliwaita, tulikutana nao kwenye ripoti ya ufanisi na walikuja kwenye Kamati.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunaelekea sehemu nzuri na huko tunakoelekea lazima tujue tunaenda kufanya maamuzi ya aina gani kwa sababu pia tukiamua hapa hatutaka mtu yeyote akaonewe kwa sababu tutakavyokuwa tunatoa maagizo kwa Serikali hatutataka mtu yeyote akaonewe. Ili mtu asionewe ni kwamba alitokea mbele ya Kamati, Kamati inapotuletea humu ndani ni kwamba *CAG* kasema, Kamati imeona nab ado imeandika kwenye taarifa yake. Kwa hiyo hakuna taasisi ama mtu yeyote ambaye anajadiliwa hapa ndani ambaye pengine kwa namna moja au nyingine makosa yako sehemu nyingine. Kama ndivyo Kamati inapaswa kusema kwamba taasisi hii ilikuja na imefanya hivi.

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma Taarifa ya *PAC* inavyoielezea *TANROADS* sina uhakika kama hayo maelezo uliyosema ndicho inachosema Kamati. Kwa sababu kama Kamati haisemi hivyo maana yake tumeenda nje, tutakuwa tunaazimia nini? Lazima tuazimie kitu ambacho amesema *CAG* imesema Kamati na wamechangia Wabunge kuhusu Taarifa ya *CAG*.

Waheshimiwa Wabunge, sijui kama naeleweka. Sasa Mheshimiwa Kuchauka nilikuwa nakuuliza hayo maswali kwa sababu unatuweka katika mazingira ambayo Bunge hili ni kama vile hizi hoja si mpya kwa hiyo tuache tu ama? Ama kwamba siyo *TANROADS,* ili uende mbele lazima uongozwe. Bunge hili halijafanya uchunguzi, ukaguzi amefanya *CAG* ameleta taarifa, wahusika wakaitwa

mbele ya Kamati ndio hayo yanayotuongoza sisi kwenye kufanya maamuzi. Sasa tukianza sisi kusema kwamba tutaanza kuruka, tunakwenda mbali, mbali wapi ambako *CAG* hajafika, sasa tusaidie wewe, kule mbali unakotaka twende.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na maana kwamba kama nilivyosema hizi taarifa kwanza siyo mpya. Kwa mfano hizi taarifa za madeni ya wakandarasi kwa Bunge hili siyo mpya kwa sababu kwenye Kamati zilizungumzwa na tumehoji sana kwamba Serikali wana…

**SPIKA:** Ngoja ngoja, weka kisemeo chako vizuri ili tusikilizane ehe…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema maana yangu ni nini? Nimetolea mfano *TANROADS* kwamba haya madeni ambayo leo *CAG* amesema *TANROADS* wamezalisha madeni, wameliingiza Taifa hili kwenye madeni ya kutokana na riba. Mimi nikasema Bunge lako siyo jipya jambo hili kwa sababu hata tulipopitisha bajeti kuna vifungu tumepitisha vya kulipa wakandarasi kwenye miradi iliyokwisha miaka ya nyuma. Kwa hiyo kama ni Bunge tulitakiwa tuanzie pale kumwambia *TANROADS* umezalishaje hili deni? Sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, wao watupe sababu, wakishatupa sababu tusiporidhika tunakwenda mbele wao ndio wangetuongoza kwamba hili deni, mimi kama Mkurugenzi wa *TANROADS* nimeletewa *certificate* na mkandarasi tarehe hii nimepeleka Hazina *certificate* ya kwanza, *certificate* ya pili ni hii na ya tatu ni hii. Pale sisi sasa kama Bunge tungepata nafasi ya kwenda mbele

zaidi lakini leo tunaona hii taarifa kama mpya, kwamba haya madeni sisi tunayajua leo…

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kuchauka huo ni wakati gani ambao sisi kama Bunge tungeiuliza hiyo *TANROADS* ili tusogee mbele, ni wakati gani, wakati wa kipindi cha bajeti?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, *yes.*

**SPIKA:** Sasa hivi ndio tunaisimamia Serikali, wakati wa bajeti tunaishauri Serikali, inayo uwezo wa kusikiliza ama isisikilize. Wewe utaiita *TANROADS* wakati wa kipindi cha bajeti wakati Serikali inaongelea *ceiling, TANROADS* atasema nini? Sasa hivi tunaisimamia Serikali, kama upo upungufu mahali wao watautafuta, lakini haimaanishi sisi tusifanye kazi kwa sababu wakati wa bajeti hatukuiita *TANROADS* mbele yetu, siyo kazi yetu kuiita *TANROADS* kipindi cha bajeti. Ni kwa sababu *TANROADS* na yeye ana mipaka yake ya kazi. Kama isingekuwa hivyo basi tungekuwa tunaiita kila taasisi ije ijieleze yenyewe mbele yetu. Sasa Mawaziri wanafanya kazi gani humu ndani? Sijui kama umeelewa hoja yangu?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nimekuelewa vizuri sana.

**SPIKA:** Kwa hiyo ni sawasawa kabisa kwa Kamati yetu ya *PAC* kuleta hoja ambayo alikagua wakati huo maana hizi ni hesabu za 2020/2021. Bajeti ya mwaka huu tuliyoipitisha itakaguliwa na hesabu zile ambazo tutapewa na *CAG* mwaka wa kesho kutwa ndio atatueleza habari za bajeti ya mwaka huu. Sawa, atakapotueleza tutashughulika nazo kama tunaposhughulika nazo hizi sasa hivi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nimekuelewa.

**SPIKA:** Umenielewa vizuri?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nimekuelewa vizuri.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, sasa swali langu je, sisi kama Wabunge tukiona mianya ya mapato ya Serikali kuvuja, tusubiri Ripoti ya *CAG*?

**SPIKA:** Wewe ulikuwa unashauri tufanyeje tukishayaona?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, tuchukue hatua.

**SPIKA:** Wakati gani?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, *at any time* tatizo linapotokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka umesoma katiba vizuri ukajua mipaka yako? Maana pia Bunge siyo Serikali wala Bunge siyo Mahakama yaani kwamba wewe ukishaamua jambo lako basi ndio ushaamua kwa kuwa wewe ni Bunge, hapana. Kila mhimili una kazi yake na sisi kazi yetu ni hii tunayoifanya sasa, wakati ule hata ukiyaona unaishauri tu Serikali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Uliniuliza swali leo ndio nimepata swali humu Bungeni mimi la kwangu. Kwa hiyo Mheshimiwa Kuchauka ameniuliza swali angalau na mimi naingia kwenye historia. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaulizana haya maswali ili tutakapofika sehemu ya kufanya maamuzi basi tufanye maamuzi ambayo sote Wabunge tumeyaelewa na tunapofanya hayo maamuzi tutakuwa tunafanya maamuzi yakielekea kwenye chombo kingine. Kwa hiyo na yenyewe itabidi wakayafanyie kazi maana sasa hawatapata fursa ya kuja kulihoji Bunge kwamba unajua mliamua hivi lakini hiyo nafasi huwa haipo ndio maana wote tuko humu ndani ili Serikali nayo inachangia tutakapofika kwenye maamuzi basi watapaswa kuyafuata hayo.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana kwa michango yenu ambayo Wenyeviti watawashukuru kesho, lakini kwa niaba yao nawashukuru kwa sababu mnaendelea kuboresha mahitimisho yao ambayo watayatoa kesho na maazimio ambayo yatatuongoza Bunge kufanya maamuzi. Kwa kusema hivyo na leo tulitengua kanuni nataraji sote tunakumbuka, kwa hivyo tutaendelea na kikao chetu kingine cha Bunge kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.55 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 5 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*

# 4 NOVEMBA, 2022